
MASOMO YA BIBLIA YA SHULE SABATO

Watu wazima



# MASOMO KATIKA *Waraka wa Yakobo*

Gombo la. 100, Na. 4

**Oktoba – Desemba, 2024**

## YALIYOMO

1. **Ujumbe wa Mungu kupitia Yakobo......................................................5**

2. **Hekima kwa kukabiliana ...............10**

3. **Kukabiliana na majaribu ..............15**

4. **Kuweka Imani Katika Matendo ...20**

5. **Kushinda Upendeleo ......................26**

6. **Imani katika Matendo ......................31**

7. **Kuomba kabla ya kufungua vinywa vyetu...............................................36**

8. **Kuchagua nini cha kufikiri ...........41**

9. **Upole wa Hekima ..........................47**

10. **Kushinda Mtazamo wetu wa Matatizo.................................................52**

11. **Kufuata Mwonekano ......................57**

12. **Kuzingatia Mbinguni....................62**

13. **Kudumu kwa Imani...................... 67**

**Masomo ya shule ya Sabato** (USPS 005-118), Gombo la 100, Toleo No. 4, Oktoba – Desemba 2024. Imechapishwa na Baraza Kuu Ulimwenguni (GC) - Seventh Day Adventist Reform Movement, Idara ya Shule ya Sabato. Nakala zote© 2024, zinachapishwa, na kusambazwa na Reformation Herald Publishing Association, 5240 Hollins Road, Roanoke, Virginia 24019-5048, U.S.A. Virginia 24022-9993. nchini Marekani.

**USA na Canada**
Wasiliana nasi: Kwa namba 1-540-366-9400
Tovuti: www.reformationherald.com
E-Meil: info@reformationherald.org

**Imetafsiriwa na: SDA Reform Movement, Tanzania Mission, Idara ya shule Sabato, S.L.P 1342, DODOMA TANZANIA.**

**Masomo ya Biblia ya Shule ya Sabato** ni utaratibu wa mafundisho ya kila siku, msingi wake pekee ni juu ya Biblia na Roho ya Unabii pasipo maelezo ya nyongeza. Nukuu itolewe kwa ufupi kadri iwezekanavyo, ili kuelekeza ufahamu. [ ] Mabano huwekwa baadhi ya sehemu ili kusaidia kuelewa jambo kwa usahihi. Jifunze zaidi katika chanzo kilichopendekezwa.

# Utangulizi

Waraka wa Yakobo ni moja kwa moja. Jinsi tunavyohitaji jumbe ndani yake hivi sasa! Hivyo kwa muda wa miezi mitatu ijayo, wanafunzi wa shule ya shule ya sabato Ulimwenguni kote watakuwa wakijishughulisha na Masomo katika Waraka wa Yakobo. Mambo muhimu juu ya ushawishi wa ulimi (kwa mema au mabaya) utii kwa mungu kwa imani, nguvu ya maombi, na mfano wa Eliya ni wa haki. Mada chache muhimu. Kwa nini haya yote yanafaa sana leo?

"Dhambi ya zama hizi ni kupuuza amri za Mungu zilizo wazi. Nguvu ya mvuto kuelekea uelekeo potofu ni kubwa sana."—*Testimonies for the Church*, vol. 3, p. 483.

"Hebu wasiwepo watu wanaojidanganya kwa kuamini kwamba wanaweza kuwa watakatifu wakati wanavunja mojawapo ya matakwa ya Mungu kwa makusudi. Kuendekeza kutenda dhambi inayojulikana kunanyamazisha sauti ya Roho anayetushuhudia na kumtenga mtu mbali na Mungu. "Dhambi ni uvunjaji wa sheria." Na "kila atendaye dhambi [avunjaye sheria] hakumwona yeye wala hakumtambua." 1 Yohana 3:6. "—*The Great Controversy*, p. 472.

"Leo panahitajika sauti ya kukemea vikali; kwa maana dhambi kuu zimewatenganisha watu wa mungu. Kukosa uaminifu kumekuwa kama mtindo wa maisha. 'hatumtaki huyu atutawale,' ndiyo lugha ya maelfu ya watu. Luka 19:14. mahubiri laini yanoyohibiriwa mara nyingi hayaleti mguso wa kudumu; tarumbeta haitoi sauti fulani. Wanadamu haguswi mioyoni na ukweli ulio wazi wenye makali wa Neno la Mungu.

"Kuna watu wengi wanaodai kuwa Wakristo, ikiwa wangeonyesha hisia zao za kweli, wangesema, kuna haja gani ya kusema waziwazi hivyo? Wanaweza pia kuuliza, kwa nini Yohana Mbatizaji alilazimika kuwaambia Mafarisayo, 'Enyi wazao wa nyoka, ni nani aliwaonya ninyi kuikimbia hasira itakayokuja?' Luka 3:7. kwanini aliikemea hasira ya Herode kwa kumwambia Herode kwamba ilikuwa ni kinyume cha sheria kwake kuishi na mke wa ndugu yake? Mtangulizi wa Kristo alipoteza maisha yake kwa uwazi wake akizungumza. Kwa nini hangeweza kusonga mbele bila kutokubarika kwa wale waliokuwa wakiishi katika dhambi?

"Kwa hiyo watu wanaopaswa kusimama kama walinzi waaminifu wa sheria ya mungu wamebishana, mpaka sela imechukua nafasi ya uaminifu, na dhambi inaendelea bila kukemewa. Ni lini sauti ya karipio la uaminifu litasikika tena kanisani?"—*Prophets and Kings*, pp. 140, 141.

"Utoshelevu umewekwa kwa kila kwa kila mwana na binti ya Adamu kupata kujuakwa ubinafsi mapenzi ya Mungu, kuikamilisha tabia ya Kikirsto na kutakaswa kupitia ukweli."—*Testimonies for the Church*, vol. 2, p. 644.

Kwa kweli tunahitaji msaada wa mungu na tunahakikishiwa waziwazi kwamba " Kwa kila maombi ya dhati yanayowekwa kwa imani kwa lolote, majibu yatarudishwa. Huenda yasije kama tulivyotarajia; lakini yatakuja, si labda kama tulivyopanga, lakini wakati ule tunapoyahitaji sana."—*Ibid.*, vol. 3, p. 209. Amen!

***Idara ya shule ya sabato GC***

## Sadaka za sabato ya kwanza kwa ajili ya kanisa dogo lililoko Reading, Pennsylvania, Marekani.




Field ya Mashariki mwa Marekani (EUSF) imegawanyika katika maeneo Pennsylvania-8081Allentown78 nane ya kijiografia yanayo-jumuisha majimbo Pennsylvania, New York, Reading, Connecticut, Rhode Island, Massachusetts, Maine, Vermont, Harrisburg, New hampshire. Katika kazi Pennsylvania kwa sasa in-akua kwa haraka.

Inakadiriwa kwamba zaidi ya watu 53% katika Baltimore jimbo hili ni watu wa kidini wanaojumuisha Wamethodisti, Walutheri, Wabaptisti, Wapentekost, na wengineo, wakiwa na wakato-liki28.3%

Katika siku za awali za ukoloni, Pennsylvania ilikuwa mahali pa kukimbilia kwa wahamiaji wanaotafuta uhuru wa kidini ili kuepuka mateso huko Ulaya. Historia hii bado inaonekana katika idadi kubwa ya waumini wa Jadi wa Amish ambao wanaendelea kukaa katika shamba kubwa katika jamii yote ya kata ya Lancaster, wakiwa wamevalia mavazi ya kawaida na kusafiri kwa farasi na gari la kubebea watu.

Kwa miaka mingi, washiriki wachache wa SDARM wame-ishi Pennsylvania na mafunzo ya umisionari yalitolewa hapa pia. Lakini uamsho wa sasa wa kupendezwa na ukweli uliopo ulianza mwaka wa 2016 katika jiji la Reading baada ya washiriki wawili kuhamia hapa kuto-ka New York. Kikundi kilipanuka na kuanza kukutana kila sabato alasiri, kikikusanyika katika bustani wakati wa kiangazi na kwenye nyumba ya dada wakati wa majira ya baridi kali. Baada ya miezi kadhaa ya kujifunza, wengi walibatizwa katika imani ya matengenezo.

Reading kuna idadi ya watu 95,000 na ni kituo cha kutengeneza vifaa vya umeme, vifaa vya matibabu, teknologia ya kuhifadhi nishati na zaidi. Kanisa letu hapa sasa ndio kubwa zaidi katika jimbo la Mashariki mwa Marekani.. Nafsi mpya zaidi zinatayarishwa kujiunga na watu wa mungu. Kwa sasa, tunaabudu katika kituo cha kukodi na tungependa kuthibitisha uwepo wetu kwa ajili ya kukua kwa kuwafikia walio nje zaidi. “popote pale kundi la waumini linapoinuliwa, nyumba ya ibada ijengwe….

”Katika sehemu nyingi ambapo ujumbe umehubiriwa na nafsi zime-hubiriwa wamekubali, wako katika mazingira machache, na wanaweza kufanya kidogo tu kupata manufaa ambayo yangeipa kazi tabia. Mara nyingi hii inafanya kuwa ngumu kupanua kazi.” —*Evangelism*, p. 376.

Kwa hivyo, tunawasihi ndugu zetu na washirika kutoka duniani kote ili kutusaidia kuendeleza nyumba ya ibada katika eneo la Reading, ili roho nyingi zaidi ziweze kuletwa zizini. Ukarimu wako mzuri utathaminiwa sana, na Bwana atakubariki nawe.

***Ndugu zenu kutoka Field ya Marekani Mashariki***

**Somo la 1** **Sabato, Octoba 5, 2024**

# Ujumbe wa Mungu kupitia Yakobo

**FUNGU LA KUKARIRI: "Yakobo, mtumwa wa mungu, na wa bwana yesu kristo, kwa kabila kumi na mbili waliotawanyika; salamu. " (Yakobo 1:1).**

"Hakuna mtu, hakuna taifa, lililo kamilifu katika kila tabia na wazo. Mtu lazima ajifunze kutoka kwa mtu mwingine. Kwa hiyo Mungu anataka mataifa tofauti kuchangamana pamoja, kuwa katika kusudi moja, na katika nia moja. Ndipo umoja uliomo ndani ya Kristo utakuwa umeigwa. " —*Testimonies for the Church*, vol. 9, pp. 180, 181.

**Inapendekezwa kusoma:** *Testimonies for the Church,* vol. 9, pp. 190–203.

## *Jumapili* *Septemba 29*

### 1. WANAFUNZI WA KRISTO

**a. Watu watatu walioitwa "Yakobo" ambao walihusishwa na kristo walikuwa nani na ni yupi tunayemwona kwa kawaida? Mathayo 10:2, 3; 13:55.**

---

**b. Taja nyakati maalum na Yesu ambazo Yakobo, ndugu yake Yohana, alipitia. Luka8:51–55;Mathayo17:1,2;Marko14:32–34.**

---

"Yohana, mwana wa Zebedayo, alikuwa mmoja wa wanafunzi wawili wa kwanza kumfuata Yesu. Yeye na kaka yake Yakobo walikuwa wamekuwa miongoni mwa kundi la kwanza la watu waliokuwa wameacha vyote kwa ajili ya kumtumikia. Kwa furaha walikuwa wameziacha nyumba na marafiki kusudi wawe naye; walikuwa wametembea na kuzungumza naye, walikuwa wamekuwa naye mahali pa faragha, na katika mikusanyiko ya hadhara. Alikuwa ameondosha hofu zao, akawaokoa na hatari, akatuliza maumivu yao, akafariji huzuni zao, na kwa uvumilivu na upendo akawafundisha, hadi mioyo yao ikaonekana kama vile imeunganishwa naye, na katika hisia za upendo wao walitamani kuwa karibu zaidi naye katika ufalme wake. " —*The Desire of Ages*, p. 548.

"Karibu na mahali pa kuingilia bustanini, Yesu aliwaacha wanafunzi pale isipokuwa watatu, akiwataka wajiombee na kumwombea na Yeye. Aliingia katika faragha za bustani ile akiwa pamoja na Petro, Yakobo na Yohana. Hawa watatu walikuwa watu wa karibu sana wa Kristo.… sasa katika pambano lake kuu, Yesu alitaka wawe karibu yake. Mara nyingi walikuwa naye usiku mzima mahali hapa. Katika nyakati hizo, " —*Ibid.*, p. 686.

## 2. KUNYWEA KIKOMBE

**a. Elezea lengo la awali la Yakobo, mwana wa Zebedayo, pamoja na ndugu yake, Yohana. Marko 10:35–38.**

---

---

"Katika kila nafasi iliyowezekana, Yohana alikuwa katika nafasi iliyofuata baada ya Mwokozi, na Yakobo alitamani kuheshimiwa kwa kuwa karibu sana na Mwokozi.

"Mama yao alikuwa mfuasi wa Kristo, na alikuwa amemhudumia kwa vitu vyake bure. Akiwa na upendo wa umama na shauku kwa wanawe, alitamani wapate nafasi ya juu katika ufalme ule. Aliwahamasisha waombe jambo hilo.

"Mama na wanawe hao kwa pamoja walikuja kwa Yesu, wakiomba kwamba awape ruhusa waomba kile mioyo yao ilichotaka kuomba.

"Mwataka niwafanyie nini?" Aliuliza.

Mama akajibu, "Agiza kwamba hawa wanangu wawili waketi mmoja mkono wako wa kuume, na mmoja mkono wako wa kushoto, katika ufalme wako."

"Yesu akawavumilia kwa upendo, pasipo kukemea ubinafsi wao kwa kile kitendo chao cha kutafuta upendeleo zaidi ya ndugu zao wengine. Alisoma mioyo yao, akajua kina cha mafungamano yao na Yeye. Upendo wao si wa kibinadamu tu; ingawa wamenajisiwa na mambo ya kidunia ya njia za kibinadamu, upendo wao ule unatiririka kutoka katika chemchemi ya upendo wake uokoao. Hataki kukemea, bali kuwaongezea kina na kuwafanya kuwa safi. Alisema, "Mwaweza kunywea kikombe ninyweacho mimi, au kubatizwa ubatizo nibatizwao mimi?"

Wakakumbuka maneno yake ya fumbo, yaliyokuwa yakielekeza kwenye majaribu na mateso yake, lakini bado wanajibu kwa kujiamini, "Twaweza." Walihesabu kama ni kuonyesha heshima kubwa kwa kuthibitisha utii wao kwake katika kushiriki mambo yote yatakayompata Bwana wao.

"Kikombe ninyweacho mimi mtakinywea, na ubatizo nibatizwao mimi mtabatizwa," alisema; mbele yake kukiwa na msalaba badala ya kiti cha enzi, na wanyang'anyi wawili ndio wangekuwa naye upande wake wa kulia na wa kushoto. "—*The Desire of Ages*, pp. 548, 549.

**b. Kama vile kristo alivyokuwa ametabiri, ni nini kiliwapata Yakobo na ndugu yake, Yohana, baada ya kupaa kwa Bwana? Matendo12:1, 2; Ufunuo 1:9.**

---

---

"Yohana na Yakobo wangeshiriki mateso ya Bwana wao, mmoja, akiwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wote kufa kwa upanga; na mwingine, mtu aliyepitia masumbufu, mashutumu na mateso." —*Ibid.*, 549.

## 3. NANI ALIANDIKA WARAKA HUO?

**a. Uvuvio unaelezeaje Yakobo, mwana wa Alfayo - mmoja wa wale kumi na wawili (lakini si Zebedayo ndugu wa Yohana)? Marko 15:40.**

"Kulikuwa na Mlawi Mathayo mtoza ushuru, aliyeitwa kutoka katika maisha ya shughuli za biashara, na kutii Rumi; Simoni mwenye bidii, adui asiyebadilika na mamlaka ya kifalme; msukumo unaojitosheleza, uliwachangamsha Petro pamoja na Andrea ndugu yake; Yuda Myahudi, aliyepambwa, mwenye uwezo, na mwenye roho mbaya; Filipo na Tomaso walikuwa waaminifu na wenye bidii, lakini wenye mioyo mizito kuamini; Yakobo mdogo na Yuda, ambao hawakuwa mashuhuri kati ya ndugu, lakini ni watu wa nguvu, wenye msimamo mzuri katika makosa yao na Katika fadhila zao; Nathanael, mtoto mwenye unyofu na uaminifu; na wana wa Zebedayo wenye kutaka makuu, wenye mioyo ya upendo."—*Education*, pp. 85, 86.

**b. Kwa nini kuna uwezekano kwamba mwandishi wa waraka wa Yakobo (anayejulikana kama mtume kwani alimjua Bwana ana kwa ana) angekuwa ndugu wa kambo wa Kristo na maelezo yake mwenyewe yanaonyeshaje kwamba tabia yake ilikuwa imebadilishwa na ushawishi wa Bwana? Yakobo 1:1 (nusu ya kwanza).**

"Kristo hakueleweka na ndugu zake; kwani hakuwa kama wao. Alifanya kazi kutuliza kila kisa cha mateso alichoona, na kila wakati alifanikiwa. Alikuwa na pesa kidogo za kutoa, lakini mara nyingi alitoa chakula chake cha unyenyekevu kwa wale ambao alifikiria kuwa wahitaji zaidi kuliko yeye mwenyewe. Ndugu zake walihisi kwamba mvuto wake ulikwenda mbali ata kuingilia mvuto wao; kwani walizungumza kwa ukali kwa masikini, na roho zilizo dhalilishwa, Kristo aliwatafuta hawa, na akasema maneno ya kutia moyo kwao. Ikiwa wakati wa mzunguko wa familia, hakuweza kufanya chochote zaidi, angeweza kimya kimya na kwa siri iwezekanavyo, kuwapa viumbe wanyonge ambao alikuwa akijaribu kuwasaidia, kikombe cha maji baridi, na kisha kuweka chakula chake mwenyewe mikononi mwao. "—*This Day With God*, p. 59.

**c. Paulo alionyeshaje heshima yake kwa Yakobo, ndugu wa Yesu, Wagalatia1:17–19; Matendo21:18.**

## 4. KUFAFANUA BAADHI YA MATATIZO

**a. Ni nini kinachoonyesha kwamba Yakobo, ndugu wa Kristo, alikuwa mtu mwenye ushawishi katika baraza muhimu katika kanisa la awali? Matendo 15:5, 6, 13, 19, 20.**

“Kwa mfano huu Yakobo anaonekana kuchaguliwa kuwa ndiye atangaze uamuzi uliofikiwa na baraza. Ilikuwa ni hukumu yake kwamba ni sheria, na hasa sheria ya tohara, isihimizwe juu ya Mataifa, au hata kupendekezwa kwao. Yakobo alitaka kuvutia akili za ndugu zake na ukweli kwamba, katika kumgeukia Mungu, watu wa Mataifa walikuwa wamefanya badiliko kubwa katika maisha yao na kwamba tahadhari nyingi zitumike ili wasiwasumbue kwa maswali yenye kutatanisha na mashaka ya umuhimu mdogo, wasije wakakata tamaa katika kumfuata Kristo. ”—*The Acts of the Apostles*, p. 195.

**b. Madai gani ya kawaida lakini yenye makosa yanakanushwa na jukumu kuu la Yakobo katika baraza hili muhimu? Mathayo 16:18.**

“Yakobo aliongoza baraza, na uamuzi wake wa mwisho ulikuwa, ‘kwa hiyo hukumu yangu ni, tusiwasumbue hao watu wa Mataifa wamemgeukia Mungu.’

“Hii ilimaliza mjadala. Katika tukio hili tunakanusha fundisho lililoshikiliwa na Kanisa Katoriki la Roma kwamba Petro alikuwa mkuu wa Kanisa. Wale ambao, wakiwa mapapa, wamedai kuwa waandamizi wake hawana msingi wa kimaandiko wa kujidai kwao. Hakuna kitu katika maisha ya Petro yanatoa kibali kwa dai kwamba aliinuliwa juu ya ndugu zake kama makamu aliye juu zaidi. Ikiwa wale waliotangazwa kuwa warithi wa Petro walikuwa wamefuata mfano wake, siku zote wangeridhika kubaki katika usawa na ndugu zao. ”—*Ibid.*, pp. 194, 195.

“Mwokozi hakuikabidhi kazi ya injili kwa Petro kama mtu binafsi. Wakati fulani baadaye, alirudia maneno yale aliyoambiwa Petro akiyatumia kwa kanisa. Kitu kile kile kilisemwa kwa wale kumi na wawili kama wawakilishi wa jamii ya waamini. Ikiwa Yesu alikuwa amekasimisha madaraka rasmi yoyote kwa mmoja wa wanafunzi wake, tusingetarajia kuwakuta mara kwa mara wakibishana kuhusu nani awe mkubwa wa wote. Wangetii matakwa ya Bwana wao, na kumheshimu yeye ambaye alimchagua. ”—*The Desire of Ages*, p. 414.

## *Alhamisi* — *Oktoba 3*

### 5. ISRAELI YA MUNGU

**a. Waraka huu umeandikwa kwa nani na unawahusishaje wote wanaomkubali Yesu kuwa Bwana? Yakobo 1:1 (nusu ya pili); Wagalatia 3:27–29.**

---

"Miongoni mwa Israeli ya Mungu wangehesabiwa wengi ambao hawakuwa wazao wa Abrahamu kwa jinsi ya kimwili. "—*Prophets and Kings*, p. 367.

"Maisha ya Kristo yalianzisha dini ambayo ndani yake hakuna tabaka, dini ambayo kwayo Myahudi na Myunani, walio huru na wafungwa, wameunganishwa katika udugu wa pamoja, sawa mbele za Mungu."—*Testimonies for the Church*, vol. 9,p. 191.

"Ukristo hufanya kifungo chenye nguvu cha muungano kati ya bwana na mtumwa, mfalme na mtawaliwa, mhudumu wa mwinjilisti na mdhambi aliyedhalilishwa ambaye amepata kutakaswa dhambi zake katika kristo."—*The Acts of the Apostles*, p. 460.

**b. Katika unabii, ni jina gani linalopewa Israeli ya mwisho wa kiroho na uzoefu wao unaelezwaje kabla tu ya kurudi kwa Kristo? Ufunuo 7:4.**

---

"Mara tulisikia sauti ya Mungu kama ya maji mengi, iliyotujulisha siku na saa ya kuja kwa Yesu. Watakatifu walio hai, 144,000 kwa idadi yao, waliifahamu na kuielewa sauti, wakati waovu wakidhani ni radi na tetemeko la ardhi….

"144,000 wote walikuwa wamepigwa mihuri na wameunganishwa kikamilifu. Kwenye paji la uso wao palikuwa na maneno Mungu, Yerusalemu Mpya, na nyota tukufu iliyo na jina jipya la Yesu. Katika hali yetu ya furaha na takatifu waovu walikuwa wamekasirika, na walitamani kutukimbilia ili watukamate na kututia gerezani, ambapo tulinyosha mkono kwa jina la Bwana, na wakaanguka chini bila msaada wowote. Ndipo sinagogi la Shetani likatambua kwamba Mungu alikuwa ametupenda sisi ambao tungeweza kuoshana miguu, na kuwasalimu ndugu kwa busu takatifu, hivyo wakaabudu miguuni mwetu."—*Testimonies for the Church*, vol. 1, p. 59.

## *Ijumaa* — *Oktoba 4*

### MASWALI TAFAKARI BINAFSI

1. **Yakobo, mwana wa Zebedayo, alikuaje akawa kama kristo zaidi?**
2. **Yakobo, ndugu wa kambo wa Yesu, alikuaje na kuwa kama kristo zaidi?**
3. **Ni uthibitisho gani katika maandiko unaoonyesha kwamba Petro hakuwa mtume mkuu?**
4. **Paulo anaelezeaje umoja na thamani sawa ya Wkristo wote?**
5. **Ni nini kinachoonyesha ushindi wa mwisho kabisa wa Israeli wa roho wa mungu?**

**Somo la 2** **Sabato, Oktoba 12, 2024**

# Hekima ya Kukabiliana

**FUNGU LA KUKARIRI: "Lakini mtu wa kwenu akipungukiwa na hekima, na aombe dua kwa Mungu, awapaye wote, kwa ukarimu, wala hakemei; naye atapewa. (Yakobo 1:5).**

"Huhitaji kwenda hata mwisho wa dunia kwa ajili ya Hekima, kwa maana Mungu yuko karibu. Sio uwezo ulionao sasa au utakaowahi kuwa nao ndio utakaokupa mafanikio. Ni yale ambayo bwana anaweza kukufanyia…. Anatamani kukupa ufahamu katika mambo ya kimwili na ya kiroho. Anaweza kunoa akili. Anaweza kutoa busara na ujuzi. Weka talanta zako katika kazi, mwombe Mungu hekima, na utapewa."—*Christ's Object Lessons*, p. 146.

**Inapendekezwa kusoma:** *Testimonies for the Church,* vol. 1, pp. 120, 121; vol. 2, pp. 232–235.

## *Jumapili* *Oktoba 6*

### 1. KUOMBA KWA HEKIMA

**a. Kwa nini tunahitaji zaidi hekima ya kibinadamu maishani, na tunaweza kuipata kwa jinsi gani? Yakobo1:5.**

"Tunahitaji kuwa na ujasiri mdogo sana katika kile ambacho mwanadamu anaweza kufanya na kujiamini zaidi katika kile ambacho mungu anaweza kufanya kwa kila nafsi inayoamini. Anatamani ili mpate kumfuata kwa imani. Anatamani sana wewe utazamie mambo makubwa kutoka kwake. —*Christ's Object Lessons*, p. 146.

"Kusikia tu mahubiri ya sabato baada ya sabato, kusoma Biblia san, maelezo yake mstari kwa mstari, hautatufaidisha sisi au wale wanaotusikia, isipokuwa tukileta kweli za Biblia katika uzoefu wetu binafsi. Ufahamu, nia, mapenzi, lazima yakabidhiwe kwa udhibiti wa neno la Mungu. Kisha kupitia kazi ya Roho Mtakatifu maagizo ya neno yatakuwa kanuni za maisha.

"Unapomwomba Bwana akusaidie, mheshimu Mwokozi wako kwa kuamini ili upate baraka zake. Nguvu zote, hekima zote, ziko chini ya amri yetu. Tunapaswa kuomba tu."—*The Ministry of Healing*, p. 514.

## 2. KUIMARISHWA KWA IMANI

**a. Tutafaidikaje ikiwa tunaiona hekima ya Mungu kuwa bora zaidi kuliko yetu, hata katika mambo ya kawaida ya maisha? Mithali 3:3–8.**

“ ‘Lakini mtu wa kwenu akipungukiwa na hekima, na aombe dua kwa Mungu, Awapaye wote kwa ukarimu, wala Hakemei; naye Atapewa.’ Ahadi kama hiyo ni ya thamani kuliko shaba au dhahabu. kama kwa unyenyekevu wa moyo tutatafuta uongozi wa Mungu katika kila tatizo na mashaka, Neno Lake lakiri kwa ahadi kwamba utapokea jawabu la neema. Na Neno Lake haliwezi shindwa. Mbingu na nchi zitapita lakini Neno Lake halitapita. Mwamini Mungu na kamwe hautashindwa wala kuaibika. „Ni vema kumtumainia Mungu kuliko kuwatumainia wanadamu. Ni heri kumkimbilia Bwana, kuliko kuwatumainia wakuu”

“Haijalisha nafasi yoyote ya maisha au nyadhifa yoyote tutakayokuwa nayo, ama shughuli yoyote tutakayofanya, tunapaswa kuwa wanyenyekevu vya kutosha kutambua kuhitaji kwetu msaada, tunapaswa daima kuegemea kabisa katika mafundisho ya Mungu, tukitambua na kukiri majaliwa utoaji/Yake Wake wa kila kitu na kuwa waaminifu kumimina roho zetu kwa maombi. Zitegemee akili zako mwenyewe ndugu mpendwa, unapotembea katika maisha ya ulimwengu huu, nawe utavuna huzuni na kukatishwa tamaa. Mtegemee Mungu kwa moyo wako wote, naye ataongoza hatua zao katika hekma, na maslahi yako yatakuwa salama katika ulimwengu huu na ule ujao. Unahitaji nuru na maarifa. Waweza kuchukua mashauri ya Mungu ama ya moyo wako; waweza kutembea katika cheche za moto uliouwasha wewe mwenyewe ama utatembea katika nuru ya Bwana kutoka kwa Jua la Haki. ”—*Testimonies for the Church*, vol. 5, p. 427.

**b. Kwa nini tunahitaji kujiondoa wenyewe kutoka kwa kutegemea sana watu wengine kwa mwongozo? Yeremia17:5–8.**

“Mashaka yanapotokea, na matatizo yanapokukabili, usitafute msaada kwa wanadamu. Mtumainie yote kwa Mungu. Kitendo cha kuwaambia wengine magumu yetu hutufanya tu kuwa dhaifu, na haileti nguvu kwao. Inaweka juu yao mzigo wa udhaifu wetu wa kiroho, ambao hawewezi kuutatua. Tunatafuta nguvu za mwanadamu mpotovu, mwenye kikomo, wakati tunaweza kuwa na nguvu za Mungu asiyekosea, asiye na kikomo. ”—*Christ’s Object Lessons*, p. 146.

## 3. KUKUZA UIMARA ZAIDI

**a. Ni sharti gani tunapaswa kutimiza kabla ya Bwana kujibu maombi yetu? Yakobo 1:6 (sehemu ya kwanza); Marko 11:24. Elezea mfano mmoja wa jinsi tunavyoweza kuamua kusitawisha nguvu katika jambo hili. 1 Wakorintho 6:3–5.**

---

---

"Lakini ni wachache wanaotambua majukumu yaliyo juu ya watumishi wachache wanaobeba mizigo katika kazi hii. Ndugu huwaita mara kwa mara watu hawa kutoka kazini ili kushughulikia maswala yao madogo-madogo, au kusuluhisha kesi ya kanisa, ambavyo wanaweza na wanapaswa kushughulikia wenyewe."Ikiwa mmoja wenu hukosa hekima, na aombe kwa Mungu, ambaye huwapa wote kwa ukarimu, na hakemei; naye atapewa. Lakini na aombe kwa imani, hakuna anayeyetetereka."Lazima awe na bidii na mwenye mstahimilivu. Ikiwa hana msimamo, mwenye mashaka daima ikiwa Bwana atafanya kama alivyoahidi, hatapokea chochote.

"Wengi hutazamia wahudumu wao kuwaletea nuru kutoka kwa Mungu, wakionekana kufikiria hii ni njia rahisi kuliko kujipa shida ya kwenda kwa Mungu moja kwa moja kwa ajili yao wenyewe. Hao hupoteza sana. Ikiwa wangemfuata kila siku Kristo na kumfanya kuwa kiongozi na mshauri wao, wangeweza kupata ufahamu bora wa mapenzi Yake, na hivyo kupata uzoefu wa thamani. Kwa kukosa uzoefu huu, ndugu hawa wanaokiri kweli wanaota mioto ya wengine; hawamjui Roho wa Mungu na hawana ujuzi wa Mapenzi yake, na kwa hivyo huhamishwa kwa urahisi kutoka kwa imani yao. Hawana msimamo, kwa sababu waliamini wengine kupata uzoefu kwa niaba yao."—*Testimonies for the Church*, vol. 2, pp. 643, 644.

**b. Mtu anayedai kuwa Mkristo analinganishwa na nini ambaye imani yake huanza kuyumba? Yakobo 1:6 (sehemu ya mwisho); Mwanzo 49:4 (sehemu ya kwanza). Tunawezaje kuepuka hii?**

---

---

"Imani ya Wakristo wengi itayumba ikiwa watapuuza kila mara kukutana pamoja kwa mkutano na sala."—*Ibid.*, vol. 4, p. 106.

"Chukua neno la kristo kama Uthibitisho wako. Je! Hajawaalika mje kwake? msiruhusu kamwe kuzungumza kwa njia isiyo na tumaini, kwa namna ya kukata tamaa. Kama mkifanya hivyo mtapoteza sana tumaini. Kwa kuangalia mwonekano na kulalamika matatizo na magumu yanapowapata, mnatoa uthibitisho wa imani iliyo dhaifu. Zungumza na kutenda kana kwamba imani yako haiwezi kushindwa."— *Christ's Object Lessons*, pp. 146, 147.

## 4. KUEPUKA MOYO ULIOGAWANYIKA

**a. Tunawezaje kuhakikisha kwamba sala yetu ya kupata hekima itajibiwa? Luka 18:1; Yakobo1:6,7.**

---

---

---

"Hili hitaji la hekima isiwe ombi lisilo na maana, likapotea akilini mara tu limalizikapo. Ni ombi ambalo huonesha hitaji madhubuti la ndani ya moyo, linaloibuka kutoka utambuzi wa kupungukiwa hekima kupambanua mapenzi ya mungu.

"Baada ya kufanywa ombi, kama jibu halijapatikana haraka, usichoke kusubiri na kutokuwa imara. Usitie shaka, shikilia ahadi, "Mwaminifu ni Yule akuitaye wewe, Yeye ambaye pia atafanya hivyo." Kama mjane asiyekata tamaa, himiza hitaji lako, kuwa kidete katika lengo lako. Je, ni kitu muhimu na cha matokeo makubwa kwako? Hakika ndivyo. Basi usitie shaka, kwa Imani yako kuweza kujaribiwa. Kama jambo unalohitji ni la thamani, inastahili ukakamavu na bidii ya kazi. Unayo ahadi, kesha na omba. Kuwa imara na ombi litajibiwa; Je si Mungu aliyeahidi? Kama Ikikugharimu kitu kukipataa utakithamini zaidi ukipatapo. Umeambiwa wazi kwamba ukitia shaka uhitaji kufikiri kwamba utapata kitu chochote toka kwa Bwana. Angalizo limetolewa hapa ili usijechoka, bali kubaki imara juu ya ahadi. Kama ukiomba, atakupatia kwa ukarimu na hakemei.

"Hapa ndipo wengi hufanya kosa. Wanashaka katika lengo lao, na Imani yao hushindwa. Hii ndiyo sababu hawapokei kitutoka kwa BWANA, ambaye ni Chanzo cha nguvu zetu. Hakuna anayehitaji kwenda gizani, akijikwaa kama kipofu; maana BWANA ametoa nuru kama wataikubali katika namna aitoavyo, nasiyo kuchagua njia zao wenyewe. Anataka bidii katika kufanya wajibu wa kila siku. "—*Testimonies for the Church*, vol. 2, pp. 130, 131.

**b. Kwa nini tuepuke kuwa na nia mbili? Yakobo 1:8; Zaburi 86:11.**

---

---

"Huku wakidai kuwa Wakristo, wengi wana umbo la ulimwengu juu yao, na mapenzi yao hayakuwekwa kwa Mungu. Wao ni wenye nia mbili, wakijaribu kumtumikia Mungu na mali kwa wakati mmoja….kwa kujaribu kuwatumikia mabwana wawili, hawana msimamo katika njia zao zote, na hawawezi kutegemewa….

"Kuna faida gani kusema mambo ya kupendeza, kudharau kazi ya shetani, na wakati huo huo kuingia katika utimilifu wa hila zake zote? Huku ni kuwa na nia mbili. "—*The SDA Bible Commentary [E. G. White Comments]*, vol. 7, p. 938.

## *Alhamisi* — Oktoba 10

### 5. KUMKUMBUKA YAKOBO

**a. Yesu anatoaje kielelezo jinsi tunavyopaswa kutoa maombi yetu kwa bidii ili tupate nguvu za kutimiza mapenzi ya Mungu? Mathayo 11:12.**

---

" 'Ufalme wa mbinguni hupatikana kwa nguvu, nao wenye nguvu wauteka.' nguvu hii huchukua moyo wote. Kuwa na nia mbili ni kutokuwa na msimamo. Azimio, kujinyima na jitihada za kujitolea zinahitajika kwa ajili ya kazi ya maandalizi. Ufahamu na dhamiri viwe na umoja; lakini kama nia haijawekwa kufanya kazi, tutashindwa. Kila uwezo wa akili na hisia lazima zihusishwe. Ibada na maombi ya dhati lazima yachukue nafasi ya udhaifu. Ni kwa bidii tu, juhudi iliyodhamiriwa na imani katika wema wa kristo tunaweza kushinda, na kupata ufalme wa mbinguni. Muda wetu wa kufanya kazi ni mfupi. Kristo atakuja mara ya pili. "—*The SDA Bible Commentary [E. G. White Comments]*, vol. 1, p. 1096.

"Kwa ukweli mkuu ambao tumebahatika kuupokea, tunapaswa, chini ya nguvu za Roho Mtakatifu tungeweza kuwa njia hai za mwanga. Basi tungeweza kukikaribia kiti cha rehema; na kuona upinde wa ahadi, kupiga magoti kwa mioyo iliyopondeka, na kuutafuta ufalme wa mbinguni kwa nguvu ya kiroho ambayo ingeleta thawabu yake yenyewe. Tungeichukua kwa nguvu, kama alivyofanya Yakobo. Ndipo ujumbe wetu ungekuwa uweza wa Mungu uletao wokovu. Dua zetu zingejaa bidii, zilizojaa hisia ya hitaji letu kuu; na tusingekataliwa. Ukweli ungeonyeshwa kwa maisha na tabia, na kwa midomo iliyoguswa na makaa ya moto kutoka kwa madhabahu ya mungu.

"Wakati uzoefu huu ni wetu, tutainuliwa kutoka katika nafsi zetu maskini, za bei nafuu ambazo tumezipenda kwa upole. Tutatua mioyoni mwetu uwezo unaoharibika wa ubinafsi, na tutajawa na sifa na shukrani kwa Mungu. Tutamtukuza Bwana, Mungu wa neema yote, ambaye amemtukuza Kristo. Naye atadhihirisha uweza wake kupitia kwetu, akitufanya kuwa kama mundu wenye makali katika shamba la mavuno. Mungu anawaita watu wake wamdhihirishe. "— *Reflecting Christ*, p. 217.

## *Ijumaa* — Oktoba 11

### MASWALI TAFAKARI BINAFSI

**1. Elezea baadhi ya funguo muhimu za kupata hekima kuu kutoka Mbinguni.**

**2. Inakuwaje tunaporidhika na kutegemea maarifa ya kibinadamu?**

**3. Nifanyeje sehemu yangu kuwaweka huru watumishi ili kuzingatia roho mpya?**

**4. Ni katika sehemu gani za maisha ninaweza kuwa na nia mbili zaidi kuliko ninavyotambua?**

**5. Elezea nguvu na umuhimu wa mapambano ya Yakobo kwa siku za mwisho.**

**Somo la 3** **Sabato, Oktoba 19, 2024**

# Kukabiliana na Jaribu

**FUNGU LA KUKARIRI: "Heri mtu astahimiliye majaribu; kwa sababu akiisha kukubaliwa ataipokea taji ya uzima, Bwana aliyowaahidia wampendao. " (Yakobo 1:12).**

"Kunena na kutenda kuendane na maombi yenu. Itafanya tofauti kubwa kwako ikiwa jaribu litathibitisha imani yako kuwa ya kweli, au kuonyesha kwamba maombi yako ya kujionyesha tu."—*Christ's Object Lessons*, p. 146.

**Inapendekezwa kusoma:** *Testimonies for the Church,* vol. 3, pp. 477–492.

## *Jumapili* *Oktoba 13*

### 1. SABABU YA KUKUA KIROHO

**a. Elezea siri jinsi Yakobo 1:2 inavyoweza kutimizwa ndani yetu. Nehemia 8:10.**

---

---

"Majaribio yote yanayopokelewa kama walimu/waelimishaji yataleta furaha. Maisha yote ya kidini yatakuwa yenye kuhuisha, kuinua, kuboresha, kunukia kwa maneno na matendo mema. Adui anafurahi sana kuwa na roho zilizohuzunika, zilizoshuka, zenye kuomboleza na kuugua; anataka maoni kama hayo yatolewe kuhusu matokeo ya imani yetu. Lakini Mungu anapanga kwamba akili isichukue kiwango cha chini. Anatamani kila nafsi ipate ushindi katika uwezo wa utunzaji/kutunza wa Mkombozi. "—*Testimonies for the Church*, vol. 6, pp. 365, 366.

**b. Kwa nini mungu anaruhusu majaribu yaje juu yetu? Yakobo 1:3; Warumi 5:3.**

---

---

"Kama tunayashinda majaribu yetu na kupata ushindi juu ya vishawishi vya shetani, ndipo tunavumilia jaribio la Imani yetu, ambayoni ya thamani kuliko dhahabu, na kuandaliwa vizuri na kuwa na nguvu kukabilina na jaribu lingine. Lakini kama tukikata tamaa na kuyapa nafasi majaribu ya shetani, tutazidi kuwa wadhaifu na hatutapata thawabu ya kujaribiwa pia hahtutakuwa tayari kukabiliana na majaribu yanayofuata. Kwa njia hii tutazidi kuwa wadhaifu zidi na Zaidi, hadi tutakuwa mateka wa vishawishi vya shetani. Tunapaswa kuvaa silaha zote za Mungu na kuwa tayari kila wakati kupambana na nguvu za giza."— *Early Writings*, p. 46.

## 2. MATOKEO BORA KULIKO TUNAVYOWAZA

**a. Elezea faida za kuwa na subira. Yakobo 1:4; Luka 21:19.**

"Mungu ni mwenye hekima na mwema hata kujibu maombi yetu siku zote kwa wakati na kwa jinsi tunavyotamani. Atafanya zaidi na bora zaidi kwa ajili yetu kuliko kutimiza matakwa yetu yote. Na kwa sababu tunaweza kumwamini yeye hekima na upendo, hatupaswi kumwomba akubali mapenzi yetu, lakini tunapaswa kutafuta kuingia na kutimiza kusudi lake. Matamanio yetu na maslahi yanapaswa kupotea katika mapenzi yake. Mambo haya yanayojaribu imani ni kwa manufaa yetu. Inadhirishwa ikiwa imani yetu ni ya kweli na ya dhati, kuegemea juu ya neno la mungu pekee, au iwe kutegemeana na hali, halina uhakika na linaweza kubadilika. Imani inaimarishwa na matendo. Ni lazima tuache subira ifanye kazi yake kamilifu, tukikumbuka kwamba kuna ahadi za thamani katika Maandiko kwa wale wanamngojea Bwana. " —*The Ministry of Healing*, p. 231.

**b. Jinsi gani na kwa nini Yakobo anatuonyesha picha kubwa kuliko mtazamo wa muda tu wa mamlaka na ustawi katika ulimwengu huu uliopotoka? Yakobo 1:9–11.**

"Kwa wakati huu, kabla ya zahama ya mwisho, kabla ya uharibifu wa kwanza wa ulimwengu, watu wameingizwa katika anasa na harakati za akili. Kwa kushughulishwa na yanayoonekana na ya mpito, wamepoteza dira milele. Maana vitu vinaharibika kwa kutumiwa, wanatoa dhabibu ya utajiri usioharibika. Akili zao zinahitaji kuinuliwa, maono yao ya maisha yapanuliwe. Wanahitaji kuamshwa kutoka kwa uchovu na ndoto za kilimwengu.

"Kutoka kwa kuinuka na kuanguka kwa mataifa kama yalivyowekwa wazi katika kurasa za maandiko matakatifu, wanahitaji kujifunza jinsi utukufu wa nje na wa kidunia ulivyo bure. Babeli, pamoja na nguvu zake zote na fahari yake, ambayo dunia yetu haijawahi kuiona tangu wakati huo nguvu na fahari ambayo watu wa siku hizo walionekana kuwa imara na kustahimili jinsi ambavyo imepita kabisa! Kama 'ua la nyasi' limeharibika hivyo huangamia yote ambayo hayana Mungu kwa msingi wake. Ni kile tu ambacho kimefungamana na kusudi lake na kudhihirisha tabia yake ndicho kinaweza kustahimili. Kanuni zake ndizo pekee ambazo zitakazoweza kudumu ulimwengu wetu unajua. " — *Education*, p. 183.

"Hazina ya dunia inapita. Ni kupitia Kristo pekee ndipo tunaweza kupata utajiri wa milele. " —*The Review and Herald*, December 10, 1901.

## 3. KATIKA JOTO LA VITA

**a. Tunapokabili majaribu, ni lazima tufanye nini kwa sala, na kwa nini? Yakobo 1:12.**

"Ishini maisha ya kawaida, halisi. Iweni wakweli katika kila fikra na neno na tendo, na "kwa unyenyekevu wa akili kila mmoja amwone mwenzake bora kuliko yeye mwenyewe." Kumbukeni kuwa tabia ya maadili inahitaji kuboreshwa kwa kukesha na kuomba kila wakati. Mnapoendelea kumtazama Kristo, daima mko salama; lakini wakati mnapofikiria dhabihu zenu au kujitoleana shida zenu, na kuanza kujihurumia, mnapoteza tumaini lenu kwa Mungu na mnakuwa katika hatari kubwa. "—*Testimonies for the Church*, vol. 4, p. 522.

"Tunapaswa kusonga mbele kwa kasi, bila kukata tamaa wala tumaini katika kazi njema, jaribu lolote litakalotukabili, wala giza lolote la maadili linaloweza kutuzunguka. Uvumilivu, imani, na upendo kwa wajibu ndio masomo ambayo lazima tujifunze. Kuishinda nafsi na kumtazama Yesu ni kazi ya kila siku. Bwana hataiacha kamwe nafsi inayomtegemea na kuutafuta msaada Wake. Taji ya uzima imewekwa juu ya paji la uso wa mshindi pekee. "—*Ibid.*, vol. 5, pp. 70, 71.

**b. Kwa nini makosa kusema kwamba Mungu hutuma majaribu? Yakobo 1:13.**

"Tusijaribu kupunguza hatia yetu kwa kutoa udhuru juu ya dhambi. Hatuna budi kukubali jinsi Mungu anavyoikadiria dhambi, na hilo ni jambo zito kweli. Ni Kalvari tu iwezayo kufunua ubaya mkubwa wa kutisha wa dhambi.

"Majaribu ni ushawishi wa kufanya dhambi, na huo hautoki kwa Mungu, bali unatoka kwa Shetani, na kwenye uovu uliomo mioyoni mwetu wenyewe. "Mungu hawezi kujaribiwa na maovu, wala yeye mwenyewe hamjaribu mtu' Yakobo 1:13, R.V.

"Shetani anataka kututia majaribuni, ili uovu wa tabia zetu udhihirishwe mbele ya wanadamu na mbele ya malaika, apate kudai kuwa sisi ni watu wake. Yule adui hutuongoza tufanye dhambi, ndipo hutushtaki mbele ya wale wa mbinguni kuwa hatustahili upendo wa Mungu. "—*Thoughts From the Mount of Blessing*, pp. 116, 117.

**c. Wakati mshitaki anaposhambulia tabia zetu zenye dosari, Bwana hututeteaje? Zakaria3:1–4; 1 Yohana 1:9–2:1.**

## 4. NGUVU ZA MUNGU KATIKA UDHAIFU WETU

**a. Elezea maneno katika maombi ya Bwana, "usitutie majaribuni." " Mathayo 6:13 (sehemu ya kwanza); Isaya 30:21.**

"[Mungu] Anatuacha tupate migogoro, mateso na shida, si kama laana, bali kama mbaraka mkuu kuliko yote katika maisha yetu. Kila jaribu tunalolishinda, kila taabu tunayoivumilia, hutuletea uzoefu mpya maishani mwetu, na kutusogeza mbele katika kazi ya ujenzi wa tabia zetu. Mtu yule ambaye hushinda majaribu kwa nguvu itokayo juu, huwadhihirishia walimwengu na wote mbinguni jinsi neema ya Kristo ilivyo na nguvu.

"Lakini wakati hatupaswi kuwa na hofu kwa ajili ya taabu, japo iwe kali, tungeomba kwamba Mungu asituache twende mahali ambapo tutavutwa mbali na tamaa za mioyo yetu miovu. Katika kusali sala hiyo aliyotupa Kristo, tunajitoa wenyewe kuongozwa na Mungu, tunamwomba atuongoze katika njia zilizo salama. Hatuwezi kusali sala hii kwa moyo mnyofu, na huku tukaazimu kwenda katika njia zetu tulizozichagua wenyewe. Tutausubiri mkono wake utuongoze….

"Si salama kwetu kusitasita na kutafakari juu ya faida itakayopatikana tukiyatii mashauri ya Shetani. Dhambi humaanisha aibu na maangamizi kwa kila mtu ajifurahishaye katika hiyo; lakini kwa tabia yake inapofusha macho na kudanganya, tena inatushawishi kwa kutuletea mambo yanayovutia sana. Tukithubutu kwenda upande wa Shetani, hatuna ahadi yo yote ya kulindwa dhidi ya uwezo wake. Kwa kadiri ya uwezo ulio ndani yetu, imetupasa kufunga kila njia ambayo kwayo huyo mjaribu anaweza kupata njia ya kuingia ndani yetu.

"Sala hii, "Usitutie majaribuni," ni ahadi kwa yenyewe. "—*Thoughts From the Mount of Blessing*, pp. 117, 118.

**b. Je ni ombi na uhakikisho gani ambao Mungu anatupatia kuhusu majaribu? Yakobo 1:14–16; 1 Wakorintho10:13.**

"Jaribu ni nini? Ni njia ambayo wale wanaodai kuwa watoto wa mungu wanapimwa na kujaribiwa. Tunasoma kwamba Mungu alimjaribu Abraham, kwamba aliwajaribu wana wa Israeli. hii ina maana kwamba aliruhusu hali zitokee ili kujaribu imani yao na kuwaongoza kumtegemea yeye ili kupata msaada. Mungu anaruhusu majaribu yawajie watu wake leo ili watambue kuwa yeye ndiye msaidizi wao. Ikiwa wanamkaribia yeye wakati wa kujaribiwa, yeye huwatia nguvu ili kukabiliana na majaribu. "—*In Heavenly Places*, p. 251.

## *Alhamisi* **Oktoba 17**

### 5. MAJARIBU KATIKA MTAZAMO

**a. Kukaa ndani ya Kristo na kwa hivyo kukombolewa kutoka majari-buni, ni nini tunapaswa kuchagua kila wakati? Luka 4:8; Wafilipi 1:21.**

---

---

"Kamwe majaribu hawezi kutulazimisha kufanya maovu. Hawezi kuongoza mawazo isipokuwa kama mawazo yamekubali kuongozwa naye. Lazima kuwepo na uhiari kwanza, lazima imani iwe imeacha kum-shikilia Kristo kwanza, ndipo Shetani anaweza kututawala. Lakini kila nia ya dhambi tunayokuwa nayo inampatia Shetani mahali pa kusimama ma-hali petu. Kila eneo ambalo linatushinda kufikia viwango vya kimbingu ndilo mlango wake ulio wazi wa kuingilia ili kutujaribu na kutuharibu. Na kila kuanguka au kushindwa kwetu kunampatia nafasi ya kumsuta Kristo. "—*The Desire of Ages*, p. 125.

**b. Ni nini kinapaswa kutuchochea kusonga mbele hadi kushinda ka-tika Kristo? Wafilipi 4:13; Ufunuo2:10 (sehemu ya mwisho); 3:21.**

---

---

"Anayejazwa Roho wa Kristo hukaa ndani ya Kristo. Pigo linaloe-lekezwa kwake linaanguka juu ya Mwokozi, ambaye anamzunguka pande zote, akiwa pamoja naye. Lo lote limpatalo yeye linatoka kwa Kristo. Yeye hana haja ya kuupinga uovu, kwa maana Kristo ndiye mlinzi wake. Haku-na cho chote kiwezacho kumgusa isipokuwa kwa kibali chake Bwana, na "mambo yote" anayoruhusu "hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema." Warumi 8:28."—*Thoughts From the Mount of Bles-sing*, p. 71.

"Taji ya uzima imewekwa juu ya paji la uso wa mshindi pekee. Kuna jukumu zito kwa kila mtu la kumfanyia Mungu kazi kwa bidii wakati tukingali tunaishi. "— *Testimonies for the Church*, vol. 5, p. 71.

## *Ijumaa* **Oktoba 18**

### MASWALI TAFAKARI BINAFSI

1. **Ninahitaji kumbuka nini wakati jaribu gumu litakaponijia?**
2. **Ni lazima nitambue nini kuhusu jinsi Mungu hujibu maombi?**
3. **Majaribu hutoka wapi, na kwa nini?**
4. **Nini hutokea wakati wowote tunapopinga majaribu?**
5. **Ninawezaje kukaa kimamilifu zaidi ndani ya kristo?**

**Somo la 4** **Sabato, Oktoba 26, 2024**

# Kuweka Imani katika Matendo

**FUNGU LA KUKARIRI: "Lakini iweni watendaji wa neno, wala si wasikiaji tu, hali mkijidanganya nafsi zenu. (Yakobo 1:22).**

"[Mwanadamu] amechaguliwa kuwa mtii kwa kila ne no litokalo katika kinywa cha Mungu, na kwamba awe, si msikiaji tu , bali mtendaji wa neno. " —*Testimonies to Ministers*, p. 454.

**Inapendekezwa kusoma:** *Testimonies for the Church,* vol. 2, pp. 24–26, 50–55, 164, 165.

## *Jumapili* *Oktoba 20*

### 1. MTOAJI MKAMILIFU

**a. Ni nini kinachodhihirisha wema mkuu wa Mungu kwetu? Yakobo 1:17.**

"Upendo wa Kristo kwa watoto wake ni wa dhati na ulio na nguvu. Na hivyo una nguvu kuliko kifo; kwa maana alikufa ili kuununua wokovu wetu, na kutufanya wamoja naye, kwa fumbo la milele. Upendo wake una nguvu sana kwamba unatawala nguvu zake zote, na hutumia rasilimali nyingi za mbinguni katika kuwatendea watu wake mema. Haina kubadilika-badilika au kivuli cha kugeuka ndiye yule jana, leo, na hata milele. Ingawa dhambi imekuwepo kwa muda mrefu, ikijaribu kupinga upendo huu na kuzuia utiririko wake wa ardhi, bado inatiririka kwa wingi kwa wale ambao Kristo aliwafia.

"Mungu anawapenda malaika wasio na dhambi, wanaofanya huduma yake na ni watiifu kwa amri zake zote; lakini hawapi neema; hawajawahi kuhitaji, kwa maana hawajawahi kufanya dhambi. Neema ni sifa iliyoonyeshwa kwa wanadamu wasiostahili. Hatukuitafuta; ilitumwa kutafuta. Mungu anafurahi kuwapa neema wale wote wenye njaa na kiu kwa ajili yake, si kwa sababu sisi tunastahili, bali kwa sababu hatustahili. Hitaji letu ni ustahili unaotupa uhakikisho wa kwamba tutapokea zawadi. —*Testimonies to Ministers*, p. 519.

**b. Jinsi gani na kwa nini tumezaliwa na mungu? Yakobo 1:18; 1 Peter 1:23; 2:9.**

## 2. KUPOZA JOTO

**a. Katika ulimwengu wa hasira, ni kwa jinsi gani na kwa nini tunapaswa kuwa tofauti? Yakobo 1:19.**

---

"Iweke sheria ya kutozungumza neno la kukemea kila mmoja, bali pongeza na kusifu kila unapoweza.

"Wengine hudhani kuwa ni fadhila/wema usiopaswa kuzuiliwa, nao wataongea wakiisifia tabia yao ya kusema waziwazi ya kuongea mambo yasiyokubalika yaliyo moyoni. Wanaacha roho ya hasira ijichoshe katika mkondo wa shutuma na kutafuta-laumu. Kadri wanavyozungumza, ndivyo wanavyozidi kusisimka, na Shetani husimama karibu kusaidia kazi hiyo, kwa kuwa inamfaa. Maneno hayo yanamkasirisha yule anayeambiwa, nayo yaweza kujirudia, na kutoa uchochezi kwa maneno makali zaidi, mpaka jambo dogo limewasha moto mkubwa. Nyote wawili mnahisi kwamba mna majaribu yote ambayo mnaweza kustahimili na kwamba maisha yenu hayana furaha zaidi. Anzeni kwa dhati kazi ya kudhibiti mawazo yenu, maneno yenu, na matendo yenu. Wakati mmoja wenu anahisi kuongezeka kwa chuki, wekeni sheria ya kwenda peke yenu na kuomba kwa unyenyekevu kwa Mungu."—*Testimonies for the Church*, vol. 4, p. 243.

**b. Kwa nini hasira kali haimpendezi Mungu na inatibiwaje? Yakobo 1:20.**

---

---

"Wengine wana woga, na wakianza kushindwa kujizuia katika neno au roho chini ya uchochezi, wanalewa sana na ghadhabu. Kama vile mlevi anavyotumia vileo . hawatafakari, na si rahisi kushawishiwa au kusadikishwa. Hawana akili timamu; shetani kwa wakati huu ana udhibiti kamili. Kila moja ya maonyesho haya ya hasira hudhaifisha mfumo wa fahamu na nguvu za kimaadili, na inafanya kuwa vigumu kuzuia hasira katika uchochezi mwingine.

"Pamoja na darasa hili kuna dawa moja tu kujidhibiti vizuri chini ya hali zote. Jitihada za kuingia mahali pazuri, ambapo ubinafsi hautaudhika, unaweza kufanikiwa kwa muda; lakini shetani anajua mahali pa kupata roho hizi maskini, na atazishambulua katika udhaifu wao tena na tena. Watakuwa na wasiwasi daima mradi tu wanajifikiria sana….Lakini kuna tumaini kwao. Wacha maisha haya yawe na dhoruba sana migogoro na wasiwasi, kuletwa katika uhusiano na kristo, na kisha nafsi haidai kwa ajili ya ukuu….Wanapaswa kujinyenyekeza wakisema waziwazi, 'Nimefanya kosa. Je, utanisamehe? Kwa maana Mungu amesema tusiache jua litue juu ya ghadhabu yetu,'hii ndiyo njia pekee iliyo salama kuelekea kushinda."—*Sons and Daughters of God*, p. 142.

## 3. KUTUNZA NURU

**a. Elezea wito wa Mungu kwa kila mmoja wetu. Yakobo 1:21.**

"Ee, ni jinsi gani yeyote aliye na nuru ya ukweli, nuru kuu waliyopewa na Mungu, anaweza kukataa ghadhabu na hukumu za Mungu kwa kumtenda dhambi na kufanya mambo yale yale ambayo Mungu amewaambia katika Neno lake kutokufanya? Wanawezaje kupofushwa na shetani kiasi cha kumvunjia Mungu heshima mbele ya uso wake, na kuzitia unajisi nafsi zao kwa kufanya dhambi wakijua? Asema mtume, 'tumefanywa kuwa tamasha kwa ulimwengu, na kwa malaika, na kwa wanadamu.' Je! Hawa wenye dhambi nitawaita wanafiki? Katika Sayuni uliza, Ni kwa namna gani mimi ni tamasha kwa ulimwengu, na kwa malaika, na kwa wanadamu? Jijibuni wenyewe, Kwa matumizi mabaya yangu ya nuru na mapendeleo na rehema alizo nazo mungu alinipa, kwa matendo machafu ambayo yanaharibu na kuchafua roho. "—*Testimonies to Ministers*, p. 447.

**b. Neno la Mungu linahusiana vipi na wokovu wetu, hasa katika siku za mwisho? 2 Timotheo 3:15; 1 Wakorintho15:1, 2.**

"Kazi ya kweli ya Roho Mtakatifu juu ya mioyo ya wanadamu imeahidiwa, ili kutoa ufanisi kupitia Neno. Kristo ametangaza Neno kuwa roho na uzima….

"Shetani atafanya kazi kwa njia ya hila zaidi kutambulisha uvumbuzi wa wanadamu waliovikwa mavazi ya malaika lakini nuru itokayo katika Neno inaangaza katikati ya giza la maadili; na Biblia haitaondolewa kamwe na maonyesho ya kimuujiza. Ukweli lazima uchunguzwe, lazima utafutwe kama hazina iliyofichwa. Nuru za ajabu hazitatolewa kando na Neno, ama kuchukua mahali pake. Shikamana na Neno, lipokee Neno lilopandikizwa, ambalo litawahekimisha wanadamu hata kupata wokovu. "—*Selected Messages*, bk. 2, p. 100.

"Wale wanaoikumbatia Kweli wanapaswa kutafuta ufahamu wa Kweli wa maandiko na ufahamu halisia kimatendo wa Mwokozi aliye hai. Akili inapaswa kukuzwa, na kumbukumbu kushughulishwa. Uvivu wote wa kiakili ni dhambi, na uchovu wa kiroho ni kifo."—*Testimonies for the Church*, vol. 4, p. 399.

"Wakati maneno yake ya maagizo yamepokelewa, na kutumiliki, kwetu Yesu ni uwepo wa kudumu, anayetawala mawazo na matendo yetu. Tumejazwa na maagizo ya mwalimu mkuu aliyewahi kujua ulimwengu. "—*Messages to Young People*, p. 160.

## 4. KIOO CHA SHERIA YA MUNGU

**a. Kwa nini ni muhimu tuchunguze mioyo yetu? Yakobo 1:22–24.**

---

"Wengi hupokea sifa kwa wema ambao hawana. Mchunguzi wa mioyo hupima nia, na mara nyingi hufanya kazi ya kupongeza sana yanayoongozwa na wanadamu yameandikwa naye kama yanayotokana na ubinafsi na unafiki duni. Kila tendo la maisha yetu, liwe zuri na la kusifiwa, au la kustahili kulaaniwa, huhukumiwa na mchunguzi wa mioyo kulingana na nia iliyomsukuma.

"Wengi hupuuza kujiangalia kwenye kioo kinachodhihirisha kasoro za tabia; kwa hivyo udhaifu na dhambi zinadumu, na ni dhahiri kwa wengine, ikiwa hazieleweki na wale walio na makosa. Dhambi ya chuki ya ubinafsi ipo kwa kiwango kikubwa, hata kwa wengine wanaodai kujitoa kwa kazi ya mungu. Ikiwa wangelinganisha tabia zao na matakwa yake, hasa na kiwango kikuu cha sheria ya mungu takatifu, wangehakikisha, kama wachunguzi wa bidii, waaminifu, kwamba kwa uwoga wamepungukiwa. Lakini wengine hawako tayari kutazama mbali vya kutosha au ndani vya kutosha kuona upotovu wa mioyo yao wenyewe. Wanataka katika mambo mengi sana, lakini wanabaki katika kutojua hatia yao kwa hiari. "—*Gospel Workers*, pp. 275, 276.

**b. Elezea uzuri wa uhuru wa kweli kupitia nguvu ya uumbaji inayokuja kwa kujisalimisha kwa kristo na mapenzi yake. Yakobo1:25; Yohana 8:32.**

---

"Katika kazi ya ukombozi hakuna kulazimisha kwa nguvu. Hakuna nguvu ya nje inayotumika. Chini ya ushawishi wa Roho wa Mungu, mwanadamu huachwa huru kuchagua nani wa kumtumikia. Katika badiliko linalotokea wakati mtu anapojisalimisha kwa Kristo, kuna kiwango cha juu kabisa cha uhuru. Kuilazimisha dhambi ni tendo la moyo wenyewe. Kweli, hatuna nguvu ya kutuwezesha kutoka katika utawala wa Shetani; lakini tunapoamua kuwa huru mbali na dhambi, na katika uhitaji mkubwa tukalilia nguvu iliyo nje na juu yetu wenyewe, nguvu za moyo zinajazwa na nguvu ya mbinguni ya Roho Mtakatifu, na zinatii maongozi ya matakwa ya kutimiza mapenzi ya Mungu.

"Hali pekee ambayo uhuru wa mwanadamu unawezekana ni ile ya kuwa kitu kimoja na Kristo. "Kweli itawaweka huru" na Kristo ndiye kweli. Dhambi inaweza kushinda tu kwa njia ya kudhoofisha akili, na kuharibu uhuru wa moyo. Kutiishwa kwa Mungu ni njia ya mtu kurejeshwa, - kwenda katika utukufu na heshima ya kweli ya mtu. Sheria ya kimbingu, ambayo tumetiishwa kwayo, ni "sheria ya uhuru." Yakobo 2:12. "—*The Desire of Ages*, p. 466.

## *Alhamisi* **Oktoba 24**

### 5. DINI YA KWELI

**a. Taja kipengere muhimu cha Ukristo ambacho mara nyingi hakipo Yakobo 1:26.**

---

---

"Kupitia msaada ambao Kristo anaweza kutoa, tutaweza kujifunza kudhibiti ulimi, vile vile alipojaribiwa kwa maneno ya haraka na ya hasira, hakufanya dhambi hata siku moja kwa midomo yake. Kwa utulivu wa subira alikutana na dhihaka, na dhihaka za wafanyakazi wenzake kwenye benchi ya seremala. Badala ya kujibu kwa hasira , angeanza kuimba mojawapo ya zaburi nzuri za Daudi; na marafiki zake kabla ya kutambua walichokuwa wakifanya, wangeungana naye katika wimbo huo. Mageuzi gani yangefanywa katika ulimwengu huu ikiwa wanaume na wanawake leo wangefuata mfano wa kristo katika matumizi ya maneno. —*The SDA Bible Commentary [E. G. White Comments]*, vol. 7, p. 936.

**b. Ni kwa Jinsi gani dini ya kweli na safi isiyo na ubinafsi inatenda kazi bila kujua? Yakobo 1:27.**

---

---

"Kuwa mchapakazi, Kudumu kutenda kwa subira ambako huhitaji kujikana nafsi, ni kazi tukufu, ambayo mbingu huifurahia. Kazi ya uaminifu inakubaliwa na Mungu kuliko ibada yenye bidii zaidi na inayodhaniwa kuwa takatifu zaidi. Ni kufanya kazi pamoja na Kristo ndiyo ibada ya kweli. Maombi, maonyo, na maneno ya mdomoni ni matunda ya bei ndogo sana, ambayo mara nyingi huambatanishwa na kazi; lakini matunda ambayo hudhihirishwa kwa kutenda matendo mema, katika kuwajali wahitaji, yatima, na wajane, ni matunda yaliyo ya kweli/dhati, na kwa kawaida huota kwenye mti mzuri."—*Testimonies for the Church*, vol. 2, p. 24.

## *Ijumaa* **Oktoba 25**

### MASWALI TAFAKARI BINAFSI

1. **Kwa nini tunaweza kuamini maisha yetu katika Mungu wa milele wa Mbinguni?**
2. **Ni nini wajibu wa wote ambao wamejikuta wakishindwa kujizuia?**
3. **Kwa nini ni muhimu kwangu kujisomea Neno la Mungu?**
4. **Elezea uhuru wa kweli ni nini.**
5. **Ninawezaje kusitawisha kiwango kikubwa zaidi cha dini ya kweli kutoka moyoni?**

SABATO, NOVEMBA 2, 2024

## Sadaka za sabato ya kwanza kwa ajili ya GC Idara ya Fasihi




Kuna msemo maarufu, tone la wino linaweza kutengeneza fikara milioni." Nyenzo zilizochapishwa huelekea kubeba uzito zaidi kuliko tu maneno yanayosemwa kwa kiasi kikubwa kutokana kudumu kwake. Kwa maandishi, tunaweza kuchua muda wa kusoma kwa kasi yetu wenyewe, na pia kurejelea nyuma na kufikiria kwa undani zaidi habari tunayotafuta kujifunza. Inasaidia wakati wa kujaribu kuchukua mada za kina za kiroho.

Hili limekuwa kweli katika historia: "Kalamu ya Luther ilikuwa na nguvu, na maandishi yake, yaliyotawanyika, yalisisimua ulimwengu. Mashirika hayo hayo yapo chini ya amri yetu, na vifaa vimeongezeka mara mia. Biblia, machapisho katika lugha nyingi, yanayoeleza kweli kwa wakati huu, yako karibu nasi na yanaweza kubebwa upesi hadi ulimwenguni kote. "—*Testimonies for the Church*, vol. 6, p. 403.

"Na kwa kiwango kikubwa kupitia nyumba zetu za uchapishaji inapaswa kutimizwa kazi ya yule malaika mwingine anayeshuka kutoka mbinguni kwa nguvu kubwa na ambaye huangaza dunia kwa utukufu wake. "—*Ibid.*, vol. 7, p. 140.

Mnamo 1849, James White alitoa kichapisho kidogo kiitwacho Ukweli wa sasa. Mafungu madogo ya Makala yaliwekwa chini sakafuni. Ndipo ndugu na dada wakayazunguka na kumsihi Mungu kwa machozi kuzibariki nakala hizi zinapotumwa. Nakala hizo zilikusanywa zikafungwa na kutumwa, naye James White akazipeleka. Maili nane hadi kwenye ofisi ya posta ya Middletown."—*Early Writings*, (xxv).

Kitendo hiki kilikuwa ni kujibu ujumbe huu: "unapaswa kuanza vijizuu na kuwatumia watu. Mwanzoni viwe vichache; Lakini kadri watu wanavyosoma, watakutumia fedha za kuchapishia, na itafaulu tangu mwanzo.' "—*Ibid.*, (xxiv).

Nini hufanyika wakati gharama za usafirishaji zinapoongezeka na vizuizi vya mipakani vikihitaji njia za ghalama kubwa zaidi za usambazaji? Bei yetu ya usajiri haitoi gharama hizi mpya. Kwa hiyo, ni lazima tutegemee ukarimu wenye fadhili wa waumini wenzetu ili kutimiza unabii ulioambiwa kwa mhubiri huyo wa awali:

"Kama watu wanavyosoma, ndivyo watakavyokutumia. "

Tunaomba sadaka hii ya sabato ya kwanza kwa idara ya Fasihi ya GC itagusa moyo wako ili kutoa ziada kwa ajili ya roho duniani kote zinazohitaji kusoma ukweli wa sasa. Asante!

*Ndugu zenu katika Idara ya Fasihi GC*

**Somo la 5** **Sabato, Novemba 2, 2024**

# Kushinda Upendeleo

**FUNGU LA KUKARIRI: "Kwa maana hakuna upendeleo kwa Mungu." (Warumi 2:11).**

"Mungu hatambui tofauti ya cheo. Kwake hakuna tabaka. Machoni pake, wanadamu ni watu tu, wazuri au wabaya. Katika siku ya hesabu ya mwisho, cheo au mali havitabadilika kwa upana wa nywele kesi ya mtu yeyote. Kwa Mungu aonaye yote, watu watahukumiwa kwa jinsi walivyo katika usafi, katika heshima, katika upendo kwa kristo. " — *Counsels on Stewardship*, p. 162.

**Inapendekezwa kusoma:** *Testimonies for the Church,* vol. 3, pp. 304–309, 320–329.

## *Jumapili* *Oktoba 27*

### 1. TATIZO LA MTAZAMO

**a. Elezea mwelekeo wa kawaida wa kidunia ambao tunaweza kuwa na hatia, labda bila hata kutambua. Yakobo 2:1–4.**

---

---

"Maskini, kazi ya Mungu ingepuuzwa. Wala kazi hiyo haitateseka ikiwa wasimamizi wake watafanya wajibu wao, bali kazi ya Kristo inapaswa kuja kwanza. Maskini wanapaswa kushughulikiwa kwa maslahi na uangalifu kama ilivyo kwa matajiri. Tabia ya kuwaheshimu matajiri huku maskini wakidharaulika na kupuuzwa ni hatia mbele za Mungu. Wale ambao wamezungukwa na faraja zote za maisha, au wanaobembelezwa na kudekezwa na ulimwengu kwa sababu wao ni matajiri, hawahisi hitaji la huruma na fikra za upole kama vile watu ambao maisha yao yamekuwa yakipambana kwa muda mrefu na umaskini." — *Testimonies for the Church*, vol. 4, p. 551.

"Ingawa Kristo alikuwa tajiri katika nyua za mbinguni, lakini alifanyika maskini ili sisi kupitia umaskini Wake tupate kuwa matajiri. Yesu aliwaheshimu maskini kwa kushiriki hali yao ya unyenyekevu. Kutoka katika historia ya maisha Yake tunapaswa kujifunza jinsi ya kuwatendea maskini." —*Ibid.*, p. 550.

**b. Tunapaswa kutambua nini kuhusu wale ambao wanaweza kuwa maskini katika mali ya ulimwengu huu lakini matajiri katika imani? Yakobo 2:5.**

---

## 2. BUSARA NA HAKI

**a. Elezea mtazamo kamili ambao yesu alifundisha kuhusiana na kuwasaidia maskini. Marko 14:3–9.**

“Wengine hubeba wajibu wa faida kupita kiasi na kuwaumiza sana wahitaji kwa kuwafanyia mengi mno. Si mara zote maskini hujituma inavyopaswa. Ingawa hawatakiwi kupuuzwa na kuachwa wakiteseka, lazima wafundishwe kujisaidia wenyewe.

“Kazi ya Mungu haipaswi kupuuzwa ili kuwajali kwanza maskini. Kristo aliwapatia wanafunzi wake somo muhimu sana juu ya jambo hili. Mariamu alipomimina mafuta hayo juu ya kichwa cha Yesu, Yuda mwenye tamaa alisihi kwa dua kwa ajili ya maskini, akinung’unika kwa kile alichoona kuwa ni upotevu wa pesa. Lakini Yesu alithibitisha kitendo hicho, akisema: “Kwa nini mnamtaabisha? amenitendea kazi njema.” “Popote itakapohubiriwa Injili katika ulimwengu wote, hilo alilolitenda litatajwa kwa ukumbusho wake.” Kwa hili tunafundishwa kwamba Kristo anapaswa kuheshimiwa katika kuwekwa wakfu kwa kilicho bora zaidi cha mali yetu. Iwapo usikivu wetu wote ungeelekezwa katika kusaidia mahitaji ya maskini, kazi ya Mungu ingepuuzwa. Wala kazi hiyo haitateseka ikiwa wasimamizi wake watafanya wajibu wao, bali kazi ya Kristo inapaswa kuja kwanza.— *Testimonies for the Church*, vol. 4, pp. 550, 551.

**b. Katika Israeli ya kale, ni mtazamo gani uliohitajika kwa wale waliosimamia haki? Mambo ya walawi 19:15; Kumbukumbu la torati 1:17; 10:17.**

**c. Leo, ni jinsi gani wote katika nafasi yoyote ya uongozi wa kanisa wanapaswa kujifunza kutumia kanuni hii hii?1 Petro 1:17; Wakolosai 3:25.**

“Wale wanaounganisha mapenzi yao na kuvutiwa kwao kwa mtu mmoja au wawili, na kuwapendelea kuliko wale wengine, wasibakie na nafasi zao kwenye ofisi hata kwa siku moja. Upendeleo huu kwa wale maalum watakaomridhisha msimamizi katika mawazo yake ya kufikirika, kwa kuwapuuza wale wanaomhofu Mungu, ambao machoni pake ni wa thamani zaidi, siyo mtakatifu na ni kosa kwa Mungu. Kile ambacho Mungu anakithamini tunapaswa kukithamini. Mapambo ya mtu mnyenyekevu na Roho iliyotulia, Mungu huichulia katika uthamani wa juu kuliko uzuri wa nje au mapambo ya nje, utajiri, au heshima ya ulimwengu.”— *Ibid.*, vol. 3, p. 24.

## 3. KUTENGENEZA MAZOEA BORA

**a. Yakobo anatoa karipio gani kuhusu upendeleo wa kupenda mali wa wanaodai kuwa waumini na kwa nini hili ni jambo zito? Yakobo 2:6,7.**

---

---

---

"Mungu amekukiri mbele ya wanadamu na mbele ya malaika kuwa wewe ni mtoto wake; omba kwamba usiliaibishe "jina lile zuri mliloitwa" nalo. Yakobo 2:7. Mungu anawatuma duniani kama wajumbe wake. Katika kila tendo la maisha yenu hamna budi kulidhihirisha jina la Mungu. Dua hili linawataka ninyi mwe na tabia yake. Hamwezi kulitukuza jina lake, yaani, hamwezi kumwakilisha kwa walimwengu, isipokuwa kama kwa maisha na tabia yenu mnayawakilisha maisha halisi na tabia ya Mungu. Hilo mnaweza tu kufanya kwa kuipokea neema na haki ya Kristo. " —*Thoughts From the Mount of Blessing*, p. 107.

**b. Ni jinsi gani tunaweza kuwa washindi katika kumwakilisha kristo kwa njia ifaayo? Warumi 2:11; Mithali23:7.**

---

---

"Soma kwa umakini tabia ya Uungu ya mwanadamu, na mara kwa mara uulize, 'Yesu angefanya nini kama angekuwa mahali pangu? Hiki kinapaswa kuwa kipimo cha wajibu wetu. Msijiweke bila sababu katika jamii ya wale ambao ustadi wao wangeweza kudhoofisha kusudi lenu la kutenda haki, au kuleta doa juu ya dhamiri yenu. Usifanye chochote kati ya wageni, ndani mitaani, kwenye magari, nyumbani, ambayo yangekuwa na mwonekano mdogo wa uovu. Fanya kitu kila siku ili kuboresha, kupendezesha na kukuza uzima ambao kristo ameununua kwa damu yake mwenyewe.

"Daima tenda kutokana na kanuni, kamwe si kutokana na msukumo. Punguza msukumo wa asili yako kwa unyenyekevu na upole. Usijiendekeze katika vitu visivyo vya muhimu na . Tusiruhusu mizaha ata kidogo kutoka katika midomo yake. Hata mawazo yenu hayaruhusiwi kuendesha fujo. Lazima yazuiliwe, na kuletwa chini ya udhibiti wa utii wa kristo. Hebu ziwekwe juu ya mambo matakatifu. Kisha neema ya kristo, watakuwa safi na wa kweli.

"Tunahitaji hisia ya mara kwa mara kuimarisha nguvu ya mawazo safi. Usalama pekee kwa nafsi yoyote ni fikra sahihi….

"Jenga tabia ya kuwasema wengine vizuri. Zingatia sifa nzuri za wale unaoshirikiana nao, na uangalie kidogo iwezekanavyo makosa na mapungufu yao. " —*The Ministry of Healing*, pp. 491, 492.

## 4. KUWA NA TABIA YA KIFALME

**a. Maandiko yanasisitiza nini kuwa muhimu sana kwa imani yetu ya Kikristo na kwa nini? Yakobo 2:8.**

"Walimu wengi wa dini wanadai kwamba Kristo aliikoesha sheria kwa kifo chake, na ya kwamba tangu wakati huo watu wako huru na masharti yake. Wapo baadhi ambao wanaieleza kama kongwa zito, na kinyume na utumwa katika sheria wanahubiri uhuru katika injili.

"Lakini hivyo sivyo manabii na mitume walivyoichukulia sheria takatifu ya Mungu. Daudi alisema: "Nami nitakwenda panapo nafasi, kwa kuwa nimejifunza mausia yako." Zaburi 119:45. Mtume Yakobo, aliyeandika baada ya kifo cha Kristo, anaitaja sheria ya amri kumi kama "sheria ya kifalme" na "sheria kamilifu iliyo ya uhuru." Yakobo 2:8; 1:25. Na mwandishi wa kitabu cha Ufunuo, nusu karne baada ya kusulibiwa kwa Kristo, anataja baraka juu ya wale "wazishikao amri zake, wawe na haki kuuendea huo mti wa uzima, na kuingia mjini kwa milango yake." Ufunuo 22:14."—*The Great Controversy*, p. 466.

"Mtu anapojisalimisha kwa kristo, akili huletwa chini ya udhibiti wa sheria; bali ni sheria ya kifalme, inayotangaza uhuru kwa kila mfungwa. Kwa kuwa mmoja na kristo, mwanadamu anawekwa huru. Utiifu kwa mapenzi ya kristo maana yake ni kurejeshwa kwa utu uzima mkamilifu.

"Utii kwa Mungu ni uhuru kutoka katika utumwa wa dhambi nyingi, ukombozi kutoka kwa shauku na msukumo wa mwanadamu. Mwanadamu anaweza kusimama mwenyewe kama mshindi, mshindi wa mielekeo yake mwenyewe, mwenye kushinda falme na mamlaka, na 'juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho.' Waefeso 6:12"—*The Ministry of Healing*, p. 131.

**b. Je, kuwa na upendeleo /au chuki kunaharibuje ushuhuda wetu kwa ajili ya kristo? Yakobo 2:9.**

"Tunaweza kudai kuwa wafuasi wa Kristo, tunaweza kudai kuamini kila ukweli katika neno la Mungu; lakini hili halitamfaa jirani yetu isipokuwa imani yetu inabebwa katika maisha yetu ya kila siku. Taaluma yetu inaweza kuwa kama juu mbinguni, lakini haitatuokoa sisi wenyewe wala wanadamu wenzetu isipokuwa sisi ni Wakristo. Mfano mzuri utafanya mengi zaidi kunufaisha ulimwengu kuliko taaluma yetu yote. "—*Christ's Object Lessons*, p. 383.

## *Alhamisi* **Oktoba 31**

### 5. MAFUNDISHO YA BUSARA KWA HURUMA

**a. Tunapaswa kukumbuka nini katika kushika sheria yetu ya maadili ya Mungu wenyewe na vilevile wakati wa kushiriki ukweli huu na kizazi kijacho? Mhubiri 11:9; 12:13, 14; Yakobo 2:10–13.**

---

"Vijana wanazaliwa na upendo wa uhuru; wanatamani uhuru; na wanahitaji kuelewa kwamba baraka hizi zisizo na kifani zinapaswa kufurahia tu katika utii wa sheria ya Mungu. Sheria hii ndiyo mlinzi wa uhuru wa kweli. Inabainisha na kukataza yale mambo yanayodhalilisha na kuwafanya watumwa, na kwa hivyo inawapa ulinzi dhidi ya nguvu za uovu kwa watiifu.

"Mtunga - Zaburi asema: 'Nami nitakwenda panapo nafasi, kwa kuwa nimejifunza mausia yako.' 'Shuhuda zako nazo ndizo furaha yangu, na washauri wangu.' Zaburi 119:45, 24.

"Katika juhudi zetu za kusahihisha maovu, tunapaswa kujilinda dhidi ya tabia ya kutafuta makosa au kushtumu. Kuendelea kuwashtumu wadanganyifu, lakini hafanyi matengenezo. Kwa akili nyingi, na mara nyingi zile za uwezekano mkubwa zaidi, mazingira ya ukosoaji usio na huruma ni mbaya kwa juhudi. Maua hayafunguki chini ya pumzi ya upepo mkali….

"Lengo la kweli la kukemewa hupatikana pale tu mkosaji mwenyewe anapoongozwa kuona kosa lake na mapenzi yake yanaorodheshwa kwa ajili ya marekebisho yake. Hili likikamilika, mweleze kwenye chanzo cha msamaha na nguvu. Tafuta kuhifadhi heshima yake na kumtia moyo kwa ujasiri na matumaini.

"Kazi hii ndiyo nzuri zaidi, ngumu zaidi, iliyowahi kujitolea kwa wanadamu. Inahitaji mbinu nyeti zaidi, usikivu bora zaidi, ujuzi wa asili ya mwanadamu, na imani na subira iliyozaliwa mbinguni. Tayari kufanya kazi na kukesha na kungoja. Ni kazi ambayo hakuna kinachoweza kuwa muhimu zaidi."—*Education*, pp. 291, 292.

## *Ijumaa* **Novemba 1**

### MASWALI TAFAKARI BINAFSI

1. **Ilhali huenda nisiwe na mengi, ni lazima nitambue nini kuhusu wengine walio na hata kidogo?**
2. **Ni rahisi vipi kuwa na upendeleo wa kipofu au chuki isiyo ya haki dhidi ya baadhi ya watu?**
3. **Mwelekeo wetu wa kufikiri huathirije jinsi tunavyowatendea watu kama hao?**
4. **Kwa nini sheria ya Mungu inaitwa sheria ya uhuru?**
5. **Elezea mtazamo wa kuwa nao katika kufundisha watu wenye mawazo potofu.**

**Somo la 6** **Sabato, Novemba 9, 2024**

# Imani Katika Matendo

**FUNGU LA KUKARIRI: "Lakini wataka kujua, wewe mwanadamu usiye kitu, kwamba imani pasipo matendo haizai? " (Yakobo 2:20).**

"Ingawa matendo mema hayataokoa hata nafsi moja, lakini haiwezekani ata nafsi moja kuokolewa bila matendo."—*Faith and Works*, p. 111.

**Inapendekezwa kusoma:** *Early Writings,* pp. 226–228, 269–273.

## *Jumapili* *Novemba 3*

### 1. IMANI NA MFANO

**a. Kwa nini ni muhimu kabisa kuishi katika upatano kamili na imani tunayokiri? 1 Wakorintho 4:9; 1 Yohana 5:3; Yakobo 2:14.**

---

---

---

"Hebu wasiwepo watu wanaojidanganya kwa kuamini kwamba wanaweza kuwa watakatifu wakati wanavunja mojawapo ya matakwa ya Mungu kwa makusudi. Kuendekeza kutenda dhambi inayojulikana kunanyamazisha sauti ya Roho anayetushuhudia na kumtenga mtu mbali na Mungu."—*The Great Controversy*, p. 472.

"Ushuhuda wa maisha ya mtu unatangaza kwa ulimwengu kama yeye ni mkweli au la na kwa imani anayokiri. Mwenendo wako unapunguza viwango vya uzito sheria ya Mungu mbele ya marafiki zako wa kidunia. Unasema kwao: "Unaweza kutii au kutotii amri. Ninaamini kwamba sheria ya Mungu, kwa namna fulani, inawabana wanadamu; lakini, baada ya yote, Bwana si mwangalifu sana kuhusu utunzaji mkali wa sheria Yake. amri, na uasi wa hapa na pale hautembelewi na ukali kutoka Kwake.

"Wengi hujitetea kwa kuivunja Sabato kwa kurejelea mfano wako. Wanabishana kwamba ikiwa mtu mwema sana kama wewe, ambaye anaamini siku ya saba ni Sabato, anaweza kujishughulisha na kazi za kilimwengu katika siku hiyo wakati hali zinapoonekana kuhitajika, bila shaka wanaweza kufanya vivyo hivyo bila kulaaniwa. Nafsi nyingi zitakukabili katika hukumu, na kufanya ushawishi wako kuwa kisingizio cha kutotii kwao sheria ya Mungu. Ingawa hii haitakuwa msamaha kwa dhambi zao, lakini hii itazungumzia kwa utisho kuhusiana na wewe. "—*Testimonies for the Church*, vol. 4, p. 250.

## 2. MBINGU NA NCHI ZINATAZAMA

**a. Yakobo anatoa mfano gani ili kufafanua unafiki wa mazungumzo matupu bila matendo? Yakobo 2:15–17.**

"Hotuba fasaha zaidi inayoweza kuhubiriwa juu ya sheria ya Amri Kumi ni kuzitenda. Utii unapaswa kufanywa kuwa jukumu la kibinafsi. Uzembe wa jukumu hili ni dhambi kubwa. Mungu hutuweka chini ya majukumu sio tu kujihakikishia mbingu wenyewe, lakini kuhisi ni jukumu la lazima kuwaonesha wengine njia na, kupitia utunzaji wetu na upendo usio wa kimasilahi, kuwaongoza kwa Kristo wale wanaokuja katika uwanja wa ushawishi wetu. Kukosekana kwa kanuni ambayo inabainisha maisha ya wengi wanaodai kuwa Wakristo ni ya kutisha. Kutozingatia kwao sheria ya Mungu huwavunja moyo wale wanaotambua madai Yake matakatifu na huwageuza hao kutoka kwa Ukweli ambao wangeukubali vinginevyo."—*Testimonies for the Church*, vol. 4, p. 58. [Author's emphasis.]

**b. Imani ya kweli katika kristo inamaanisha nini? Yakobo 2:18; Mathayo 6:24.**

"Mungu ameshasema, na anamaanisha hivyo hivyo kwamba mwanadamu anapaswa atii. Haulizi kama ina urahisi kwake kufanya hivyo. Bwana wa uzima na utukufu hakuangalia urahisi au radhi Yake pale alipoacha cheo Chake cha daraja la juu na kuwa Mtu wa huzuni ajuaye sikitiko, akikubali fedheha na kifo ili kumkomboa mwanadamu kutokana na matokeo ya uasi wake. Yesu alikufa, si ili amwokoe mwanadamu katika dhambi zake, bali kutoka kwa dhambi zake. Mwanadamu anapaswa kuacha upotovu wa njia zake, kufuata mfano wa Kristo, kuchukua msalaba Wake na kumfuata, kujikana nafsi, na kumtii Mungu kwa gharama yoyote.

"Ikiwa sisi ni watumishi wa Kweli wa Mungu, kusiwe na maswali akilini mwetu iwapo tutii amri Zake au kutafuta mapenzi yetu ya kimwili. Iwapo waaminio Ukweli hawadumishwa/hawataimarishwa na imani yao katika siku hizi zenye amani, ni nini kitakachowategemeza wakati mtihani mkuu utakapokuja na amri itakapotolewa dhidi ya wale wote ambao hawataiabudu sanamu ya mnyama na kupokea chapa yake katika maisha yao; kwenye paji la uso au mikononi mwao? Kipindi hiki cha adhama hakiko mbali. Badala ya kuwa dhaifu na kutokuwa na msimamo, watu wa Mungu wanapaswa kukusanya nguvu na ujasiri kwa ajili ya wakati wa taabu."—*Ibid.*, pp. 250,251. [Author's emphasis.]

## 3. KUJIFUNZA KUTOKA KWA ABRAHAM

**a. Ni hali gani mbaya ya kiroho tunayoonywa kwa dhati? Yakobo 2:19.**

---

"Wengi wanakubali kwamba Yesu Kristo ni Mwokozi wa ulimwengu, lakini wakati huo huo wanajiweka mbali naye, na kushindwa kutubu. Dhambi zao, wanashindwa kumpokea Yesu kama Mwokozi wao binafsi. Imani yao ni kibali tu cha akili na hukumu kwa ukweli; lakini ukweli hauletwi moyoni, ili kutakasa roho na kubadilisha tabia. "—*Selected Messages*, bk. 1, pp. 389, 390.

"Unaweza kuamini Ukweli wote; ila kama bado kanuni zake hazijachukuliwa katika maisha yako, ukiri wako hautakuokoa. Shetani anaamini na kutetemeka. Anatenda kazi. Anajua muda wake ni mfupi, na ameshuka chini kwa nguvu kubwa kufanya kazi zake ovu sawasawa na imani yake. Lakini watu wamkirio MUNGU hawaungi mkono imani yao kwa matendo yao. Wanaamini katika ufupi wa wakati, huku bado wanashikilia tu kwa hamu vitu vya ulimwengu huu kana kwamba ulimwengu utakaa miaka elfu kama ulivyo sasa."—*Testimonies for the Church*, vol. 2, p. 161.

**b. Tunawezaje kuchochewa na mfano wa Abraham? Warumi 4:1– 3; Yakobo2:20–22.**

---

"Abraham alimwamini Mungu. Tunajuaje kwamba aliamini? Matendo yake yalishuhudia tabia ya imani yake, na imani yake ikahesibiwa kwake kuwa haki.

"Tunahitaji imani ya Abraham katika siku zetu, ili kuangaza giza linalotuzunguka, kufungia nje nuru tamu ya jua ya upendo wa Mungu, na ukuaji mdogo wa kiroho…. kila jukumu linalofanywa, kila dhabihu inayotolewa kwa jina la yesu, huleta thawabu kubwa sana. Katika tendo lenyewe la wajibu, Mungu husema na kutoa baraka zake. "—*The SDA Bible Commentary [E. G. White Comments]*, vol. 7, p. 936.

"Wanadamu wanahesabiwa haki kwa imani, lakini watu wanahukumiwana kupewa thawabu kulingana na matendo yao. "— *The Signs of the Times*, November 20, 1884.

"Haki ya Kristo inajumuisha matendo sahihi na matendo mema kutoka katika nia safi, isiyo na ubinafsi."—*Testimonies for the Church*, vol. 3, p. 528.

"Kuzishika amri za Mungu kunahitaji matendo mema kutoka kwetu, kujikana, kujitolea, na kujitoa kwa faida ya wengine, siyo kwamba kazi zetu nzuri pekee zinaweza kutuokoa, lakini hakika hatuwezi kuokolewa bila matendo mema. Baada ya kufanya yote ambayo tunaweza kufanya, basi tutasema: Hatujafanya zaidi ya wajibu wetu, sisi ni watumwa tusio na faida, tusiostahili upendeleo hata mdogo kutoka kwa Mungu. Kristo lazima awe haki yetu na taji ya furaha yetu. "—*Ibid.*, p. 526.

## 4. MANENO YA KUTIA MOYO

**a. Elezea jinsi kielelezo cha maisha ya Abraham kinapaswa kuonyeshwa katika maisha yetu kama waumini katika Kristo. Mwanzo 26:5; Yakobo 2:23, 24.**

---

---

"Matendo mema ni matunda ya imani. Mungu anapofanya kazi moyoni, na mwanadamu kuyakabidhi mapenzi yake kwa Mungu, na kushirikiana na Mungu, yeye anafanya katika maisha kile ambacho Mungu anafanya kazi ndani yake kwa njia ya Roho Mtakatifu, na kuna upatanisho kati ya kusudi la moyo na utendaji wa maisha. Kila dhambi lazima ikataliwe kama kitu cha chuki kilichomsulubisha Bwana wa uzima na utukufu, na muumini lazima awe na uzoefu wa maendeleo kwa kuendelea kufanya kazi za kristo. Ni kwa kuyasalimisha mapenzi daima, kwa utii wa kudumu, ndipo baraka ya kuhesabiwa haki inabaki.

"Wale wanaohesabiwa haki kwa imani lazima wawe na moyo wa kuishika njia ya Bwana. Ni ushahidi kwamba mtu hahesabiwi haki kwa imani wakati matendo yake hayalingani na mahubiri yake. Yakobo asema, 'Waona kwamba imani ilitenda kazi pamoja na matendo yake, na ya kwamba imani ile ilikamilishwa kwa njia ya matendo yale.?' (Yakobo 2:22).

"Imani isiyozaa matendo mema haihesabii haki ya nafsi. "—*Selected Messages*, bk. 1, p. 397.

**b. Kwa nini wote wanaoshuhudia makafiri leo wanaweza kutiwa moyo na jinsi Rahabu, kahaba anavyotajwa kuwa ambaye Mungu alimhesabia haki? Yakobo 2:25; Waebrania 11:31.**

---

---

"Katika Yeriko yenye maovu ushuhuda wa mwanamke wa kipagani ulikuwa 'Bwana, Mungu wenu, yeye ndiye Mungu katika mbinguni juu na katika nchi chini' Yoshua 2:11. ujuzi wa Yehova ambao ulikuwa umemjia hivyo, ulithibitisha wokovu wake….na kuongoka kwake halikuwa jambo pekee la rehema ya mungu kwa waabudu sanamu ambao walikubali mamlaka yake ya Kiungu. "—*Prophets and Kings*, p. 369.

"Wote ambao, kama Rahabu, Mkanaani, na Ruthu Mmoabu waligeuka kutoka kwenye ibada ya sanamu na kuelekea kumwabudu Mungu wa kweli, walipaswa kuungana na watu wake waliochaguliwa. "—*Christ's Object Lessons*, p. 290.

"Kazi kubwa inapaswa kufanywa katika miji yetu, na mashamba yote yameiva kwa mavuno. Usikivu wetu utaitwa kila upande, kwa kuwa nafsi zilizotubu katika nchi za Kikristo na za kipagani zitapaza sauti zao kwa msaada. Kusiwe na chembe moja ya kujiinua ; usalama wako pekee ni kumtumainia Mungu. "—*The General Conference Bulletin*, April 1, 1895.

## Alhamisi — Novemba 7

### 5. NJIA ZA USHINDI

**a. Elezea jinsi tunavyoweza kuwa na ushindi katika kristo. Yakobo 2:26; 2 Petro 1:3, 4.**

---

"Ni muhimu kuwa na imani katika Yesu, na kuamini umeokolewa kupitia yeye; lakini kuna hatari katika kuchukua msimamo ambao wengi huchukua katika kusema, 'Nimeokolewa.' Wengi wamesema: 'Lazima mfanye matendo mema; nawe utaishi'; lakini pasipo Kristo hakuna awezaye kufanya matendo mema. Wengi katika siku hizi husema, 'Amini, amini tu, na uishi.' Imani na matendo huenda pamoja, kuamini na kutenda vimeunganaa. Bwana anahitaji si chini ya nafsi sasa, kama vile alivyotaka Adamu katika Paradiso kabla ya kuanguka utii mkamilifu, uadilifu usio na dosari. Hitaji la Mungu chini ya agano la neema ni pana sawa na mahitaji alifanya katika Paradiso patana na sheria yake, ambayo ni takatifu, na ya haki na njema….Mtu awaye yote asikubaliane na udanganyifu huo unaompendeza moyo wa asili, ambao Mungu ataukubali unyoofu, haijalishi imani ni ipi, hata maisha yawe yasiyokamilika kiasi gani. Mungu anataka kutoka kwake utii kamili wa mtoto.

"Ili kukidhi matakwa ya sheria, imani yetu lazima ishike haki ya Kristo, tukiikubali kuwa haki yetu. Kupitia kuungana na Kristo, kwa kukubali haki yake kwa imani sisi tunaweza kustahili kufanya kazi za Mungu, kuwa watenda kazi pamoja na kristo. Ikiwa uko tayari kupeperuka pamoja na mkondo wa uovu, na usishirikiane na mashirika ya mbinguni katika kuzuia makosa katika familia yako, na katika kanisa, ili haki ya milele iweze kuletwa, huna imani. Imani hufanya kazi kwa upendo na kutakasa roho. Kwa njia ya imani Roho mtakatifu anafanya kazi ndani ya moyo ili kuumba utakatifu ndani yake; lakini hili haliwezi kufanyika isipokuwa wakala wa kibinadamu atafanya kazi pamoja na Kristo….Ili tuwe na haki ya Kristo, tunahitaji kila siku kubadilishwa kwa uvutano wa Roho, kuwa washiriki wa asili ya Kimungu."—*Selected Messages*, bk. 1, pp. 373, 374.

## Ijumaa — Novemba 8

### MASWALI TAFAKARI BINAFSI

1. **Katika kudai kushika sheria ya Mungu, ni lazima nitambue nini kuhusu ushawishi wangu?**
2. **Mbingu inahitaji nini kwa waumini wa kikristo?**
3. **Kwa nni Abraham mara nyingi anaitwa baba wa waaminifu?**
4. **Kati ya marafiki zangu, ni nani anayeweza kuishia kuwa Rahabu aliyeongoka?**
5. **Nitawezaje kuwa na uzoefu wa ushindi wa Kikristo?**

Somo la 7 **Sabato, Novemba 16, 2024**

# Kuomba kabla ya kufungua Vinywa vyetu

**FUNGU LA KUKARIRI: "Nifunzeni, nami nitanyamaa kimya; Mkanijulishe ni jambo gani nililokosa. " (Ayubu 6:24).**

"Mtu asiyejikwaa katika kunena, huyo ni mtu mkamilifu,awezaye kuuzuia na mwili wake wote kama kwa lijamu." Nuru inayoangazia njia yetu, ukweliambao unajitambulisha kwa dhamiri zetu, utailaani na kuiharibu roho, au kuitakasa nakuibadilisha. Tunaishi karibu sana na mwisho wa majaribu hivyo tusiridhike na kazi ya juu juu."—*Testimonies for the Church*, vol. 1, p. 308.

**Inapendekezwa kusoma:** *Testimonies for the Church,* vol. 2, pp. 50–55, 314–318; vol. 5, pp. 55–59, 175–177.

## *Jumapili* *Novemba 10*

### 1. KUTULIZA NAMNA YETU

**a. Ni nini chapasa kuwekwa akilini na wale ambao siku zote ni wepesi kujaribu kuwatawala wengine? Yakobo 3:1; Marko 9:35.**

"Mungu anamwajibisha kila mtu kwa ushawishi unaozunguka nafsi yake, kwa sababu yake mwenyewe na kwa ajili ya wengine. "—*Counsels to Parents, Teachers, and Students*, p. 102.

"Kwa kawaida, wanadamu wana ubinafsi na maoni yao. Lakini ubinafsi hutoweka katika maisha ya wale wanaojifunza masomo ambayo kristo anatamani kuwafundisha. Wanakuwa washirika wa asili ya Kimungu, na kristo anaishi ndani yao. Wanawachukulia watu wote kama ndugu, wenye matarajio sawa, uwezo, majaribu, wakitamani huruma na wanaohitaji msaada.

"Kamwe hatupaswi kumdhalilisha kiumbe mwenzetu. Tunapoona kwamba makosa yamefanywa tunapaswa kufanya yote tuwezayo kuwasaidia wale ambao wamekosea, kwa kuwaambia uzoefu wetu wenyewe tulifanya makosa makubwa sana, subira na ushirika, fadhili na usaidizi, kwa upande wa wafanyakazi wenzetu, vilitupa ujasiri na tumaini." —*The Signs of the Times*, May 11, 1904.

## 2. KUKUZA MTAZAMO BORA

**a. Ni karipio gani kali linalotolewa kwa wale walio wakali kwa wengine huku wakikataa kukiri makosa yao wenyewe? Mhubiri 7:20; Yakobo 3:2 (sehemu ya kwanza).**

---

---

"Je hamtatambua mapungufu yenu wenyewe na kuvaa silaha zote za haki? Je, hutakuwa macho na kukosoa sana roho na tabia zako na maneno yako kama vile ulivyo juu ya wengine, ili Mungu asije akavunjiwa heshima, na ukweli wake ukawakilishwa vibaya? Utambuzi wako ungeboreshwa sana ikiwa ungefanya hivi. Kweli, neno lililo hai, lingekuwa kama moto uliofungwa katika mifupa yako, ambao ungeangaza kwa uwazi, utofauti usio na shaka kumuakilisha kristo kwa ulimwengu….

"Je hakuna hata mmoja wa wale ambao wamejifanya wapelelezi kuona mwelekeo wa nafasi ambayo wamechukua katika kujaribu kuwadhibiti nguvu? Macho yao safi ya kiroho yalikuwa wapi? Kwa nini wangeweza kutambua kibanzi kwenye jicho la ndugu, na boriti kwenye jicho lao wenyewe? "—*Testimonies to Ministers*, pp. 295, 296.

**b. Ni nini kinachoonyesha kwamba mtu amefikia kiwango cha ukamilifu wa kimaadili na ni jinsi gani pekee hii inawezekana? Yakobo 3:2; 1 Wakorintho13:5 (nusu ya pili).**

---

---

"Ambapo ulimi usiodhibitiwa hupata nafasi ya kufanya kazi yake isiyo takatifu furaha ya Bwana haiwezi kudumu.

"Watu wenye kutia shaka, wanaowawazia na kuwasema vibaya ndugu zao, wakumbuke kwamba wanafanya mambo ya shetani. Hebu kila mshiriki wa kanisa afanye kazi kwa dhamira ya dhati, na kwa maombi kwa ajili ya usaidizi, kuponya mshiriki mgonjwa, kila mmoja ajisikie kuwa ni wajibu na upendeleo wake kupitisha tofauti ndogo na makosa bila maoni. Usikuze makosa madogo yaliyofanywa na mtu fulani, lakini fikiria wema ulio ndani yake. Kila wakati makosa haya yanafikiriwa na kuzungumzwa, yanakuwa makubwa. Mlima umetengenezwa kwa kilima cha mole. Hisia mbaya na ukosefu wa kujiamini ndiyo tokeo. "—*Australasian Union Conference Record*, April 15, 1903.

"Weka agano na Mungu kwamba Mtu yeyote asipokosea kwa neno, huyo ni mtu mkamilifu, na awezaye kuutawala mwili wote pia." Yakobo 3: 2. Kumbuka kwamba maneno ya kulipiza kisasi hayamfanyi mtu ahisi kwamba amepata ushindi. Hebu Kristo azungumze kupitia kwako. Usipoteze baraka inayotokana na kutokuwaza ubaya wowote"—*Testimonies for the Church*, vol. 7, p. 243.

## 3. INAANZIA KWENYE MZIZI

**a. Fuatilia mwelekeo usiofaa unaofuata pindi tunapokaa na kinyongo, na ueleze njia peke ya kuepuka hili. Waebrania 12:15; Yakobo 3:3–5.**

"Umehifadhi chuki yako dhidi ya mumeo na wengine ambao wamekukosea, lakini umeshindwa kugundua ni wapi umekosea na kuzidisha hali kwa njia yako mbaya. Roho yako imekuwa kali dhidi ya wale ambao wamekutenda udhalimu, na hisia zako zimepatikana kwa lawama na lawama. Hii inaweza kutoa afueni ya muda kwa moyo wako ulioelemewa, lakini imeacha kovu la kudumu juu ya nafsi yako. Ulimi ni kiungo kidogo, lakini umesitawisha matumizi yake yasiyofaa mpaka imekuwa moto uteketezao.

"Vitu hivi vyote vimependa kuangalia maendeleo yako ya kiroho. Lakini Mungu anaona jinsi ilivyo ngumu kwako kuwa mvumilivu na mwenye kusamehe, na anajua jinsi ya kuhurumia na kusaidia. Anahitaji wewe kurekebisha maisha yako, kurekebisha kasoro zako. Anatamani kwamba roho yako thabiti, isiyoyumba itawaliwe na neema Yake. Unapaswa kutafuta msaada wa Mungu, kwa sababu unahitaji amani na utulivu badala ya dhoruba na mabishano. Dini ya Kristo inakuamuru uache kidogo kutenda mambo kwa msukumo/mihemko, na zaidi kutoka kwa sababu iliyotakaswa na hukumu tulivu. "—*Testimonies for the Church*, vol. 4, p. 139.

**b. Kipi tunapaswa kukitambua kuhusu maneno tunayo tamka? Yakobo 3:6.**

"Maneno yako yatatangaza, matendo yako yataonesha, wapi ilipo hazina yako"—*Ibid.*, vol. 1, pp. 698, 699.

"Dada F anasukumwa na mhemko, na kutafuta makosa, na amekuwa na mengi ya kusema dhidi ya ndugu na dada zake. Hii itasababisha machafuko katika kanisa lolote. "—*Ibid.*, vol. 2, p. 51.

"Hebu wale wanaofurahi kufuatilia maneno ya uongo na uzushi dhidi ya watumishi wa Kristo wakumbuke kwamba Mungu ni shahidi wa matendo yao. Mguso wao wa kashfa hautii unajisi vyombo visivyo na roho bali tabia za wale ambao Kristo amewanunua kwa damu Yake. Mkono uliowafuata wahusika kwenye kuta za ikulu ya Belshaza unaweka rekodi ya uaminifu ya kila tendo la dhuluma au uonevu unaofanywa dhidi ya watu wa Mungu."—*Ibid.*, vol. 5, pp. 244, 245.

## 4. HATA IKITOKEA KUWA NI UKWELI. . .

**a. Ni maombi gani yenye nguvu yanayotolewa kuhusu mwelekeo hatari unaoenea katika siku zetu? Zaburi 15:1–3; 1 Wakorintho 13:6.**

"Ulimi unaofurahia ufisadi/hila, ulimi unaobwabwaja na kusema, Taarifu/ripoti, na mimi nitaitaarifu/nitaripoti, umeelezwa na mtume Yakobo kuwa umeandaliwa kwa moto wa jehanamu. Unatema cheche za moto kila upande. Anajali kwa kiasi gani mteja wa uvumi kwamba anawachafua wasio na hatia? Haiachi shuguli yake mbaya, ingawa anaharibu matumaini na ujasiri wa wale ambao tayari wamezama chini ya mizigo yao. Anajali tu kuiendekeza tabia yake ya kupenda kashfa. Hata wale wanaojiita Wakristo hufumba macho yao katika kila kilicho safi, cha uaminifu, kilicho bora, na cha kupendeza, na kufanyia kazi kile ambacho ni kibaya na cha kuchukiza, na kukichapisha/kukitangaza ulimwenguni.

"Ninyi wenyewe mmemfungulia milango Shetani aingie. Mmempatia nafasi ya heshima katika upelelezi wenu, au mikutano ya uchunguzi. Lakini hamjaonyesha heshima kwa tabia bora iliyoanzishwa kwa miaka mingi ya uaminifu. Lugha za wivu, za kulipiza kisasi zimefanya vitendo na misukumo kwa rangi zanazokidhi maoni yao wenyewe. Wameifanya nyeusi ionekane ni nyeupe, na nyeupe iwe nyeusi. Wakati ilipopingwa kwa matamshi yao, wengine wamesema: "Ni kweli." Je, kukubali kwamba yaliyosemwa ni ya kweli kunahalalisha njia yenu? Hapana, hapana. Ikiwa Mungu atachukua mashtaka yote ambayo kwa kweli yanaweza kuletwa dhidi yenu, na kuyafanya kuwa mjeledi wa kuwaadhibu, vidonda vyenu vitakuwa vikubwa, na vilivyochimbika zaidi na zaidi kuliko vile ambavyo mmempatia ndugu -----.angekuwa yale yote ambayo mnamwakilisha kuwa, ambayo najua hayuko hivyo, mwenendo wenu bado isingepata udhuru.

"Tunaposikiliza shutuma dhidi ya ndugu zetu, tunachukua shutuma hizo………. [Zaburi 15:1–3 Imenukuliwa.]"—*Testimonies for the Church*, vol. 5, pp. 57, 58.

**b. Katika dhambi saba zilizotajwa kuwa machukizo kwa Bwana, ni ngapi zinazohusika na maneno yetu? Mithali 6:16–19.**

## *Alhamisi* — Novemba 14

### 5. SILAHA INAYO JERUHI

**a. Jinsi gani na kwa nini ni lazima tuepuke mazoea ya kawaida sana ya kusengenya? Ayubu 6:24; Mithali 11:13; 26:20–22.**

---

"Ulimwengu wa uvumi/umbeya ungekuwa kama kila mtu angekumbuka kuwa wale wanaomwambia makosa ya wengine watayatangaza pia makosa yake kwa uhuru wakipata fursa nzuri. Tunapaswa kujitahidi kuwafikiria vizuri watu wote, hasa ndugu zetu, hadi tutakapolazimika kufikiria vingine. Hatupaswi kutoa taarifa mbaya kwa haraka. Mara nyingi hizi ni matokeo ya wivu au kutokuelewana, au zinaweza kuendelea kutokana na kutia chumvi mambo kuuelewa ukweli kwa juu juu tu. Punde wivu na tuhuma zinapopata nafasi, zitapandikiza matangazo yao yatakayopeperushwa kama upepo. Endapo ndugu ameiacha njia, basi huo ndio wakati wa kuionesha nia yako ya Kweli kwake. Nenda kwake kwa wema, omba naye na kwa ajili yake, ukiikumbuka gharama isiyo na kipimo ambayo Kristo ameilipa kwa ajili ya ukombozi wake. Kwa njia hii unaweza kuokoa roho kutoka mautini, na kuficha wingi wa dhambi.

"Kutazama, kutamka neno, au hata lafudhi ya sauti, vinaweza kujaa uongo, vikizama kama mshale ndani ya moyo, na kusababisha jeraha lisilopona. Kwa hiyo shaka, aibu, vinaweza kutupwa juu ya yule ambaye kupitia kwake Mungu angefanya kazi nzuri, na ushawishi wake unakuwa umeathirika, umuhimu wake umeharibiwa. Miongoni mwa baadhi ya makundi ya wanyama, ikiwa mmoja wao amejeruhiwa na kuanguka, mara moja huwekwa chini na kuraruliwa na wenzake. Roho hiyo hiyo ya kikatili inaendekezwa na wanaume na wanawake wanaolibeba jina la Wakristo. Wanaonyesha bidii ya kifarisayo kwa kuwapiga mawe wengine wasio na hatia kuliko wao. Kuna wengine ambao wanaelekeza makosa na kushindwa kwa wengine ili wageuze umakini kutoka dhambi zao, au wapate sifa ya juhudi kubwa kwa Mungu na kanisa."—*Testimonies for the Church,* vol. 5, pp. 58, 59.

"Wakati ambao mara nyingi ni mbaya zaidi kuliko kupotezwa katika uvumi usiofaa, ujinga, na uovu unapaswa kutolewa kwa vitu vya juu na vyenye heshima."—*Ibid.*,p. 176.

## *Ijumaa* — Novemba 15

### MASWALI TAFAKARI BINAFSI

1. **Kwa nini nipunguze tabia ya kuwa na maoni juu ya kila kitu.**
2. **Taja kipengele muhimu cha tabia kama ya Kristo ambayo mara nyingi hupuuzwa.**
3. **Tunapowadharau waumini wenzetu mbele ya wengine, Mungu huonaje jambo hilo?**
4. **Ninahitaji kujifunza nini kutokana na Zaburi ya 15 na kwa nini ni muhimu?**
5. **Ninawezaje kuwa na hatia ya kupanda mafarakano kati ya ndugu na kwa nini ni lazima kuacha?**

Somo la 8 **Sabato, Novemba 23, 2024**

# Kuchagua nini cha Kufikiri

**FUNGU LA KUKARIRI: "Enyi wazao wa nyoka, mwawezaje kunena mema, mkiwa wabaya? Maana, kinywa cha mtu huyanena yaujazayo moyo wake. " (Mathayo 12:34, nusuya pili).**

"Omba kabla ya kusema, na malaika wa mbinguni watakusaidia na watawafukuza malaika waovu, ambao wanaweza kukuongoza kutokumheshimu Mungu, kudharau kazi Yake, na kudhoofisha nafsi yako mwenyewe. " —*Testimonies for the Church*, vol. 2, p. 82.

**Inapendekezwa kusoma:** *Thoughts From the Mount of Blessing,* pp. 125– 129.

## *Jumapili* *Novemba 17*

### 1. DAWA YA SUMU

**a. Tunaposhambuliwa na mazoea ya usemi wa watu wenye nia mbaya, ni ujumbe gani wa Mungu kwetu, hata kati ya haya yote? Yakobo 3:7, 8; Waebrania 10:38.**

---

---

"[Ndugu J] Anahurumiwa na malaika wa mbinguni, kwa maana amezungukwa na giza. Masikio yake yanasikia maneno ya kutoamini na giza kwa mfululizo. Ana mashaka na maswali yanayotupwa kila mara mbele yake. Ulimi ni ulimwengu wa uovu. "Bali ulimi hakuna awezaye kuufuga; ni uovu usiotulia, umejaa sumu iletayo mauti." Kama Ndugu J angeshikamana na Mungu kwa uthabiti zaidi na kuhisi kwamba anapaswa kuhifadhi uaminifu na maadili yake mbele za Mungu hata kwa gharama ya uhai wake wa asili, angepokea nguvu kutoka juu. Kama anaruhusu imani yake kuathiriwa na giza na ukafiri unaomzunguka mashaka na maswali na mazungumzo mengi - hivi karibuni atakuwa kwenye giza totoro na mashaka na kutoamini, na hatakuwa na nuru wala nguvu katika Ukweli.

"Hapaswi kufikiria kwamba kwa kutafuta kuridhiana na marafiki zake, ambao wana uchungu dhidi ya imani yetu, atafanya iwe rahisi kwake. Ikiwa atasimama kwa kusudi moja la kumtii Mungu kwa gharama yoyote atapata msaada na nguvu. Mungu anampenda na kumhurumia Ndugu J. Anajua kila mashaka, kila hali ya kukatisha tamaa, kila usemi wa uchungu. Anayafahamu yote. Ikiwa ataweka kando kutokuamini kwake na kusimama katika Mungu bila kutikiswa, imani yake itaimarishwa kwa mazoezi." —*Testimonies for the Church*, vol. 4, pp. 236, 237.

## 2. JAMBO ZITO

**a. Yale yaliyoandikwa kuhusu usemi wa udanganyifu na uchochezi na kwa nini ni lazima tuombe ili kushinda katika nyanja hii ya maisha? Zaburi 5:8–10.**

---

---

"Hotuba ni mojawapo ya zawadi kuu za Mungu kwa mwanadamu. Ulimi ni kiungo kidogo, lakini maneno ambayo hutunga, yakitolewa kwa sauti yana nguvu kubwa. Bwana atangaza, 'hakuna mtu awezaye kuufunga ulimi.' umeweka taifa dhidi ya taifa, na umesababisha vita na umwagaji damu. Maneno yamewasha moto ambao umekuwa mgumu kuzima. Pia wameleta furaha na shangwe kwa nafsi nyingi. Na maneno yanaposemwa kwa sababu Mungu anasema, 'sema nao maneno yangu,' mara nyingi husababisha huzuni kwa toba.

"Kipaji cha hotuba kinabeba jukumu kubwa. Inahitaji kulinda kwa uangalifu; kwa maana ni nguvu kuu kwa uovu na kwa wema."—*The SDA Bible Commentary [E. G. White Comments]*, vol. 3, p. 1142.

"Lazima kuwe na matengenezo kamili katika maisha yako, mabadiliko kwa kufanywa upya nia yako. Mungu anahitaji watu Wake wakusaidie kwa sababu unahitaji msaada, na unapaswa kuwa mnyenyekevu sana ili kusaidiwa na wao. Unapojaribiwa kumwachia mshiriki mkorofi, ah! kumbuka kwamba malaika mwenye kuweka kumbukumbu anaandika kila neno. Yote yameandikwa kitabuni, na, usipooshwa kwa damu ya Kristo, lazima ukutane nayo tena. Sasa una kumbukumbu isiyo safi mbinguni. Toba ya dhati mbele za Mungu itakubaliwa. Unapokaribia kuzungumza kwa hasira na shauku, funga kinywa chako. Usiseme neno."—*Testimonies for the Church*, vol. 2, p. 82.

**b. Elezea jinsi maneno yetu yanavyotoka kwa wingi ya kile tunachokifikiri na kuhusu namna tulivyo. Yeremia17:9; Mathayo 12:33–37; 14:6–8.**

---

---

"Maudhui ya mazungumzo hufunua hazina ya moyo. Mazungumzo yasiyo ya thamani, ya kawaida, maneno ya kubembeleza, midhaa ya kipumbavu, yanayosemwa ili kuunda kicheko, ni biashara ya shetani, na wote wanaojiingiza katika mazungumzo haya ni biashara ya bidhaa zake. Mivuto inafanywa kwa wale wanaosikia mambo haya sawa na yale yaliyofanywa na Herode wakati binti wa Herode aliyecheza mbele yake. Shughuli hizi zote zimeandikwa katika vitabu vya mbinguni; na siku kuu ya mwisho watatokea katika nuru zao za kweli mbele ya wakosefu. Ndipo wote watakapotambua ndani yao matendo ya kuvutia na ya udanganyifu ya ibilisi, ili kuwaongoza kwenye njia pana lango pana linalofungua kwa uharibifu wao. "—*Testimonies to Ministers*, pp. 84, 85.

## 3. MOYO WOTE UNAHITAJIKA

**a. kwa nini tutegemee usemi thabiti kutoka kwa waumini katika ukweli uliopo? Yakobo 3:9, 10. Ni onyo gani linalotolewa ikiwa tunashindwa kuhusu jambo hili.**

---

"Ikiwa mtakuwa na mazoea ya kuthamini hisia kwamba Mungu huona na kusikia yote unayofanya na kusema, na kuweka kumbukumbu ya uaminifu ya maneno na matendo yenu yote, na kwamba lazima mkutane nayo yote, basi katika yote mnayofanya na kusema mtatafuta kufuata maagizo ya dhamiri iliyoelimika na kuamka. Ulimi wenu utatumiwa kwa utukufu wa Mungu na utakuwa chanzo cha baraka kwenu na kwa wengine. Lakini kama mkijitenga na Mungu kama mnavyofanya, jihadharini usije ulimi wenu ukadhihirisha ulimwengu wa uovu na kukuleteeni hukumu ya kutisha; kwa kuwa roho zitapotea kupitia ninyi/kwenu."—*Testimonies for the Church*, vol. 4, p. 244.

**b. Ni sala gani inaweza kutusaidia kufikiri na kuzungumza kwa uthabiti zaidi? Zaburi 86:11.**

---

"Ikiwa mpokeaji wa maarifa ya Biblia hafanyi mabadiliko yoyote katika mazoea au matendo yake kuendana na nuru ya kweli, nini basi? je! Roho anapigana vita na mwili, na mwili dhidi ya roho; na mmoja wa hawa lazima ashinde. Ikiwa kweli huitakasa nafsi, dhambi inachukiwa na kuepukwa, kwa sababu kristo anakubaliwa kuwa mgeni mwenye kuheshimiwa. Lakini kristo hawezi kushiriki moyo uliogawanyika; dhambi na yesu kamwe hawako katika ushirika. "—*Testimonies to Ministers,* p. 160.

"Kesha na uombe daima. Jitoe nafsi yako kikamilifu kwa Bwana na haitakuwa vigumu kumtumikia. Una moyo uliogawanyika. Hii ndio sababu giza badala ya nuru linakuzingira. Ujumbe wa mwisho wa rehema sasa unatolewa. Ni ishara ya uvumilivu na huruma ya Mungu. Njoo! Ndiyo mwaliko unaotolewa sasa. Njooni! kwa maana vitu vyote viko tayari sasa. Huu ni mwito wa mwisho wa rehema. Baadae kitakuja kisasi cha Mungu Mwenye ghadhabu. "—*Testimonies for the Church,* vol. 2, p. 225.

"Ni kwa moyo wote, ni wanaume na wanawake walioamua kwa moyo wote, ndio watakaosimama sasa. Kristo aliwapepeta wafuasi Wake tena na tena, hadi wakati fulani walibaki kumi na mmoja na wanawake wachache waaminifu walioweka msingi wa kanisa la Kikristo. Wapo wale ambao watasimama nyuma wakati mzigo unapaswa kubebwa; lakini wakati kanisa linapowaka na kung'aa, wanapata shauku, wanaimba na kupiga kelele, na kusisimka; lakini kuweni makini nao. Shauku inapokwisha, ni akina Kalebu wachache tu waaminifu watakaokuja mbele na kuonesha kanuni isiyotetereka. Hawa ni chumvi ambayo huhifadhi harufu. "—*Ibid.*, vol. 5, p. 130.

## 4. MAJI KUTOKA KWENYE CHEMCHEM SAFI

**a. Ni kanuni gani inayofunua kwamba moyo pekee uliofanywa upya kwa neema ya Mungu unaweza kuleta matendo thabiti? Yakobo 3:11, 12. toa mifano fulani inayofaa.**

---

---

"Unadhifu na utaratibu wa mavazi, na usafi katika makao yote, vinapaswa kuzingatiwa kwa uthabiti na watunza-sabato, ambao wanaonekana kuwa wa ajabu, na wanaangaliwa kwa ajili ya makosa yao. Ushawishi wao unapaswa kuwa mtakatifu. Kweli takatifu ambazo tunakiri kamwe hazitawashushia hadhi wapokezi, na kuwafanya wawe wakali na wakorofi, wasiojali nafsi zao, na wachafu katika nyumba zao. Ikiwa mpokezi ana tabia ya ulegevu, ukweli humwinua, na kumfanyia matengenezo kamili. Isipokuwa ukweli una athari hii, mtu binafsi hajahisi uwezo wake wa kuokoa. Kutojari na mavazi yasiyo na utaratibu sio alama ya unyenyekevu. Hapa wengine wamejidanganya. Maisha, matendo, maneno, yatasema ikiwa mtu huyo ana unyenyekevu wa kweli, na mavazi hayo yataambatana na matunda yaliyodhihirishwa. Chemchemi safi haiwezi kutoa maji matamu na machungu. Safisha chemchemi na vijito vitakuwa safi. Nyumba ya Mungu mara nyingi hunajisiwa na watoto wa watunza-sabato. Wazazi wao huwaruhusu kukimbia kuzunguka nyumba, kucheza, kuzungumza, usikivu wa watu, na wadhihirishe hasira zao mbaya katika mikutano ile ile ambapo wamekusanyika ili kumwabudu Mungu. Nimeona kwamba katika kusanyiko la watakatifu utulivu mtakatifu utawale. Lakini nyumba ambamo watu wa Mungu hukusanyika mara nyingi hufanywa kuwa Babeli kamilifu, mahali pa fujo. Hii haimpendezi Mungu. Ikiwa wazazi hawana udhibiti, na hawawezi kuwadhibiti watoto wao katika mkutano, Mungu angependezwa zaidi kubaki nao nyumbani na watoto wao wakorofi. Afadhali wapate hasara ya mikutano, kuliko kuwa na idadi kubwa ya kuudhi, na mikutano yao kuharibika. Wazazi wakiwaacha watoto wao bila kudhibitiwa, bila kutiishwa nyumbani. Hawawezi kuwaruhusu wafanye wapendavyo katika mikutano. Nani anapaswa kuwajibika katika jambo hili? Hakika ni wazazi, awapaswi Kuhisi taabu ikiwa wengine hawataki amani yao ivurugike wanapokutana ili kumwabudu Mungu.

"Wazazi ndi wanapaswa kuwajibika katika jambo hili, na huenda likawapelekea kuona na kutimiza wajibu wenu uliopuuzwa. mkiwabeba watoto wenu hadi kwenye nyumba ya Mungu wanapaswa kueleweshwa kwamba wao ni mahali ambapo Mungu hukutana na watu wake. Hakuna utaratibu ule unaozingatiwa kati ya watunza -sabato katika suala hili ambapo upo katika makanisa ya jina. Wazazi, mnakazi ya kufanya. Kuwatiisha watoto wenu nyumbani, nawe unaweza kuwatawala katika nyumba ya Mungu."— *Spiritual Gifts*, vol. 2, pp. 288, 289.

## *Alhamisi* **Novemba 21**

### 5. HEKIMA NA KUPEWA MAARIFA

**a. Kwa nini kila mmoja wetu anahitaji kuchunguza mtazamo wake kutoka ndani kwenda nje -moyoni, neno, na tendo? 2 Wakorintho 13:5.**

" 'Jijaribuni wenyewe kwamba mmekuwa katika imani; jithibitisheni wenyewe . (2 Wakorintho 13:5). kosoa hasirakwa ukaribu, tabia, mawazo, maneno, mielekeo,makusudi, na matendo. Tunawezaje kuomba kwa akili mambo tunayohitaji isipokuwa tuthibitishe kwa maandiko hali ya afya afya yetu ya kiroho?"—*Selected Messages*, bk. 1, p. 89.

"Ndugu na dada zangu, mnatumia vipi zawadi ya usemi? Je! mmejifunzakudhibiti ulimi ili uweze kutii maagizo ya dhamiri iliyoangaziwa na mapenzi matakatifu? Je! Mazungumzo yenu hayana mizaha, kiburi na uovu, udanganyifu na uchafu? Je! hamna hila mbele za Mungu? Maneno yana nguvu kubwa. Shetani kama ikiwezekana ataufanya ulimi uwe hai katika huduma yake. Kwa sisi wenyewe hatuwezi kumdhibiti mshiriki asiye na nidhamu wa mwili wetu, yaani ulimu. Ni neema ya Bwana ndiyo tumaini letu pekee."—*Testimonies for the Church*, vol. 5, p. 175.

"Yeye anayejiweka mwenyewe bila kujibakiza chini ya uongozi wa Roho wa Mungu, atapata kwamba akili yake inapanuka na kukua. Anapata elimu katika hudumu ya Mungu isiyoegemea upande mmoja na yenye upungufu, inayokuza tabia ya upande mmoja, bali yenye matokeo ya ulinganifu na ukamilifu. Udhaifu ambao umedhihirika katika utashi unaoyumba na tabia isiyo n nguvu, unashindwa, kwa maana ibada na uchaji Mungu humleta mtu huyo katika uhusiano wa karibu sana na Kristo. Yeye ni mmoja na Kristo, mwenye utimamu na nguvu za kanuni. Ufahamu wake uko wazi, naye hudhihirisha hekima hiyo inayotoka kwa Mungu. "—*Selected Messages*, bk. 1, p. 338.

## *Ijumaa* **Novemba 22**

### MASWALI TAFAKARI BINAFSI

**1. Nijibuje ninapokabiliwa na mazungumzo yenye sumu?**

**2. Watu wanaposema mambo ,inaashiria nini hasa kuwahusu?**

**3. Elezea vita vinavyoendelea katika akili ya mwanadamu, na jinsi ambavyo vinaweza kushinda.**

**4. Ni tabia /mielekeo gani ya mgodi ambayo inaweza kuwa inaonyesha maji machafu ndani?**

**5. Jinsi gani na kwa nini namna yangu ya kuzungumza ibadilishwe?**

**Somo la 9** **Sabato, Novemba 30, 2024**

# Upole wa Hekima

**FUNGU LA KUKARIRI: "Ni nani aliye na hekima na ufahamu kwenu? Na aonyeshe kazi zake kwa mwenendo wake mzuri, katika upole wa hekima. " (Yakobo 3:13).**

"Mwokozi wetu alistaajabisha watu kwa usafi wake na maadili yaliyotukuka, huku upendo wake uliwatia moyo kwa shauku. Maskini na wanyenyekevu zaidi hawakuogopa kumkaribia. "— *Gospel Workers (1892)*, p. 261.

**Inapendekezwa kusoma:** *Testimonies for the Church,* vol. 5, pp. 167–177.

## *Jumapili* *Novemba 24*

### 1. "UTAMBUZI" ULIOPINDISHWA

**a. Tunapaswa kujihadhari kabisa na uovu gani mbaya na kwa nini? Yakobo 3:14, 15.**

---

---

"Anayeufungua moyo wake kwa mashauri ya adui, akidhania mabaya, na kutamani wivu, mara kwa mara anayapotosha haya. Nia mbaya, kuiita maono maalum, ubaguzi, au utambuzi katika kugundua hatia na kufahamu nia mbaya za wengine. Anaona kwamba zawadi ya thamani imewekewa dhamana kwake; na hujitenga na ndugu hasa ambao anapaswa kuwa katika maelewano nao; yeye hupanda juu ya kiti cha hukumu, na kufunga moyo wake dhidi ya yule ambaye yeye anadhania kuwa amekosea, kana kwamba yeye mwenyewe yuko juu ya majaribu. Yesu hutengana naye, na kumwacha atembee katika nuru yake aliyoiwasha mwenyewe.

"Mtu yeyote miongoni mwenu asijisifu tena dhidi ya kweli kwa kutangaza kwamba roho hiyo ni tokeo la lazima la kushughulika kwa uaminifu na wakosaji na kusimama katika kuitetea ile kweli. Hekima kama hiyo ina watu wengi wanaoipenda, lakini ni ya udanganyifu na inadhuru. Haiji kutoka juu, bali ni tunda la moyo usiofanywa upya. Mwanzilishi wake ni shetani mwenyewe. Asiwe na mshitaki wa wengine ajidhanie kuwa ana utambuzi; kwani kwa kufanya hivyo huzivisha sifa za shetani mavazi ya haki. Natoa wito kwenu, ndugu zangu, kutakasa hekalu la roho ya vitu hivi vyote vinavyotia unajisi; kwa maana wao ni mizizi ya uchungu. "— *The SDA Bible Commentary [E. G. White Comments]*, vol. 7, pp.936, 937.

## 2. TABIA YA SUMU

**a. Elezea matokeo yasiyoepukika ya husuda na ugonvi. Yakobo 3:16.**

"Mtu mmoja katika taasisi au kanisa anaruhusu mawazo yasiyofaa kwa kuwanenea ndugu maovu, anaweza kuchochea tamaa mbaya zaidi ya moyo wa mwanadamu, na kueneza chachu ya uovu ambayo itatenda kazi kwa wote wanaojiunga. Pamoja naye. Kwa njia hii adui wa haki yote anapata ushindi, na matokeo ya kazi yake ni kubatilisha maombi ya Mwokozi aliposihi kwamba wanafunzi wake wanaweza kuwa kitu kimoja kama yeye alivyo mmoja na Baba. "—*The SDA Bible Commentary [E. G. White Comments]*, vol. 7, p. 937.

**b. Tofauti na mielekeo ya kibinadamu inayoanzishwa na adui wa nafsi zetu kwa jinsi gani tunapaswa kujumuika na wenzetu? Yohana 13:34.**

"Unatoa hukumu kwa watu, na kutoa maoni kuhusu njia zao na tabia zao, wakati hauelewi msimamo wao au kazi yao. Unaangalia vitu kwa mtazamo wako na kisha uko tayari kuhoji au kushutumu mwenendo wanaoufuata, bila kutazama kwa uwazi mambo kila upande. Huna ujuzi wa majukumu ya wengine na haupaswi kuhisi kuwajibika kwa matendo yao, lakini fanya jukumu lako, ukiwaacha wengine na Bwana. Uwe na roho ya uvumilivu, dumisha amani na utulivu wa akili, na uwe mwenye shukrani.

"Wewe u nyeti, unaumizwa haraka sana, na ikiwa neno linasemwa linalopelekea njia tofauti na ile ambayo umekuwa ukifuata, unaumizwa. Unahisi unalaumiwa, na kwamba lazima ujitetee mwenyewe, na kuokoa maisha yako; na katika bidii yako kuokoa maisha yako, unayapoteza. Una kazi ya kufanya ya kufisha nafsi yako na kukuza roho ya kuchukuliana na watu na uvumilivu. "—*Testimonies for the Church*, vol. 2, p. 424.

"Wale wanaokosoa na kuhukumiana wao kwa wao wanavunja amri za Mungu, na ni kosa kwake. Hawampendi Mungu wala viumbe wenzao. Ndugu na dada, tuondoe uchafu wa ukosoaji na tuhuma na malalamiko, na msivae hisia zenu kwa nje. Baadhi ni nyeti sana hivi kwamba hawawezi kujadiliwa nao. Kuwa mwangalifu sana kuhusiana na maana ya kushika sheria ya Mungu, na kuhusu kama unashika au kuvunja sheria. Hilo ndilo ambalo Mungu anataka tuwe makini nalo."—*The SDA Bible Commentary [E. G. White Comments]*, vol. 7, p. 937.

## 3. KUSHUGHULIKIA KUKATA TAMAA

**a. Je, imeandikwa nini kuhusu wale wanaoipenda sheria ya Mungu? Zaburi 119:165.**

“Acha mawazo ya kufikiri kwamba hautumiwi sawa, kwamba umedhulumiwa, kwamba watu wanataka kukuzingira wakudhuru. Macho yako yanakuambia yasiyo kweli. Shetani anakuongoza kuchukua maoni haya yaliyopotoka ya vitu.”— *Testimonies for the Church*, vol. 2, p. 424.

“Ulimwengu unapenda dhambi, na unachukia haki, na hii ndiyo iliyokuwa sababu ya chuki yake kwa Yesu. Wote wanaolikataa pendo lisilo mwisho la Kristo watauona Ukristo kama kitu kinacholeta usumbufu. Nuru ya Kristo hufagilia mbali giza linalofunika dhambi zao, na uhitaji wa matengenezo unakuwa dhahiri. Wakati wale wanaojikabidhi katika nguvu za Roho Mtakatifu wanaanza kujipiga vita wao wenyewe, wale wanaong’ang’ania dhambi hupiga vita ukweli na wale wanaouwakilisha.

“Mapambano hutokea, na wafuasi wa Kristo hushtakiwa kwamba ni wataabishaji wa watu. Lakini ni kule kuwa pamoja na Mungu kunakowaletea uadui dhidi ya ulimwengu. Wanakutana na dhihaka alizofanyiwa Kristo. Wanatembea katika njia aliyopita mtu mwema kuliko wote duniani. Lazima wakutane na mateso kwa furaha, wala si kwa huzuni. Kila moto wa majaribu ni njia ya Mungu ya kuwatakasa. Kila jaribu linawafanya kufaa kuwa watenda-kazi pamoja naye. Kila shida ina nafasi yake katika lile pambano kuu kwa ajili ya haki, na kila moja litaongeza kitu katika furaha ya ushindi wao wa mwisho. Wakiwa na picha hii, kujaribiwa kwa imani yao na subira vitakubaliwa kwa furaha badala ya kuonekana kuwa vitu vya kutisha na vya kujikinga navyo. ”—*The Desire of Ages*, p. 306.

**b. Hata pale tunapotendewa isivyo haki, tunakumbushwa nini? Mathayo 5:11, 12, 41; 1 Petro 4:12–15.**

“Yeye aliye Kichwa kitakatifu cha kanisa, mwenye nguvu zaidi ya washindi, angewaelekeza wafuasi Wake kwenye maisha Yake, taabu Zake, kujinyima kwake, mapambano yake, na mateso, kwa kudharauliwa, kwa kukataliwa, kudhihaki. dharau, matusi, dhihaka, uongo, juu ya njia ya Kalvari hadi kwenye tukio la kusulubiwa, ili waweze kutiwa moyo kusonga mbele kuelekea kwenye alama kwa ajili ya tuzo na thawabu ya mshindi. Ushindi unahakikishwa kupitia imani na utii. Na tufanye matumizi ya maneno ya Kristo kwa kesi zetu binafsi.”—*The Review and Herald*, July 24, 1888.

## 4. HEKIMA KUTOKA JUU

**a. Je, ni sifa gani ya kwanza ya hekima iliyozaliwa Mbinguni— na kwa nini hii ni muhimu kwetu? Yakobo 3:17 (sehemu ya kwanza); Mathayo 5:8.**

---

---

"Katika mji wa Mungu hakitaingia cho chote kinachotia unajisi. Wote ambao watakuwa wakazi kule, watakuwa wamekuwa na moyo safi wakiwa hapa. Ndani ya yule anayejifunza juu ya Yesu, kutaonekana hali inayoendelea ya kuchukia tabia mbaya, lugha chafu, na mawazo yote yasiyofaa. Kristo akikaa moyoni, kutakuwa na usafi na uadilifu wa mawazo na mwenendo.

"Lakini maneno haya ya Yesu, "Heri wenye moyo safi," yana maana sana - sio tu safi katika maana ile ambayo ulimwengu unauelewa usafi, yaani, kuachana na anasa, kuwa safi mbali na tamaa mbaya za mwili, bali ni kuwa mkweli katika makusudi yaliyojificha moyoni na sababu zake zinazopelekea kuyafanya mambo hayo, ni kuachana na kiburi na kutaka makuu, ni kuwa mnyenyekevu, asiyejipenda mwenyewe, mwenye tabia kama ya mtoto mdogo." —*Thoughts From the Mount of Blessing*, pp. 24, 25.

**b. Elezea lengo letu lazima liwe katika kujitayarisha kwa ajili ya Kristo. 1 Yohana 3:2, 3 .**

---

---

"Katika mambo yale yanayotupata kila siku katika maisha yetu, tunatambua wema wake na huruma zake kwa njia ya maongozi yake yanayodhihirishwa kwetu. Tunamtambua yeye kwa tabia ya Mwanawe. Roho Mtakatifu anaichukua ile kweli inayomhusu Mungu na yeye aliyemtuma, na kuifunua katika ufahamu wetu na mioyoni mwetu. Wenye moyo safi wanamwona Mungu katika uhusiano mpya unaowafanya wampende kama Mkombozi wao; na wakati wanatambua usafi na uzuri wa tabia yake, wanatamani sana kufanana naye. Wanamwona yeye kuwa ni Mungu anayetamani sana kumkumbatia mwana aliyetubu, na mioyo yao inajawa na furaha isiyoneneka, yenye utukufu

"Wenye moyo safi wanamtambua Muumbaji katika kazi zake zilizofanywa kwa mkono wake wenye nguvu nyingi, katika vitu vizuri vilivyomo ulimwenguni. Katika Neno lake lililoandikwa wanasoma ufunuo wa rehema zake kwa wazi zaidi, wema wake, na neema yake. Kweli zile zilizofichwa kwa wenye hekima na wenye busara hufunuliwa kwa watoto wachanga. Uzuri na thamani ya ile kweli, mambo ambayo hayatambuliwi na wenye hekima wa dunia, daima huendelea kufunuliwa wazi kwa wale walio na hamu inayomtegemea kama ile ya mtoto ya kutaka kujua na kufanya mapenzi ya Mungu. Tunaitambua, sisi wenyewe, ile kweli tunapokuwa washirika wa tabia ya uungu

"Wenye moyo safi wanaishi mbele za Mungu kabisa kwa kipindi anachowapa katika ulimwengu huu. " —*Ibid.*, pp. 26, 27.

## *Alhamisi* **Novemba 28**

### 5. SIFA MUHIMU ZAIDI

**a. Baada ya usafi, taja sifa tano zinazofuata za hekima iliyozaliwa Mbinguni—ambazo bila hizo mvuto wetu unaharibika. Yakobo 3:17 (sehemu ya kati).**

---

---

"Unahitaji wema, adabu, upole, na unyenyekevu wa Kristo. Una sifa nyingi za thamani ambazo zinaweza kukamilishwa kwa utumishi wa hali ya juu zaidi ukitakaswa kwa Mungu. Unapaswa kuhisi umuhimu wa kuwaendea ndugu zako kwa wema na adabu, si kwa ukali wa kupitiliza. Hutambui madhara unayofanya kwa roho yako kali na ya kutawala kwao. Wahudumu katika mkutano wako wanakatishwa tamaa, wakipoteza ujasiri ambao wanaweza kuwa nao ikiwa ungewapa heshima, wema, ujasiri, na upendo. Kwa namna ya kutenda kwenu mmetenganisha mioyo ya ndugu zenu kutoka kwenu, hivi kwamba mashauri yenu hayakuwa na uvutano mwingi juu yao kwa wema."— *Christian Leadership*, pp. 6, 7.

"Kama matarajio yako hayajafahamika, upo katika hatari ya kukatishwa tamaa na kutotulia, na kutamani mabadiliko. Lazima uepuke tabia ya kukosoa, jitahidi kuvumilia. Kuwa makini kwa kila kitu kinachoashiria roho ya kuhukumu. Haimpendezi MUNGU kwa roho ya namna hii kuwa ndani ya mtumishi Wake wa uzoefu wa muda mrefu. ni vizuri kwa kijana, kama amebarikiwa unyenyekevu na uzuri wa ndani, kudhihirisha shauku na ari, lakini ari ya haraka na roho ya kuhukumu vinapooneshwa na kijana ambaye ana miaka michache tu ya uzoefu, haifai kabisa na inachukiza sana. Hakuna kinachoweza kuharibu ushawishi wake haraka sana kama hiki. Utulivu, upole, uvumilivu, saburi, kutokukasirishwa mapema, akichukuliana mambo yote, akitumaini yote, akistahimili yote haya ni matunda yanayokua juu ya mti wa thamani wa upendo, ambao ni wa ukuaji wa kimbingu. Mti huu ikiwa utatunzwa, utathibitika kuwa wa kijani kibichi wakati wote. Matawi yake hayataoza, majani yake hayatanyauka. Ni wa asili yakutokufa, wa milele, ukimwagiliwa mara kwa mara na umande wa mbinguni. "—*Testimonies for the Church*, vol. 2, pp. 134, 135.

## *Ijumaa* **Novemba 29**

### MASWALI TAFAKARI BINAFSI

1. **Ni katika hali gani ninajaribiwa kuhukumu nia na kuiita utambuzi?**
2. **Je, tabia ya kuwakosoa wengine inavunjaje amri za Mungu?**
3. **Wakati tabia ya sumu inapoanzishwa dhidi yangu, nikumbuke nini?**
4. **Ni nini maana ya kuwa "safi moyoni"?**
5. **Je, ninawezaje kuwa mwenye kufikiwa zaidi—rahisi "kusihi"?**

## Sadaka ya Kwanza ya Sabato kwa ajili ya Makao Makuu ya Union ya Kolombia




Kolombia ni taifa lililo Amerika kusini lenye wakazi ya milioni 51. Viwandani pamoja na mafuta, viwanda, nguo, ujenzi, kilimo, benki na huduma. Kati ya wakazi 73% ya wakazi ni Wakatoliki; 9.1%wanadai kuwa dini zisizo za kikristo 6.9% ni wainjilisti, 6.5% hawana dini, 2.9% ni Waprotestanti, na 0.9 wanajitangaza kuwa hawaamini Mungu. Hali hii inawakilisha changamoto kubwa kwa kanisa la mungu hapa. katika miaka ya 1960, ujumbe wa malaika wa tatu ulifika Kolombia huku taifa hilo likiathirika kiadili kutokana na vita vya wenyewe kwa wenyewe. Katikati ya msukosuko huo, tulifikia washiriki wapatao 100 kufikia mwaka wa 1971 wakati kanisa liliposajiliwa rasmi. Siku hizo wafanyakazi walikuwa wachache, lakini hawakukosa kamwe ujasiri na juhudi ya kutoa kila kitu kwa ajili ya kazi waliyoipenda. Sikuzote tutathamini utegemezo wa wachungaji na wahudumu ambao, wakiacha nchi zao na faraja, walikuja kwa shangwe kutegemeza kazi katika Kolombia—wakijitoa wenyewe kwa moyo wote kueneza ujumbe hapa.

Kwa neema ya Mungu, mwaka 2006, Union ya Kolombia ilipangwa, na leo ina Field tatu. Makao makuu ya Union yako katika eneo la vijijini manispaa ya Barbosa, Santander.

Ili kutumikia ndugu zetu na wale wanaopendezwa zaidi na kweli, tunaona uhitaji wa haraka wa kupanua majengo yaliyopo leo. Hivi sasa, tuna shamba ambapo ofisi zetu, shule za wamishonari na idara ya vyombo vya habari inafanya kazi. Hapa pia tunaandaa makongamano, semina, na mapumziko ya kiroho kwa washiriki wetu na wale wapya wanaopendezwa na ujumbe.

Sehemu ya miundombinu tayari imejengwa kwenye mali hii, na vifaa vya ziada vinaendelea kwa sasa, lakini, tunakosa rasilimali za kuzimaliza. Ndiyo maana tunaomba ukarimu wa kanisa la kifamilia duniani kote. Usaidizi wa matoleo yako ya ukarimu utaturuhusu kuwa na vifaa vinavyofaa zaidi kuhudumia roho zilizo na njaa ya maarifa ya Bwana.

Tunathamini sanamichango yako. Milele pekee ndiyo itaweza kuonyesha ni kiasi gani michango na matoleo yako yatakuwa yamefanya.

*Ndugu na dada zako kutoka Union ya kolombia*

# Kushinda Mtazamo wetu wa Matatizo

**FUNGU LA KUKARIRI: "Basi mtiini Mungu. Mpingeni shetani, naye atawakimbilia. " (Yakobo 4:7).**

"Upendo kwa Ukweli safi, uliotakaswa, upendo kwa Mkombozi Mpendwa, itarahisisha kazi ya kushinda."—Testimonies for the Church, vol. 4, p. 38.

**Inapendekezwa kusoma:** *Testimonies for the Church,* vol. 3, pp. 39–47.

## *Jumapili* **Desemba 1**

### 1. HAKI ISIYO NA UBINAFSI

**a. Taja sifa mbili za mwisho zilizotajwa katika orodha ya hekima iliyozaliwa Mbinguni. Yakobo 3:17 (sehemu ya mwisho).**

---

"Mtume Yuda anasema: "Wahurumieni wengine walio na shaka." Tofauti hii si ya kutekelezwa katika roho ya upendeleo. Hakuna uso unaopaswa kuoneshwa roho inayodokeza: "Ikiwa utanipa upendeleo, nami nitakupendelea." Hii ni sera isiyotakaswa, ya kidunia, na ambayo haimpendezi Mungu. Ni kulipa fadhila na pongezi kwa ajili ya kupata faida. Inaonesha upendeleo kwa baadhi ya watu, wakitarajia kupata manufaa kupitia kwao. Ni kutafuta nia yao njema kwa kujiridhisha binafsi au kujiendekeza mwenyewe, ili tuheshimiwe kwa makadirio makubwa zaidi ya wengine kwamba tunastahili kama sisi wenyewe."—*Testimonies for the Church*, vol. 4, pp. 221, 222.

"Mungu hapendezwi na kazi ya uvivu inayofanywa katika makanisa. Anatarajia mawakili wake wawe wa kweli na waaminifu katika kutoa karipio na kusahihisha. Wanapaswa kufukuza makosa kwa kanuni ambayo Mungu ametoa katika Neno Lake, si kulingana na mawazo na misukumo yao wenyewe. Isiwepo hali ya ukali kutumika, wala kuto kuwa na haki, uharaka, na kazi za msukumo kufanyika. Juhudi zinazofanywa kulisafisha kanisa kutokana na uchafu wa kiadili lazima zifanywe kwa njia ya Mungu. Kusiwe na upendeleo, hakuna unafiki. Ni lazima pasiwepo na watu wapendao, ambao dhambi zao zinachukuliwa kuwa ni dhambi kidogo kuliko za wengine. Loo, ni kiasi gani sisi sote tunahitaji ubatizo wa Roho Mtakatifu. Kisha tutafanya kazi daima na nia ya Kristo, kwa wema, huruma, na faraja, tukionyesha upendo kwa mtenda dhambi huku tukichukia dhambi kwa chuki kamilifu."—*The Ellen G. White 1888 Materials*, p. 144.

## 2. KUMWAKILISHA KRISTO KWA HAKI

**a. Ni kwa jinsi gani Kristo anaweza tu kuwakilishwa ipasavyo katika usemi wetu? Yakobo 3:18.**

---

"Inawezekana kwa midomo yetu tunamkiri Kristo lakini katika matendo yetu tunamkana. Matunda ya Roho yaliyooneshwa maishani ndiyo yanayoonesha kama tumemkiri. Ikiwa tumeacha yote kwa ajili ya Kristo, maisha yetu yatakuwa ya unyenyekevu, mazungumzo yetu yatakuwa ya kimbingu, na mwenendo wetu utakuwa usio na lawama. Ushawishi wenye nguvu, utakaso wa ukweli katika nafsi, na tabia ya Kristo iliyooneshwa katika maisha, huko ndiko kumkiri Yesu. Ikiwa maneno ya uzima wa milele yamepandwa mioyoni mwetu, matunda yatakuwa nihaki na amani. Tunaweza kumkana Kristo maishani mwetu kwa kupenda raha au kujipenda wenyewe, kwa mzaha na kwa utani, na kwa kutafuta heshima ya ulimwengu. Tunaweza kumkana katika sura yetu ya nje kwa kufanana na ulimwengu, kwa sura ya kiburi au mavazi ya ya gharama. Ni kwa kukesha tu kila wakati na kuvumilia kwa maombi yasiyokoma ndipo tunapoweza kuonesha katika maisha yetu tabia ya Kristo au ushawishi wa ukweli unaotakasa.Wengi humfukuza Kristo kutoka kwenye familia zao kutokana na roho ya papara na shauku. Watu wa aina hiyo wana kitu cha kushinda katika jambo hili."—*Testimonies for the Church*, vol. 1, pp. 303, 304.

**b. Ni mielekeo gani ya kawaida ya kibinadamu ambayo hujitokeza katika maisha ya kila siku ambayo kwa kweli inahitaji kukomeshwa—na kwa nini? Yakobo 4:1–3.**

---

"Ni jambo la kusikitisha kutoridhika na mazingira yetu au mazingira ambayo tumewekwa ambapo majukumu yetu yanaonekana kuwa ya unyenyekevu na yasiyo na umuhimu. Wajibu wa kibinafsi na unyenyekevu hayakufurahishi huna pumziko, huna raha, huna kuridhika. Yote haya yanatokana na ubinafsi….

"Wale ambao wanaojiita Wakristo ambao daima hunung'unika na kulalamika, na huonekana kufikiria kwamba furaha na uso wa ucheshi ni dhambi, hawana vazi la Kweli la dini."—*Ibid.*, vol. 3, p. 334.

"Je, nile kiasi maradufu mara kwa mara, kwa sababu ina ladha nzuri, ningewezaje kuinama na kumuomba mungu anisaidie katika kazi yangu ya uandishi, wakati sikuweza kupata wazo kwa sababu ya ulafi wangu? Je, ninaweza kumwomba mungu atunze mzigo huo usio na akili juu ya tumbo langu? Huko kungekuwa ni kumvunjia heshima. Hiyo itakuwa ni kuuliza kula juu ya tamaa yangu. Sasa ninakula kile ninachofikiri ni sawa, na kisha ninaweza kumwomba anipe nguvu ya kufanya kazi ambayo amenipa kufanya. "—*Ibid*., pp. 373, 374.

" Wakati dini ya Kristo inatawala moyoni, dhamiri inakubali, na amani na furaha vinatawala; Shida na mtanziko vinaweza kuzunguka, lakini kuna nuru katika nafsi."—*Ibid*., vol. 4, p. 47.

## 3. KUEPUKA MITEGO YA KAWAIDA

**a. Ni kanuni gani kuu iliyo muhimu katika uhusiano halisi na Kristo, tofauti na imani ya juujuu tu katika jina pekee? Yakobo 4:4.**

“Wale wanaoanza maisha yao ya Kikristo kwa nusu nusu, hatimaye watapatikana wakiwa wameorodheshwa kwenye upande wa adui, chochote ambacho huenda kilikuwa nia yao ya kwanza. Na kuwa muasi, msaliti kwa njia ya Mwenyezi Mungu, ni mbaya zaidi kuliko kifo; maana yake ni upotevu wa uzima wa milele.

“Wanaume na wanawake wenye nia mbili ni washirika bora wa Shetani. Maoni yoyote mazuri wanayoweza kuwa nayo juu yao wenyewe, wao ni wapotoshaji. Wote walio washikamanifu kwa Mungu na kweli wanapaswa kusimama imara kwa ajili ya yaliyo sawa kwa sababu ni sawa. Kufunga nira pamoja na wale ambao hawajawekwa wakfu, na bado kuwa waaminifu kwa ukweli, ni jambo lisilowezekana. Hatuwezi kuungana na wale wanaojitumikia wenyewe, wanaofanya kazi katika mipango ya kidunia, na tusipoteze uhusiano wetu na Mshauri wa mbinguni. Tunaweza kujiokoa kutoka kwa mtego wa adui, lakini tumechubuliwa na kujeruhiwa, na uzoefu wetu ni mdogo.”—*The Review and Herald*, April 19, 1898.

**b. Kwa nini ni lazima tung’oe kwa uthabiti kila mwelekeo mmoja wa wivu? Yakobo 4:5, 6 .**

“Kasoro moja kubwa katika tabia ya Sauli ilikuwa kupenda kwake sifa. Sifa hii ilikuwa na ushawishi unaotawala juu ya matendo na mawazo yake; kila kitu kilionyeshwa na hamu yake ya kusifiwa na kujiinua. Kiwango chake cha mema na mabaya kilikuwa kiwango cha chini cha makofi maarufu. Hakuna mtu aliye salama aishiye ili awapendeze watu, wala hatafuti ukubali wa Mungu kwanza.”— *Patriarchs and Prophets*, p. 650.

“Ni wivu uliomfanya Sauli ahuzunike na kumweka hatarini mtu mnyenyekevu wa kiti chake cha enzi. Je, tabia hii mbaya ya imetenda uovu gani katika ulimwengu wetu! Uadui uleule ulikuwepo ndani ya moyo wa Sauli ambao ulichochea moyo wa Kaini dhidi ya ndugu yake Abeli, kwa sababu matendo ya Abeli yalikuwa ya haki, na Mungu alimheshimu, na matendo yake mwenyewe yalikuwa maovu, na Bwana hangeweza kumbariki. Wivu ni uzao wa kiburi, na ukiwekwa moyoni, utasababisha chuki, na hatimaye kulipiza kisasi na kuua.”—*Ibid*., p. 651.

“Utii, upendo, na shukrani kwa Mungu huweka mwanga wa jua moyoni, ingawa siku inaweza kuwa na mawingu mengi. Kujikana mwenyewe na msalaba wa Kristo uko mbele yako. Je! Utainua msalaba?”—*Testimonies for the Church*, vol. 4, p. 47.

## 4. KUZINGATIA NA KUJITOA

**a. Ni jambo gani muhimu hutupatia ushindi wa kweli na wa kudumu katika Kristo? Yakobo 4:7.**

---

---

"Wengine wanahisi hitaji lao la upatanisho, na kwa kulitambua hitaji hili, na shauku ya mabadiliko ya moyo, mapambano huanza. Kukataa mapenzi yao wenyewe, labda vitu vyao walivyochagua kuvipenda au kuvitafuta, inahitaji juhudi, ambayo wengi husita na kuyumba na kurudi nyuma. Walakini vita hii lazima ipigwe na kila moyo ambao umeongoka Kweli. Lazima tupigane na vishawishi nje na ndani. Lazima tupate ushindi juu ya ubinafsi, tusulubishe mapenzi na tamaa; na kisha tuanze umoja wa roho na Kristo. Kama tawi kavu na lisilo na uhai likiwa limepandikizwa kwenye mti ulio hai, ndivyo tunavyoweza kuwa matawi hai ya Mzabibu wa Kweli. Na matunda yaliyozaliwa na Kristo yatazaliwa na wafuasi Wake wote. Baada ya umoja huu kuundwa, unaweza kuhifadhiwa tu kwa kuendeleza bidii za dhati na juhudi. Kristo hutumia nguvu Zake kuhifadhi na kulinda muunganiko huu mtakatifu, na mwenye dhambi tegemezi, asiyeweza kujisaidia lazima afanye sehemu yake kwa nguvu isiyochoka, vinginevyo shetani kwa nguvu yake ya kikatili, ya hila atamtenga mtu huyo na Kristo.

"Kila Mkristo lazima ajilinde kila wakati, akiangalia kila njia ya moyo/roho ambayo shetani anaweza kuitumia kumfikia. Lazima aombe msaada wa Mungu na wakati huo huo kwa uhakika kabisa aupinge kila mwelekeo wa kutenda dhambi. Kwa ujasiri, kwa imani, kwa bidii isiyochoka, anaweza kushinda. Lakini akumbuke kwamba ili kupata ushindi Kristo lazima akae ndani Yake na yeye ndani ya Kristo."—*Testimonies for the Church*, vol. 5, p. 47.

**b. Paulo anarudiaje maelezo ya Yakobo kuhusu uhai wa kiroho katika maisha ya Kikristo? Warumi 6:6–11.**

---

---

"Mawazo ya ulimwengu, ubinafsi, na tamaa vimekuwa vikitafuna hali ya kiroho na maisha ya watu wa Mungu. "—*Ibid.*, vol. 1, p. 141.

"Tunahitaji imani thabiti zaidi na ibada yenye bidii zaidi. Tunahitaji kufa nafsi zetu, na katika akili na moyo kuthamini upendo wa kuabudu kwa Mwokozi wetu. Tutakapomtafuta Bwana kwa moyo wote tutampata, na mioyo yetu yote itawaka kwa upendo Wake. Nafsi itazama katika kutokuwa na umuhimu, na Yesu atakuwa yote na katika yote kwa nafsi. . . . .

"Ni lazima tumkaribie Mungu. Ni lazima tuwe watenda kazi pamoja Naye, vinginevyo udhaifu na makosa yataonekana katika yote tunayofanya. "— *Ibid.*, vol. 6, p. 51.

## *Alhamisi* **Desemba 5**

### 5. TAFAKARI KWA MAOMBI YA KIASI

**a. Ni uhakikisho gani na mwito gani wa kutafakari kila mmoja wetu katika vita dhidi ya mielekeo yetu wenyewe miovu? Wakolosai 3:1–3; Yakobo 4:8, 9 .**

---

"Haiwezekani kwa yeyote kuutambua ukweli wakati ulimwengu umeyachukua mapenzi yao. Ulimwengu unaingilia kati yao na Mungu, ukificha maono na kupunguza hisia kwa kiwango kwamba hawawezi kuvitambua vitu vitakatifu. Mungu huwaita watu kama hawa: „Itakaseni mikono yenu, enyi wenye dhambi, na kuisafisha mioyo yenu, enyi wenye nia mbili. Huzunikeni na kuomboleza na kulia. Kucheka kwenu na kugeuzwe kuwa kuomboleza, na furaha yenu kuwa hamu." Wale ambao wameichafua mikono yao kwa uchafu wa ulimwengu wanatakiwa kujisafisha kutokana na madoa yake. Wale ambao wanafikiri wanaweza kuutumikia ulimwengu wakiwa wanampenda Mungu wana nia-mbili. Hawawezi kumtumikia Mungu na mali. Ni watu wenye nia mbili, wanaupenda ulimwengu na wanapoteza hisia zote za wajibu wao kwa Mungu, na bado wanakiri kuwa ni wafuasi wa Kristo. Wao hawako kwa hiki wala kile. Wataupoteza ulimwengu wote endapo hawataitakasa mikono yao na kusafisha mioyo yao kwa kutii kanuni safi za ukweli. "—*Testimonies for the Church*, vol. 1, pp. 530, 531.

**b. Ni nini kinatokea tunaposujudu mbele za Mungu kwa unyenyekevu? Zaburi 34:18; 1 Petro 5:6, 7 .**

---

"Ikiwa sasa utanyenyekea mbele za Mungu, na kuungama makosa yako, na kumrudia kwa moyo wako wote, unaweza kuwa bado familia yenye furaha. Kama hautafanya hivi, lakini ukaishia kuchagua njia yako mwenyewe, furaha yako ipo ukingoni. "—*Ibid.*, vol. 2, p. 304.

## *Ijumaa* **Desemba 6**

### MASWALI TAFAKARI BINAFSI

1. **Nikichunguza kwa kina nia yangu ya ndani, ni katika maeneo gani ninaweza kuwa mnafiki?**
2. **Taja baadhi ya njia ambazo kwazo maneno yetu mara nyingi humwakilisha Kristo vibaya.**
3. **Ni katika maana gani wivu ni kukana imani kwa uzito—na kumtukana Mungu?**
4. **Kwa nini nahitaji kuwa mfu kwa nafsi yangu ili niwe hai katika**

**Kristo?**

5. **Je, somo hili lina muhtasari gani baadhi ya masuala ya kweli ninayohitaji kushinda?**

**Somo la 11** **Sabato, Desemba 14, 2024**

# Kufuata Mwonekano Mnyenyekevu

**FUNGU LA KUKARIRI: "Jidhilini mbele za Bwana, naye atawakuza. " (Yakobo 4:10).**

"Tunapofuata njia ya unyenyekevu ya utiifu, tunaacha njia angavu ya kuelekea mbinguni kwa wengine kutembea ndani yake. Ni fursa yetu kuwa na uzoefu wa kina zaidi katika mambo ya Mungu."—*The Signs of the Times,* March 17, 1890.

**Inapendekezwa kusoma:** *Testimonies for the Church,* vol. 2, pp. 41–44, 678–686.

## *Jumapili* *Desemba 8*

### 1. KUEPUKA UTAMBUZI WA UONGO

**a. Ni tabia gani mbaya sana inayohitaji kuachwa na wote wanaodai kuwapenda ndugu zao, na kwa nini? Yakobo 4:11, 12 .**

---

---

---

"Haipaswi kuchukuliwa kuwa jambo jepesi kuwasema vibaya wengine au kujifanya waamuzi wa nia au matendo yao."—*Patriarchs and Prophets*, p. 385.

"Thamani ya kweli ya maadili haitafuti kujitengenezea nafasi kwa kufikiria na kusema maovu, kwa kuwashusha thamani wengine. Wivu wote, matukano yote, pamoja na kutokuamini kote, lazima viondolewe mbali na watoto wa Mungu."— *Our High Calling*, p. 234.

"Juhudi za dhati zinapaswa kufanywa katika kila kanisa katika kuondoa kuzungumza maovu na roho ya ukosoaji miongoni mwa washiriki kama dhambi zinazozaa maovu makubwa zaidi ndani ya kanisa. Ukali na kutafuta makosa lazima vikemewe kama kazi za Shetani. Upendo na ujasiri wa pande zote lazima uhimizwe na kuimarishwa kwa washiriki wa kanisa. Hebu wote, kwa kumcha Mungu na kwa upendo kwa ndugu zao, wazibe masikio yao dhidi ya masengenyo na mashutumu. Mwelekezeni mchonganishi au mleta habari (nipashe) kwenye mafundisho ya Neno la Mungu. Mwambieni ayatii Maandiko na apeleke malalamiko yake moja kwa moja kwa wale anaofikiria kuwa wamekosea. Hatua hii ya umoja ingeleta mafuriko ya nuru ndani ya kanisa na kufunga mlango wa mafuriko ya uovu. Hivyo Mungu atatukuzwa, na roho nyingi zitaokolewa. "—*Testimonies for the Church,* vol. 5, pp. 609, 610.

## 2. KUCHUKULIA NURU KWA UZITO

**a. Tunapofanya mipango, tunahitaji kukumbuka nini kila mara? Zaburi 16:8; Yakobo 4:10, 13–16 .**

---

---

"Jiweke wakfu kwa Mungu asubuhi; fanya hii iwe kazi yako ya kwanza kabisa. Maombi yako na yawe, 'Nichukue, Ee Bwana, kuwa wako kabisa. Ninaweka mipango yangu yote miguuni pako. Nitumie leo katika huduma Yako. Kaa nami, na kazi yangu yote itekelezwe ndani yako.' Hili ni jambo la kila siku. Kila asubuhi jiweke wakfu kwa Mungu kwa ajili ya siku hiyo. Peleka mipango yako yote Kwake, ili itekelezwe au uiache kama vile riziki Yake itakavyoonyesha. Hivyo siku baada ya siku unaweza kuwa unayatoa maisha yako mikononi mwa Mungu, na hivyo maisha yako yatafinyangwa zaidi na zaidi baada ya maisha ya Kristo." —*Steps to Christ*, p. 70.

**b. Elezea wajibu mzito na uwajibikaji tulionao kila mmoja wetu kwa nuru ya mbinguni inayotolewa kwetu katika nyanja zote za maisha. Yakobo 4:17; Mathayo 12:31, 32 .**

---

---

"Si Mungu anayepofusha macho ya watu na kuifanya mioyo yao kuwa migumu. Yeye huwapelekea nuru ili kusahihisha makosa yao, na kuwaongoza katika njia salama; macho yao hupofushwa na mioyo yao kufanywa migumu kwa sababu ya wao kuikataa nuru hiyo. Mara nyingi hali hii hutokea taratibu, na kama vile pasipo kuonekana. Nuru huja moyoni kwa njia ya neno la Mungu, kupitia watumishi wake, au kupitia kazi za moja kwa moja za Roho wake; lakini pale hata mshale mmoja wa nuru unapopuuzwa, kunakuwa na sehemu ya uhafifisho wa uelewa wa kiroho, na udhihirisho wa pili wa nuru huonekana kwa uwazi uliopungua. Hivyo giza huongezeka, mpaka kunapokuwa usiku moyoni. "— *The Desire of Ages*, p. 322.

"Ni hatari kubwa kutamka neno ulilo na mashaka nalo, hatari ya kuhoji na kukosoa nuru ya kimbingu. Mazoea ya kupinga pasipo uangalifu na heshima huathiri tabia, na huelekeza katika utovu wa heshima na kutoamini. Watu wengi wanaokuwa na mazoea haya wameendelea hivyo pasipo kutambua hatari iliyopo, mpaka walipokuwa katika hali ya kupinga na kukataa kazi ya Roho Mtakatifu. "—*Ibid.*, p. 323.

"Watu wanapozungumziwa kuhusu afya, mara nyingi husema: „Tunajua mengi zaidi kuliko tunavyofikiri." Hawatambui kwamba wanawajibika kwa kila miale ya nuru kuhusiana na ustawi wao wa kimwili, na kwamba kila tabia yao iko wazi kwa ukaguzi wa Mungu. "—*Testimonies for the Church*, vol. 6, p. 372.

## 3. UTAJIRI KUPITA KIASI

**a. Ni maonyo gani yanatolewa kuhusiana na majaribu yanayo wazunguka wale walio barikiwa mali nyingi kuliko wengine? Yakobo 5:1.**

"Wachungaji hawapaswi kutumia maneno ya kusifia au kuwapendelea watu. Kumekuwa na hatari kubwa ya kukosea hapa, na bado ipo, ya kufanya tofauti kidogo na matajiri, au kuwabembeleza kwa umakini maalum, ikiwa sio kwa maneno. Kuna hatari ya „kupendezwa na watu" kwa sababu ya faida, lakini kwa kufanya hivyo masilahi yao ya milele yako hatarini. Mchungaji anaweza kuwa kipenzi maalum cha mtu tajiri, na anaweza kuwa huru sana pamoja naye; hii humtukuza mchungaji, na yeye pia humwaga sifa juu ya fadhili za mfadhili wake. Jina lake linaweza kuinuliwa kwa kuonekana kwenye chapisho, na bado mfadhili huyo huria anaweza kuwa hafai kabisa sifa aliyopewa. Ukarimu wake haukutokana na kanuni ya kina, inayoishi ya kutenda mema na mali zake, kuendeleza kazi ya Mungu kwa sababu aliithamini, bali ulitoka katika nia ya ubinafsi, hamu ya kufikiriwa kuwa ni mkarimu. Anaweza kuwa ametoa kutoka kwa msukumo, lakini ukarimu wake hauna kina cha kanuni. Anaweza kusukumwa na kusikiliza ukweli wenye kuchochea ambao kwa muda huo ulifungua kamba zake za mkoba; lakini, baada ya yote, ukarimu wake hauna nia ya kina. Anatoa kwa kujionesha; mkoba wake unafunguliwa kimkakati na hufungwa salama kimkakati. Hastahili pongezi, kwa maana yeye kwa kila hali na neno ni mtu bahili na asipoongoka kabisa, mkoba wake na vyote vitasikia kemeo linalokausha: „Nendeni sasa, enyi matajiri, kulia na kuomboleza kwa ajili ya huzuni zitakazo kuja juu yenu . Utajiri wako umeharibika, na mavazi yako yameliwa na nondo. Hao wataamka mwishowe kutoka kwa udanganyifu wa kutisha. Wale ambao walisifu ukarimu wao maonesho walimsaidia Shetani kuwadanganya na kuwafanya wafikiri kwamba walikuwa wakarimu sana, wenye kujitolea sana, wakati hawakujua kanuni za kwanza za ukarimu au kujitolea"—*Testimonies for the Church,* vol. 1, pp. 475, 476.

**b. Tutaboresha vipi vipaumbele vyetu kuhusu pesa? Mithali 11:4 .**

"Kwa kutenda, ukarimu hupanua na kuimarisha, mpaka inakuwa kanuni nakutawala ndani ya nafsi. Ni hatari sana kwa roho kuruhusu ubinafsi na uchoyo vipate nafasi hata ndogo moyoni. "—*Ibid*., vol. 3, pp. 548, 549.

## 4. KUACHA SANAMU

**a. Ni nini mara nyingi sababu ya watu kupata utajiri? Yakobo 5:2 (sehemu ya kwanza).**

"Katika kizazi hiki hamu ya kupata faida ni shauku kuu. Utajiri mara nyingi hupatikana kwa ulaghai. Kuna watu wengi wanaohangaika na umaskini, wanalazimika kufanya kazi kwa bidii kwa ujira mdogo, hawawezi kupata hata mahitaji duni ya maisha. Taabu na kunyima, bila matumaini ya mambo bora, hufanya mzigo wao kuwa mzito. Wakiwa wametunzwa na kudhulumiwa, hawajui waelekee wapi kupata nafuu. Na haya yote ili matajiri waunge mkono ubadhirifu wao au watimize tamaa yao ya kulimbikiza!

"Kupenda pesa na kujionyesha kumeifanya dunia hii kuwa pango la wezi na wanyang'anyi. Maandiko huonyesha uchoyo na uonevu utakaokuwapo kabla tu ya kuja kwa Kristo mara ya pili."—*Prophets and Kings*, pp. 650, 651.

**b. Ni nini kinachochochea sehemu kubwa ya ulimwengu leo—na ni mwito gani unaohitaji kufanywa kwa wale wanaoongozwa nao? 1 Timotheo 6:9, 10; Kumbukumbu la Torati 8:18, 19 .**

"Biblia haimlaumu mtu kwa kuwa tajiri, ikiwa amepata utajiri wake kwa uaminifu. Sio pesa, bali kupenda pesa, ndio chanzo cha maovu yote. Mungu ndiye awapaye wanadamu uwezo wa kupata mali; na mikononi mwa yule anayetenda kama wakili wa Mungu, akitumia mali yake bila ubinafsi, mali ni baraka, kwa aliye nayo na kwa ulimwengu pia. Lakini wengi, wakiwa wamezama katika kupendezwa kwao na hazina za kilimwengu, wanakuwa wasiojali madai ya Mungu na mahitaji ya wanadamu wenzao. Wanachukulia mali zao kama njia ya kujitukuza. Wanaongeza nyumba kwa nyumba, na ardhi kwa ardhi; wanazijaza nyumba zao anasa, huku wote wanaowazunguka ni wanadamu katika taabu na uhalifu, katika magonjwa na kifo. Wale wanaotoa maisha yao kwa kujitanguliza wenyewe wanasitawisha ndani yao wenyewe, si sifa za Mungu, bali sifa za yule mwovu.

"Watu hawa wanahitaji injili. Wanahitaji kugeuzwa macho yao kutoka kwenye ubatili wa vitu vya kimwili ili kutazama thamani ya utajiri wa kudumu. . . .

"Wengine wamefaa kufanya kazi kwa madarasa ya juu. Hawa wanapaswa kutafuta hekima kutoka kwa Mungu ili kujua jinsi ya kuwafikia watu hawa, wasiwe na mazoea ya kawaida tu nao, bali kwa juhudi binafsi na imani iliyo hai ili kuwaamsha wapate mahitaji ya nafsi, ili kuwaongoza kwenye ujuzi wa ukweli. kama ilivyo ndani ya Yesu."—*The Ministry of Healing*, pp. 212, 213.

## *Alhamisi* **Desemba 12**

### 5. KUANGALIA ZAIDI YA MALI

**a. Elezea matokeo ya faida iliyopatikana kwa njia isiyo halali. Yakobo 5:2 (sehemu ya mwisho).**

"Utajiri huleta majukumu makubwa. Kupata utajiri kwa njia isivyo haki, kwa hila katika biashara, kwa kumwonea mjane na yatima, au kwa kujilimbikizia mali na kupuuza mahitaji ya mhitaji, mwishowe italeta adhabu ya haki iliyoelezewa na mtume aliyevuviwa."—Testimonies for the Church, vol. 2, p. 682.

**b. Je, ni ujumbe gani maalum wa Mungu kuhusu utajiri? 1 Timotheo 6:17–19.**

---

---

"Wanyenyekevu na maskini zaidi wa wanafunzi wa Kweli wa Kristo, ambao ni matajiri wa matendo mema, wamebarikiwa zaidi na ni wa thamani mbele za Mungu kuliko watu wanaojivunia utajiri wao mwingi. Wao ni wenye heshima zaidi katika nyua za mbinguni kuliko wafalme waliotukuka sana na wakuu wasio matajiri kwa Mungu.. . . .

"Wale wanaojilimbikizia mali au kuwekeza kwa kiasi kikubwa katika ardhi, wakati wakinyima familia zao faraja ya maisha, wanatenda kama watu wenye wazimu. Hawaziruhusu familia zao kufurahia vitu ambavyo Mungu amewapatia tele. Pamoja na kwamba wana mali nyingi, familia zao hulazimishwa mara kwa mara kufanya kazi zaidi ya nguvu zao kutunza mali zaidi za kujilimbikizia. Ubongo, mfupa, na misuli hutumikishwa kwa kiasi kikubwa kujilimbikizia, na majukumu ya dini na ya Kikristo yanapuzwa. Kazi, kazi, kazi, ni tamaa toka asubuhi hadi usiku.

"Wengi hawaoneshi shauku ya dhati ya kujifunza mapenzi ya Mungu na kuelewa madai Yake kwao. Wengine wanaojaribu kuifundisha Kweli kwa wengine wao wenyewe hawalitii Neno la Mungu. Zaidi kazi ya Mungu inavyokuwa na waalimu kama hao, ndivyo itakavyosonga mbele kidogo. "— Ibid., pp. 682, 683.

## *Ijumaa* **Desemba 13**

### MASWALI TAFAKARI BINAFSI

1. **Ninapokazia sana mapungufu ya wengine, ninafanya nini?**
2. **Elezea jinsi Roho Mtakatifu anahuzunishwa tunapopuuza nuru iliyotumwa na Mbingu.**
3. **Ni jinsi gani watu matajiri na wachungaji wao wanaweza kunaswa?**
4. **Kwa nini pupa inaongezeka na kwa nini tunapaswa kuiepuka sasa kuliko wakati mwingine wowote?**
5. **Eleza uzuri na faida za unyenyekevu katika Kristo.**

# Kuzingatia Mbinguni

**FUNGU LA KUKARIRI: "Nanyi vumilieni, mthibitishe mioyo yenu, kwa maana kuja kwake Bwana kunakaribia. " (Yakobo 5:8).**

"Unahitaji kuvikwa daima haki ya Kristo. Unahitaji kukumbuka kwamba wewe ni mtoto wa Mungu, na kwamba unapaswa kuwa na moyo mpole, fadhili, mvumilivu. Angalia kwa makini kwamba ubinafsi na choyo havitakaa ndani ya nafsi yako."— *Manuscript Releases*, vol. 13, p. 288.

**Inapendekezwa kusoma:** *Early Writings,* pp. 72, 73.

## *Jumapili* *Desemba 15*

### 1. MUDA WA KUTATHIMINI UPYA!

**a. Ni nini kitatokea hivi karibuni kwa vitu vilivyothaminiwa sana na mara nyingi vinavyotamaniwa tangu zamani—na hii inapaswa kutukumbusha nini? Isaya 31:6, 7 .**

---

---

"Ni upendo wa ubinafsi wa pesa uliotumiwa vibaya ndio mzizi wa maovu yote. Utajiri utathibitika kuwa baraka ikiwa tunauona kuwa wa Bwana, kupokelewa kwa shukrani na kurudishwa kwa shukrani kwa Mpaji.

"Lakini utajiri usioelezeka una thamani gani ikiwa umehifadhiwa katika majumba ya kifahari au katika hisa za benki? Je, hawa wana uzito gani kwa kulinganisha na wokovu wa nafsi moja ambayo Mwana wa Mungu asiye na mwisho amekufa kwa ajili yake?"—*Testimonies for the Church*, vol. 6, p. 453.

"Wale wanaochagua kutoa udhuru na kuendelea katika dhambi na kupatana na ulimwengu wataachwa katika sanamu zao…. Wakati Kristo atakapokuja katika utukufu wake na utukufu wa Baba Yake, pamoja na malaika wote wa mbinguni wakimzunguka, wakimsindikiza njiani kwa sauti za ushindi, wakati sauti ya muziki unaopendeza ikisikika katika sikio, ndipo wote watavutiwa; hakutakuwa na mtazamaji mmoja asiyejali. Nadharia hazitaijaza roho wakati huu. Rundo La dhahabu ya mtu mwenye choyo, liliyofurahisha macho yake, halina mvuto tena. Miji na majumba ya kifalme ambayo watu wenye kiburi wa dunia wamejenga, na ambayo imekuwa sanamu zao, na watayaacha kwa hiyari na machukio."—*Ibid*., vol. 2, p. 41.

## 2. KABLA HUJACHELEWA. . .

**a. Maandiko yanawaonyeshaje wale ambao, kwa kuahirisha mambo, wanapoteza nafasi yao ya kumheshimu Mungu kwa mali zao? Hosea 4:17; Mathayo 25:11,**

**b. b.Elezea matokeo ya mwisho ya wote—pamoja na wale wanaokiri ukweli wa sasa—ambao kwa ubinafsi wanashikilia mali. Yakobo 5:3.**

"[Yakobo 5:1–3 Imenukuliwa] Niliona kwamba maneno haya ya kuogofya yanatumika hasa kwa matajiri ambao wanadai kuamini ukweli wa leo. Bwana anawaita watumie mali zao kuendeleza mashauri yake. Fursa zinawasilishwa kwao, lakini hufunga macho yao kwa mahitaji ya kazi hiyo, na kushikamana sana na hazina yao ya kidunia. Upendo wao kwa ulimwengu ni mkubwa kuliko upendo wao kwa ukweli, upendo wao kwa wanadamu wenzao, au upendo wao kwa Mungu. Anahitaji mali zao, lakini wao kwa ubinafsi, kwa tamaa, huhifadhi kile walicho nacho. Wanatoa kidogo sasa na kisha kupunguza dhamiri zao, lakini hawajashinda upendo wao kwa ulimwengu huu. Hawatoi dhabihu kwa ajili ya Mungu. Bwana ameinua wengine ambao wanathamini uzima wa milele, na ambao wanaweza kuhisi na kutambua kitu cha thamani ya roho, na wamejitolea kwa hiari mali zao za kuendeleza kazi ya Mungu. Kazi inafungwa; na hivi karibuni mali za wale ambao wameweka utajiri wao, mashamba yao makubwa, ng'ombe zao, nk, havitahitajika. Nilimwona Bwana akigeukia wale wenye hasira, na akiwa na ghadhabu, alirudia maneno haya: "Nendeni sasa, enyi matajiri." Amewaita, lakini hamkusikia. Upendo wa ulimwengu huu umezamisha sauti yake. Sasa hana faida tena kwenu, na anawaacha muende, akiwasihi: "Nendeni sasa, enyi matajiri."

"Lo, niliona ni jambo baya sana kuachwa na Bwana – jambo la kutisha kushikilia mali inayoweza kuharibika hapa, wakati Yeye amesema kwamba ikiwa tutauza na kutoa sadaka, tunaweza kuweka hazina mbinguni. Nilioneshwa kwamba wakati kazi inamalizika, na ukweli unaendelea kwa nguvu kubwa, watu hawa matajiri wataleta uwezo wao na kuuweka miguuni mwa watumishi wa Mungu, wakiwasihi waupokee. Jibu kutoka kwa watumishi wa Mungu litakuwa: "Nendeni sasa, enyi matajiri. Mali zenu hazihitajiki. Mliizuia wakati mngeweza kufanya vizuri nayo katika kuendeleza kusudi la Mungu. Masikini wameteseka; hawakubarikiwa na mali zenu. Mungu hatakubali utajiri wako sasa. Nendeni zenu sasa, enyi matajiri."—*Testimonies for the Church*, vol. 1, pp. 174, 175.

## 3. KUJIFUNZA KANUNI YA DHAHABU

**a. Waliofanikiwa mara nyingi huwatendeaje wale wanaowaajiri— au wanaonunua kutoka kwao—na ni nini tunapaswa kukumbuka? Yakobo 5:4–6; Mathayo 7:12.**

---

"Mungu hayumo katika utajiri wote unaopatikana. Shetani mara nyingi ana uhusiano mwingi na upatikanaji wa mali kuliko Mungu. Sehemu kubwa ya utajiri huo hupatikana kwa kumkandamiza aliyeajiriwa katika mshahara wake. Tajiri mwenye tamaa ya asili hupata utajiri wake kwa kumkandamiza aliyeajiriwa, na kuchukua faida ya watu binafsi popote awezapo, na hivyo kuongeza hazina ambayo itakula mwili wake kama moto.

"Uaminifu wa dhati, na hatua za kuheshimika, havijachukuliwa na baadhi ya watu. Hao lazima wachukue hatua zilizo tofauti sana na wafanye kazi haraka kukomboa wakati. Watunza Sabato wengi wana makosa katika jambo hili. Wanachukua fursa kujinufaisha kwa ajili ya ndugu zao masikini, na wale walio na utajiri zaidi kuliko thamani halisi ya vitu, zaidi ya vile ambavyo wangeweza kulipia vitu vile vile, wakati ndugu hawa hawa wanaaibika na kufadhaika kwa kukosa pesa. Mungu anajua mambo haya yote. Kila tendo la ubinafsi, kila ulafi wa kutamani, utaleta thawabu yake.

"Niliona kuwa ni ukatili na ukosefu wa haki kutofikiria hali ya ndugu. Ikiwa anafadhaika, au ni maskini, lakini anafanya kadri awezavyo, upendeleo unapaswa kufanywa kwa ajili yake, na hata thamani kamili ya vitu anavyoweza kununua kwa matajiri haipaswi kuulizwa; lakini wanapaswa kuwa na matumbo ya huruma kwake. Mungu atakubali matendo mema kama hayo, na mtendaji hatapoteza thawabu yake. Lakini kumbukumbu ya kutisha inasimama dhidi ya watunza Sabato kwa vitendo vinavyokaribiana na kutamani."—*Testimonies for the Church*, vol. 1, pp. 175, 176.

**b. Katika nyakati za awali, waumini walishiriki vipi kwa uhuru? 2Wakorintho 8:1, 2 .**

---

"Nilioneshwa nyuma wakati ambapo kulikuwa na wachache tu waliosikiliza na kuukubali ukweli. Hawakuwa na bidhaa nyingi za ulimwengu huu. Matakwa ya kazi hiyo yaligawanywa kati ya wachache sana. Halafu ilikuwa ni lazima kwa wengine kuuza nyumba zao na mashamba, na kupata nafuu ya kuwahudumia kama makazi, au nyumba, wakati mali zao ziliazimishwa kwa uhuru na ukarimu kwa Bwana, kuchapisha ukweli, na vinginevyo kusaidia katika kuendeleza kazi ya Mungu. Nilipowaangalia watu hawa waliojitoa muhanga, niliona kwamba walikuwa wamejinyima faragha kwa faida ya kazi. Nikaona malaika amesimama karibu nao, akiwaelekeza juu, na kusema: "Mna mifuko mbinguni! Mna mifuko mbinguni ambayo haichakai. Vumilieni hadi mwisho, na thawabu yenu itakuwa kubwa."—*Ibid.*, p. 176.

## 4. UADILIFU MUHIMU KWA LEO

**a. Katika kukuza tabia zetu, kwa nini subira ni muhimu sana? Yakobo 5:7.**

" 'Mkulima hungoja matunda ya nchi yaliyo ya thamani, huvumilia kwa ajili yake, hata yatakapopata mvua ya kwanza na ya Mwisho.' Yakobo 5:7. Kwa hiyo Mkristo anapaswa kungojea kwa uvumilivu matunda ya neno la Mungu maishani mwake. Mara nyingi tunapoomba kwa ajili ya neema za Roho, Mungu hufanya kazi ya kujibu maombi yetu kwa kutuweka katika mazingira ya kuendeleza matunda haya; lakini hatuelewi kusudi lake, na tunashangaa, na tunafadhaika. Hata hivyo hakuna anayeweza kuendeleza neema hizi isipokuwa kupitia mchakato wa kukua na kuzaa matunda. Sehemu yetu ni kupokea neno la Mungu na kulishika kwa nguvu, tukijitoa wenyewe kikamilifu chini ya udhibiti wake, na kusudi lake ndani yetu litatimizwa.

" 'Mtu akinipenda,' Kristo alisema, 'atalishika neno langu; na Baba yangu atampenda, nasi tutakuja kwake, na kufanya makao kwake.' Yohana 14:23. maneno ya mtu mwenye nguvu, akili kamilifu itakuwa juu yetu; kwa kuwa tuna muunganisho ulio hai na chanzo cha nguvu za kudumu. Katika maisha yetu ya kiungu tutaletwa katika utumwa wa Yesu Kristo. Hatutaishi tena maisha ya kawaida ya ubinafsi, lakini Kristo ataishi ndani yetu. Tabia yake itatolewa tena katika asili yetu. Hivyo tutazaa matunda ya Roho Mtakatifu—'mmoja thelathini, na huyu sitini, na huyu mia."—*Christ's Object Lessons*, p. 61.

**b. Unapojaribiwa na kufadhaika kuhusu kuongezeka kwa uovu kwenye sayari hii, kwa nini uaminifu wa subira husaidia sana? Yakobo 5:8; Luka 21:19.**

"Ulimwengu umekuwa na ujasiri katika uvunjaji wa sheria ya Mungu. Kwa sababu ya uvumilivu Wake wa muda mrefu, wanadamu wamekanyaga mamlaka Yake. Wametia nguvu wao kwa wao katika dhuluma na ukatili kwa urithi wake, wakisema, 'Mungu ajuaje? Yako maarifa kwake aliye juu?' Zaburi 73:11 . Lakini kuna mstari zaidi ambayo hawawezi kupita. Umekaribia wakati ambapo watakuwa wamefikia kikomo. Hata sasa wamekaribia kuvuka mipaka ya subira ya Mungu, mipaka ya neema yake, mipaka ya rehema zake. Bwana atakusudia kudhihirisha heshima yake mwenyewe, kuwakomboa watu wake, na kukandamiza kuinuka kwa udhalimu."—*Ibid.*, uk. 177, 178."—*Ibid.*, pp. 177, 178.

## *Alhamisi* **Desemba 19**

### 5. MIFANO YA KUTUTIA NGUVU

**a. Katika uwezo wa kanisa, ni nini tunachozingatia mara kwa mara—na ni nini tunapaswa kuweka akilini badala yake? Mambo ya Walawi 19:18; Yakobo 5:9, 10**

---

"Habili, Mkristo wa kwanza kabisa katika watoto wa Adamu, alikufa kifo cha mfiadini. Henoko alitembea na Mungu, na ulimwengu haukumjua. Nuhu alidhihakiwa kama shupavu wa dini asiyetumia akili na mvumishaji wa mambo ya kuogofya. "Wengine walijaribiwa kwa dhihaka na mapigo, naam, kwa mafungo, na kwa kutiwa gerezani." "Lakini wengine waliumizwa vibaya hata kuuawa, wasikubali ukombozi, ili wapate ufufuo ulio bora." Waebrania 11:36,35.

"Katika nyakati zote wajumbe wa Mungu aliowachagua wamedhihakiwa na kuteswa, lakini kwa mateso yao, maarifa ya kumjua Mungu yalienezwa kila mahali. Kila mwanafunzi wa Kristo hana budi kuingia katika safu za jeshi lake na kuiendeleza mbele kazi ile ile, akijua kwamba maadui wa kazi hiyo hawawezi kufanya lo lote dhidi ya hiyo kweli, bali kwa ajili ya hiyo kweli. Mungu anakusudia kwamba kweli yake italetwa mbele ya watu na kuwa somo la kuchunguzwa na kujadiliwa, hata kwa njia ya dharau inayowekwa juu yake. Akili za watu ni lazima zitikiswe sana; kila mabishano, kila shutuma, kila juhudi ya kuzuia uhuru wa dhamiri, ni njia anayotumia Mungu kuziamsha akili za watu ambazo, vinginevyo, zingeweza kulala usingizi.

"Ni mara nyingi jinsi gani matokeo hayo yameonekana katika historia ya wajumbe wa Mungu! Stefano, mwenye tabia nzuri na mnenaji mwenye ufasaha, alipopigwa mawe na kufa kutokana na uchochezi wa Baraza Kuu la Kiyahudi (Sanhedrin), hapakuwa na hasara yo yote kwa kazi ya Injili. Nuru ile ya mbinguni iliyoutukuza uso wake, huruma ya Mungu aliyoionesha katika ombi lake alipokuwa akifa, vilikuwa kama mshale mkali uliomchoma mioyoni mwake yule Mwanabaraza la Kiyahudi aliyesimama karibu pale, na Sauli, yule Farisayo mtesaji, akawa chombo kiteule cha Mungu ili alichukue jina la Kristo mbele ya mataifa, na wafalme, na wana wa Israeli "— *Thoughts From the Mount of Blessing*, pp. 33, 34.

## *Ijumaa* **Desemba 20**

### MASWALI TAFAKARI BINAFSI

1. **Je, ninahitaji kutambua nini kuhusu thamani ya pesa yangu?**
2. **Nini maana ya changamoto ya Kristo katika Yakobo 5:1?**
3. **Ni udhaifu gani ninaweza kuwa na hatia kuhusiana na mwingiliano wa kifedha?**
4. **Hatimaye, subira itang'aaje kama wema wa adili miongoni mwa watu wa Mungu?**
5. **Je, wafia imani walioteswa katika historia wamewekaje mtazamo wao?**

# Kudumu kwa Imani

**FUNGU LA KUKARIRI: "Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, mpate kuponywa. Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana, akiomba kwa bidii." (Yakobo 5:16).**

"Sala ya unyenyekevu, yenye bidii itaokoa nafsi kutoka kwenye kifo, na kuungama na kurudishiwa kutaficha wingi wa dhambi."—*The Review and Herald*, December 16, 1902.

**Inapendekezwa kusoma:** *The Ministry of Healing*, pp. 225–233; *Testimonies for the Church,* vol. 3, pp. 271–293.

## *Jumapili* *Desemba 22*

### 1. MATUMAINI

**a. Ayubu anatambuliwa kwa wema gani hasa—na hii inatuambia nini kuhusu Mungu? Yakobo 5:11.**

"[Mungu] na kuyakubali majuto yao. Hutazamia shukrani kutoka kwetu, kama vile mamamzaziamtazamiavyo mtoto wake mpendwa kumchekea na kumwonesha kwamba amemjua. Mungu ataka tufahamu jinsi anavyotupenda na kutuhurumia kwa moyo wake wote. Anatuita tumwendee na taabu zetu naye atatusaidia; tumpelekee huzuni zetu, naye atatufariji kwa upendo wake; tumpelekee majeraha yetu, naye atatuponya; tumpelekee udhaifu wetu, naye atatuwezesha kwa uwezo wake; tumwendee jinsi tulivyo bila kitu, naye atatujaza. Hakuna hata mtu mmoja ambaye amekwenda kwake na kukatishwa tamaa kwa kutokupata msaada aliotumainia. "Wakamwelekea macho wakatiwa nuru: wala nyuso zao hazitaona haya.'

"Wale wanaomtafuta Mungu faraghani, na kumweleza Bwana haja zao, na kumwomba msaada wake, hawatamsihi bure bila kupata. "—*Thoughts From the Mount of Blessing*, pp. 84, 85.

**b. Je, Yakobo anarudiaje maneno ya Kristo kuhusiana na ukweli? Yakobo 5:12; Mathayo 5:37.**

"Kila jambo wafanyalo Wakristo lapaswa kuwa dhahiri kabisa kama ulivyo mwangaza wa jua. "—*Ibid.*, p. 68.

## 2. IMANI DHIDI YA DHULUMA

**a. Ikiwa tunaugua magonjwa, ni kwa jinsi gani na kwa nini tunahimizwa kuja kwa Mtoa Uhai mkuu? Yakobo 5:13–15; Zaburi 103:1–3.**

“Mungu yuko tayari kuwarudisha wagonjwa katika afya sasa kama vile Roho Mtakatifu aliposema maneno haya kupitia mtunga-zaburi. Na Kristo ndiye tabibu yule yule mwenye huruma sasa alipokuwa wakati wa huduma yake hapa duniani. Ndani Yake mna zeri ya kuponya kila ugonjwa, na kurejesha nguvu kwa kila udhaifu. Wanafunzi wake katika wakati huu wanapaswa kuwaombea wagonjwa kama vile wanafunzi wa zamani walivyoomba. Na kupona kutafuata; kwa maana ‘kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa.’ Tuna nguvu za Roho Mtakatifu, uhakikisho tulivu wa imani, unaoweza kudai ahadi za Mungu. Ahadi ya Bwana, ‘Wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya’ (Marko 16:18), ni ya kutegemewa tu sasa kama ilivyokuwa katika siku za mitume.” —*The Ministry of Healing*, p. 226.

**b. Ni usawa gani tunapaswa kufahamu tunapotafuta afya? Zaburi 66:18.**

“Hatustahili rehema [ya Bwana], lakini tunapojitoa Kwake, Yeye hutupokea. Atafanya kazi kwa ajili na kupitia kwa wale wanaomfuata.

“Lakini tu tunapoishi kwa utiifu kwa neno Lake ndipo tunaweza kudai utimizo wa ahadi zake. Ikiwa tutamtii Yeye tu kwa sehemu, kwa moyo nusu, ahadi Zake hazitatimizwa kwetu.” —*Ibid.*, p. 227.

“Njia ambayo Kristo alifanya kazi ilikuwa ni kuhubiri neno, na kuondoa mateso kwa miujiza ya uponyaji. Lakini naagizwa kwamba hatuwezi sasa kufanya kazi kwa njia hii; kwani Shetani atatumia nguvu zake kwa kufanya miujiza. Watumishi wa Mungu leo hawangeweza kufanya miujiza, kwa sababu kazi za uwongo za uponyaji, zinazodai kuwa za kimungu, zitafanywa.

“Kwa sababu hii Bwana ameweka alama kwa njia ambayo watu wake wanapaswa kuendeleza kazi ya uponyaji wa kimwili pamoja na mafundisho ya neno. Vituo vya sanitariumu vitaanzishwa, na pamoja na taasisi hizi wataunganishwa wafanyakazi ambao wataendeleza kazi ya kweli ya kimishonari ya matibabu. Kwa hivyo ushawishi wa ulinzi unatupwa karibu na wale wanaokuja kwenye sanitariamu kwa matibabu. Huu ndio mpango ambao Bwana amefanya ambapo kazi ya umishonari wa kitabibu wa injili unapaswa kufanywa kwa ajili ya roho nyingi.” — *Medical Ministry*, p. 14.

## 3. AINA MBILI TOFAUTI ZA UJASIRI

**a. Taja kipengele muhimu cha uponyaji ambacho kinapuuzwa kwa huzuni. Yakobo 5:16**

---

---

"Wana makosa kiasi gani wale wanaofikiri kwamba kuungama dhambi kutaondoa utu wao, na kupunguza ushawishi wao miongoni mwa wanadamu wenzao. Wakishikilia wazo hili potovu, ingawa wanaona makosa yao, wengi hushindwa kuyaungama, lakini badala yake hupita makosa ambayo wamewatendea wengine, na hivyo kuhuzunisha maisha yao wenyewe, na kuficha maisha ya wengine. Haitaumiza hadhi yako kuungama dhambi zako. Achana na hadhi hii ya uwongo. Angukia Mwamba na uvunjike, na Kristo atakupa hadhi ya kweli na ya mbinguni. Usiruhusu kiburi, kujiona au kujihesabia haki kuwa mwadilifu kumzuie mtu yeyote kuungama dhambi yake, ili apate kudai ahadi. 'Afichaye dhambi zake hatafanikiwa; bali yeye aziungamaye na kuziacha atapata rehema' (Mithali 28:13). Usimzuie Mungu chochote, wala usipuuze kuungama makosa yako kwa ndugu zako. 'Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, mpate kuponywa' (Yakobo 5:16). Dhambi nyingi huachwa bila kuungama ili kumkabili mwenye dhambi katika siku ya hesabu ya mwisho; afadhali zaidi kuzikabili dhambi zako sasa, kuziungama na kuziweka mbali, wakati Sadaka ya upatanisho inakusihi kwa niaba yako. Usikose kujifunza mapenzi ya Mungu juu ya somo hili. Afya ya nafsi yako na wokovu wa wengine inategemea njia unayofuata katika jambo hili." —*Selected Messages*, bk. 1, pp. 326, 327.

**b. Alipohangaikia uasi wa kiroho wa taifa lake, Eliya alichukua hatua gani—na Mungu alimhifadhi jinsi gani? 1 Wafalme 17:1–3.**

---

---

"Kwa uchungu wa nafsi [Eliya] alimsihi Mungu awatie nguvuni wale watu waliopendelewa hapo awali katika njia yao mbaya, awatembelee kwa hukumu, ikihitajika, ili wapate kuongozwa kuona katika nuru yake ya kweli kuondoka kwao kutoka Mbinguni. Alitamani sana kuwaona wakiletwa kwenye toba kabla hawajafikia hatua ya kutenda maovu kiasi cha kumkasirisha Bwana ili awaangamize kabisa. . . .

"Kwa Eliya alikabidhiwa kazi ya kuwasilisha kwa Ahabu ujumbe wa Mbinguni wa hukumu…. Katika ikulu hakuomba kiingilio, wala kusubiri kutangazwa rasmi. Akiwa amevaa mavazi chakavu ambayo kwa kawaida huvaliwa na manabii wa wakati huo, aliwapita walinzi, bila kuonekana, na kusimama kwa muda mbele ya mfalme aliyeshangaa."—*Prophets and Kings*, pp. 120, 121.

## 4. KUJIFUNZA KUTOKA KWA ELIYA

**a. Kwa nini maombi ya Eliya kwa Mungu yaliamsha taifa lake lililoasi yametolewa kuwa kielelezo kwetu? Yakobo 5:17.**

"Ombi la kurudiwa-rudiwa, maonyo, na pingamizi yalishindwa kuleta Israeli kwenye toba. Wakati ulikuwa umefika ambapo lazima Mungu aseme nao kwa njia ya hukumu. Kwa kuwa waabudu wa Baali walidai kwamba hazina za mbinguni, umande na mvua, havikutoka kwa Yehova, bali kutoka kwa nguvu zinazotawala za asili, na kwamba ni kupitia nishati ya uumbaji ya jua kwamba dunia ilitajirishwa na kufanywa. ili kuzaa kwa wingi, laana ya Mungu ilikuwa kutulia sana juu ya nchi iliyochafuliwa. Makabila yaliyoasi ya Israeli yangeonyeshwa upumbavu wa kutegemea nguvu za Baali kwa ajili ya baraka za muda. Mpaka wamgeukie Mungu kwa toba, na kumkiri Yeye kama chanzo cha baraka zote, haitaanguka juu ya nchi, hakuna umande wala mvua."—*Prophets and Kings*, p. 120.

**b. Baada ya Israeli kufanya upya imani yao kwa Mungu, ni kwa jinsi gani maombi ya Eliya ni mfano kwetu? Yakobo 5:18; 1 Wafalme 18:39–45.**

"Mara sita [Eliya] aliomba kwa bidii, na bado hapakuwa na dalili kwamba ombi lake lilikubaliwa, lakini kwa imani yenye nguvu alihimiza ombi lake kwa kiti cha neema. Lau angekata tamaa kwa mara ya sita, maombi yake yasingejibiwa, lakini alivumilia mpaka jibu likaja. Tunaye Mungu ambaye sikio lake halijaziba maombi yetu; na tukithibitisha neno Lake, ataheshimu imani yetu. Anataka sisi maslahi yetu yote yaunganishwe na masilahi Yake, na ndipo anaweza kutubariki kwa usalama; kwa maana basi hatutajiletea utukufu wakati baraka ni yetu, bali tutatoa sifa zote kwa Mungu. Mungu huwa hajibu maombi yetu mara ya kwanza tunapomwita; kwani akifanya hivi, tunaweza kuichukulia kirahisi kuwa tulikuwa na haki ya baraka na neema zote alizotupa. Badala ya kuchunguza mioyo yetu ili kuona kama uovu wowote ulikaribishwa na sisi, dhambi yoyote iliyofanywa, tunapaswa kuwa wazembe, na kushindwa kutambua utegemezi wetu Kwake, na haja yetu ya msaada Wake.

"Eliya alijinyenyekeza mpaka akawa katika hali ambayo hatajitwalia utukufu huo. Hili ndilo sharti ambalo juu yake Bwana husikia sala, kwa maana ndipo tutakapotoa sifa Kwake."—T*he SDA Bible Commentary [E. G. White Comments]*, vol. 2, pp. 1034, 1035.

## *Alhamisi* — *Desemba 26*

### 5. KUENDELEZA HURUMA KAMA YA KRISTO

**a. Katikati ya kujawa na kukata tamaa juu yetu na watu wenye kasoro katika ulimwengu ulioanguka, Yakobo anafunga barua yake kwetu kwa ombi gani la mwisho? Yakobo 5:19, 20**

---

"Usimpe mkosaji nafasi ya kuvunjika moyo. Usikubali ugumu wa Kifarisayo kuingia na kumdhuru ndugu yako. Usiruhusu dhihaka za uchungu ziingie akilini au moyoni. Usiruhusu dharau yoyote ionekane katika sauti. Ikiwa unazungumza neno lako mwenyewe, ikiwa unachukua mtazamo wa kutojali, au kuonyesha mashaka au kutoamini, inaweza kuthibitisha uharibifu wa nafsi. Anahitaji ndugu mwenye moyo wa huruma wa ndugu huyo ili kuugusa moyo wake wa ubinadamu. Hebu ahisi mguso wenye nguvu wa mkono wenye huruma, na asikie kunong'ona, Tuombe. Mungu atawapa uzoefu mzuri ninyi nyote wawili. Maombi yanatuunganisha sisi kwa sisi na kwa Mungu. Maombi humleta Yesu kando yetu, na kuipa roho iliyozimia, iliyofadhaika nguvu mpya ya kuushinda ulimwengu, mwili, na shetani. Maombi hugeuza kando mashambulizi ya Shetani.

"Mtu anapoacha kutokamilika kwa kibinadamu na kumtazama Yesu, mabadiliko ya kiungu hufanyika katika tabia. Roho wa Kristo akifanya kazi juu ya moyo huufananisha na sura yake. Basi acha iwe juhudi yako kumwinua Yesu. Hebu jicho la akili lielekezwe kwa 'Mwana-Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu. Yohana 1:29. Na unaposhiriki katika kazi hii, kumbuka kwamba 'yeye amrejezaye mwenye dhambi hata atoke katika upotevu wa njia yake, ataokoa roho na mauti, na kuficha wingi wa dhambi.' Yakobo 5:20 . . . .

"Katika msamaha wa Mungu moyo wa mkosaji unavutwa karibu na moyo mkuu wa Upendo usio na kikomo. Wimbi la huruma ya kimungu hutiririka ndani ya nafsi ya mtenda-dhambi, na kutoka kwake hadi kwa nafsi za wengine." — *Christ's Object Lessons,* pp. 250, 251.

## *Ijumaa* — *Desemba 27*

### MASWALI TAFAKARI BINAFSI

**1. Ni nyakati gani katika maisha yangu nimeona rehema nyingi za Mungu kwangu?**


**2. Ni kwa njia zipi ninaweza kuwa na hatia ya kudhani kuhusu afya yangu?**

**3. Sala ya Eliya kwa ajili ya taifa lake ilijibiwaje?**

**4. Kwa nini Eliya alihitaji kusali mara nyingi sana ili mvua irudi?**

**5. Ninapaswa kuwa na mtazamo wa huruma zaidi na nani, na kwa nini?**

# Sadaka za Sabato ya Kwanza




## Oktoba, 05

Kwa ajili ya kanisa dogo lililoko Reading, Pennsylvania, Marekani

(Angalia, Uk. 4)

## Novemba, 02

Kwa ajili ya GC Idara ya Fasihi

(Angalia, Uk. 25)







## Desemba, 07

Kwa ajili ya Kwa ajili ya Makao Makuu ya Union ya Kolombia

(Angalia, Uk. 51)